ORODHA YA WAJUMBE WA BARAZA LA WAWAKILISHI ZANZIBAR

MHE. PANDU AMEIR KIFICHO - SPIKA

1. Mhe. Ali Abdalla Ali	Naibu Spika/Jimbo la Mfenesini.
2. Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa	Mwenyekiti wa Baraza Jimbo la Kikwajuni.
3. Mhe. Mgeni Hassan Juma	Mwenyekiti wa Baraza/ Nafasi za Wanawake.
4. Mhe. Balozi Seif Ali Iddi	MBM/Makamu wa Pili wa Rais/Kiongozi wa Shughuli za Serikali/Kuteuliwa na Rais.
5. Mhe. Dr. Mwinyihaji Makame Mwadini	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais Ikulu na Utawala Bora/ Jimbo la Dimani.
6. Mhe. Omar Yussuf Mzee	MBM/Waziri wa Fedha/ Kuteuliwa na Rais.
7. Mhe. Haji Omar Kheri	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ/Jimbo la Tumbatu.
8. Mhe. Fatma Abdulhabib Fereji	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais/Kuteuliwa na Rais.
9. Mhe. Mohammed Aboud Mohammed	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais/ Kuteuliwa na Rais.
10.Mhe. Abubakar Khamis Bakary	MBM/Waziri wa Katiba na Sheria/Jimbo la Mgogoni.
11. Mhe. Rashid Seif Suleiman	MBM/ Waziri wa Afya/ /Jimbo la Ziwani.
12.Mhe. Ramadhan Abdalla Shaaban	MBM/Waziri wa Ardhi, Maakazi, Maji na Nishati/ Kuteuliwa na Rais.
13.Mhe. Juma Duni Haji	MBM/Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Kuteuliwa na Rais.
14.Mhe. Zainab Omar Mohammed	MBM/Waziri wa Uwezeshaji, Ustawi wa Jamii, Vijana, Wanawake na Watoto/Kuteuliwa na Rais.
15.Mhe. Abdillah Jihad Hassan	MBM/Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Magogoni.
16.Mhe. Ali Juma Shamuhuna	MBM/Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Jimbo la Donge.
17.Mhe Dr. Sira Ubwa Mamboya	MBM/Waziri wa Kilimo na Maliasili/Kuteuliwa na Rais.
18.Mhe. Nassor Ahmed Mazrui	MBM/Waziri wa Biashara,

	Viwanda na Masoko/Jimbo la Mtoni.
19.Mhe. Said Ali Mbarouk	MBM/Waziri wa Habari, Utamaduni Utalii na Michezo/Jimbo la Gando.
20.Mhe. Haroun Ali Suleiman	MBM/Waziri wa Nchi, Ofisi Ya Rais, Kazi na Utumishi wa Umma/Jimbo la Makunduchi.
21.Mhe. Haji Faki Shaali	MBM/ Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Mkanyageni.
22.Mhe. Machano Othman Said	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Chumbuni.
23. Mhe. Shawana Bukheit Hassan	MBM/Waziri Asiekuwa na Wizara Maalum/Jimbo la Dole.
24. Mhe. Issa Haji Ussi (Gavu)	Naibu Waziri wa Miundombinu na Mawasiliano/Jimbo la Chwaka.
25. Mhe. Zahra Ali Hamad	Naibu Waziri wa Elimu na Mafunzo ya Amali/Nafasi za Wanawake.
26.Mhe.Mahmoud Thabit Kombo	Naibu Waziri wa Afya/ Jimbo la Kiembesamaki
27.Mhe. Bihindi Hamad Khamis	Naibu Waziri wa Habari, Utamaduni,Utalii na Michezo/ Nafasi za Wanawake.
28.Mhe. Haji Mwadini Makame	Naibu Waziri wa Ardhi, Makaazi, Maji na Nishati/ Jimbo la Nungwi.
29.Mhe. Thuwaybah Edington Kissasi	Naibu Waziri wa Biashara, Viwanda na Masoko/Jimbo la Fuoni.
30.Mhe. Mohammed Said Mohammed	Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi/Jimbo la Mpendae.
31.Mhe. Mtumwa Kheir Mbarak	Naibu Waziri wa Kilimo na Maliasili/Nafasi za Wanawake.
32.Mhe. Said Hassan Said	Mwanasheria Mkuu.
33.Mhe. Abdalla Juma Abdalla	Jimbo la Chonga
34.Mhe. Abdalla Moh'd Ali	Jimbo la Mkoani
35.Mhe. Abdi Mosi Kombo	Jimbo la Matemwe
36.Mhe. Ali Mzee Ali	Kuteuliwa na Rais

37.Mhe. Ali Salum Haji	Jimbo la Kwahani
38.Mhe. Amina Iddi Mabrouk	Nafasi za Wanawake
39.Mhe. Asaa Othman Hamad	Jimbo la Wete
40.Mhe. Asha Abdu Haji	Nafasi za Wanawake
41.Mhe. Asha Bakari Makame	Nafasi za Wanawake
42.Mhe. Ashura Sharif Ali	Nafasi za Wanawake
43.Mhe. Bikame Yussuf Hamad	Nafasi za Wanawake
44.Mhe. Farida Amour Mohammed	Nafasi za Wanawake
45.Mhe. Fatma Mbarouk Said	Jimbo la Amani
46.Mhe. Hamad Masoud Hamad	Jimbo la Ole
47.Mhe. Hamza Hassan Juma	Jimbo la Kwamtipura
48.Mhe. Hassan Hamad Omar	Jimbo la Kojani
49.Mhe. Hija Hassan Hija	Jimbo la Kiwani
50.Mhe. Hussein Ibrahim Makungu	Jimbo la Bububu
51.Mhe. Ismail Jussa Ladhu	Jimbo la Mji Mkongwe
52.Mhe. Jaku Hashim Ayoub	Jimbo la Muyuni
53.Mhe. Kazija Khamis Kona	Nafasi za Wanawake
54.Mhe. Makame Mshimba Mbarouk	Jimbo la Kitope
55.Mhe. Marina Joel Thomas	Kuteuliwa na Rais
56.Mhe. Mbarouk Wadi Mussa (Mtando)	Jimbo la Mkwajuni
57.Mhe. Mlinde Mabrouk Juma	Jimbo la Bumbwini
58.Mhe. Mohammed Haji Khalid	Jimbo la Mtambile
59.Mhe. Mohamedraza Hassanali Mohamedali	Jimbo la Uzini
60.Mhe. Mohammed Mbwana Hamadi	Jimbo la Chambani
61.Mhe. Mussa Ali Hassan	Jimbo la Koani
62.Mhe. Mwanaidi Kassim Mussa	Nafasi za Wanawake
63.Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi	Nafasi za Wanawake
64.Mhe. Nassor Salim Ali	Jimbo la Rahaleo

65.Mhe. Omar Ali Shehe	Jimbo la Chake-Chake
66.Mhe. Panya Ali Abdalla	Nafasi za Wanawake
67.Mhe. Rufai Said Rufai	Jimbo la Tumbe
68.Mhe. Raya Suleiman Hamad	Nafasi za Wanawake
69.Mhe. Saleh Nassor Juma	Jimbo la Wawi
70.Mhe. Salim Abdalla Hamad	Jimbo la Mtambwe
71.Mhe. Salma Mohammed Ali	Nafasi za Wanawake
72.Mhe. Salma Mussa Bilali	Nafasi za Wanawake
73.Mhe. Salmin Awadh Salmin	Jimbo la Magomeni
74.Mhe. Shadya Mohamed Suleiman	Nafasi za Wanawake
75.Mhe. Shamsi Vuai Nahodha	Jimbo la Mwanakwerekwe
76.Mhe. Subeit Khamis Faki	Jimbo la Micheweni
77.Mhe. Suleiman Hemed Khamis	Jimbo la Konde
78.Mhe. Suleiman Othman Nyanga	Jimbo la Jang'ombe
79.Mhe. Ussi Jecha Simai	Jimbo la Chaani
80.Mhe. Viwe Khamis Abdalla	Nafasi za Wanawake
81.Mhe. Wanu Hafidh Ameir	Nafasi za Wanawake

Ndugu Yahya Khamis Hamad **Katibu wa Baraza la Wawakilishi**

MKUTANO WA KUMI NA SABA

Kikao cha Saba - Tarehe 30 Oktoba, 2014

(Kikao kilianza saa 3.00 Asubuhi)

DUA

Mhe.Naibu Spika,(Ali Abdalla Ali) alisoma Dua

HATI ZA KUWASILISHA MEZANI

Mhe. Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa Nam. 1 ya mwaka 1998 na Kuanzisha Upya Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 2014 na Mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria:

Hotuba ya Uwasilishaji wa Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa Nam. 1 ya Mwaka 1998 na Kuanzisha upya Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 na mambo Mengine yanayohusiana na hayo.

MASWALI NA MAJIBU

Nam. 44

Matatizo la Baa ya Kienyeji Iliyopo Wawi na Matendo Maovu Yanayofanyika Katika Eneo Hilo

Mhe. Saleh Nassor Juma - Aliuliza:-

Tatizo la baa ya kienyeji iliyopo *Fidel Castro* katika Jimbo la Wawi maarufu "Mochwari" ni tatizo nyeti linaloathiri jamii nzima ya Jimbo la Wawi pamoja na vitongoji vyake vyote. Kwa kuwa Uhalifu, Wizi, Ngono zembe pamoja na matendo mengi ya Kiharamia hufanyika katika eneo zima la Jimbo la Wawi kupitia baa hiyo ya Mochwari, na kwa tatizo hili tayari nimeshalipigia kelele sana kupitia Wizara mbali mbali na hadi hii leo halijapatiwa ufumbuzi licha ya ahadi iliyotolewa ya kulishughulikia.

Je, ni lini Serikali kupitia vyombo vya *ULINZI* likiwemo Jeshi la Wananchi *TPDF*, Jeshi la Polisi Tanzania pamoja na vikosi vyote vya SMZ vitaendesha "*OPERESHENI TOKOMEZA GONGO, BANGI, UNGA* na *NGONO ZEMBE*" katika eneo lote la Mochwari.

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, kwa idhini yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi swali lake Nam. 44 kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, Jeshi la Polisi linafahamu fika kuwepo na kujikita kwa uhalifu katika eneo linalofahamika kama Mochwari huko *Fidel Castro* katika Jimbo la Wawi. Kwa kiasi kikubwa uhalifu huo umekuwa ukitokana na kushamiri kwa biashara ya pombe za kienyeji na dawa za kulevya na bangi.

Mhe. Naibu Spika, Jeshi la Polisi Mkoa wa Kusini Pemba katika harakati za kupambana na uhalifu na wahalifu na kwa kufahamu kwamba hilo la Mochwari ni miongoni mwa maeneo sugu, hivyo Jeshi la Polisi limeanzisha Operesheni maalum za nguvu na za mara kwa mara kwa nia ya kukomesha uhalifu huo.

Mhe. Naibu Spika, pamoja na jitihada hizo Jeshi la Polisi kwa kujua hali hiyo limeamua kushirikiana na kikundi cha Ulinzi Shirikishi cha Vitongoji na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama kwa nia ya kuwa na operesheni endelevu hadi zitakapomalizika kabisa kero za uhalifu katika eneo hilo, tunawaomba sana raia wema waendelee kutoa

ushirikiano kwa Jeshi lao la Polisi katika kupambana na uhalifu ili kukomesha vitendo viovu katika eneo hilo na nchi nzima.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Waziri naomba kuuliza suala moja la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Mochwari inaendelea kuuza gongo, bangi pamoja na ulevu wa kila aina miaka kadhaa iliyopita, na kwa kuwa Jeshi la Polisi lipo na vyombo vyengine vya ulinzi vipo na vimeshakwenda mara kadhaa pale lakini huwatia watu hatiani lakini baada ya muda unawaona wanarudi pale pale huku wakiwa kifua mbele na kuendeleza biashara yao.

Je, kuendelea kuuza gongo wale na huku wakiwa kifua mbele si kuitia fedheha Serikali yetu kwa wale kujifanya wao washindi, hili la kwanza.

La pili, kwa kuwa lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ni mambo haya kupunguza umasikini pamoja na kuengezea kipato wananchi wa nchi hii, na kwa kuwa wananchi wa pale Wawi na Vitongoji vyake wameekeza maisha yao katika mifugo wakiwamo ng'ombe, kuku na mbuzi, na kwa kuwa mifugo yao inaibiwa hivi hivi na kuuzwa pale Mochwari, tena ukifika pale unakuta nyama tu kichwa hukioni wala ngozi huioni.

Mhe. Naibu Spika, suali Mheshimiwa.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Sasa suala langu je, huku kuruhusu wale na kuuza gongo na kutuibia ng'ombe zetu huku ndio kuwapunguzia watu umasikini, au kuongezea.

Na (c) kwa kuwa wanafunzi ni *curious in nature, they want to know more than that they know*. Kwa sababu wanafunzi ni watu wanaopenda penda sana kuonja mambo na kwa sababu kule Fidel Castro kuna wanafunzi wa kike na wanafunzi wa kiume, je, wakija wakiona gongo wakionja kidogo, wakiona walevi wakiwakamata kamata kidogo hatutawaingiza hawa wanafunzi katika matendo mabaya ikiwemo kunywa pombe pamoja na ngono uzembe.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Naibu Spika, kwanza nataka nimuhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi na wananchi wote wa Jimbo la Wawi na nchi kwa jumla, kwamba Serikali haiwezi kushindwa na vitendo vinavyofanywa na wahalifu kwa nia ya kuharibu silka, utamaduni na mazingira yetu na kuchafua jina zuri la nchi yetu. Hivyo nataka nimhakikishie kwamba wahalifu hao hawatokuwa na nafasi; tutapambana nao kuhakikisha kwamba tunaondosha aina yoyote ya uhalifu. Kama wao ni Mochwari basi tutawatafutia Mochwari halisi ambayo wataridhika na Mochwari hiyo. Nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mwakilishi kwamba nina mpango wa ziara ya kwenda Pemba Wiki ijayo, nataka kwenda nione hilo eneo, tuone nani hao wenye nguvu ya kufanya hivyo.

Kuhusu suala la wizi wa mifugo Mheshimiwa hatukubaliani kabisa kwenye suala zima la wizi wa mifugo; kwa kuwa tunajua wananchi wetu miongoni mwa sehemu moja wanayotegemea katika maisha yao ni mifugo ambayo wanaifuga. Kwa hivyo wanapotokea wahalifu kwenda kuiba mifugo ili wauze nyama zake huko kwenye maklabu ya pombe ambayo hayako kihalali na hao namhakikishia kwamba tutapambana nao na tutafuatilia kwa karibu zaidi. Nitaonana na RPC wa Mkoa wa Kusini Pemba leo tuzungumze nijue nini kinachoendelea.

Ni kweli kama kunatokea uhalifu jirani na pana shule nzuri kama ile ya *Fidel Castro* vijana wetu kwa kupita pita pale wanaweza kuona mambo ambayo wanaweza kupendelea kuyafanya, kitu ambacho ni kinyume kabisa na mila na desturi za nchi hii. Hivyo tutaendelea kupambana na hali hiyo ili kuondoa kabisa eneo hilo katika maeneo hayo, kuwahakikishia wanafunzi wetu wanasoma katika utulivu ili waweze kutimiza lengo lao lililokusudiwa la kwenda shule na kupata elimu bora.

Mhe. Shadya Mohammed Suleiman: Ahsante sana Mheshimi Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii ya kuweza kumuuliza Mheshimiwa Waziri suala moja la nyongeza.

Mhe. Waziri kwa kuwa jeshi la Polisi mara kadhaa hufika Mochwari na kukamata vifaa vya kupikia gongo na kuwaweka kizuizini baadhi ya watuhumiwa. Je, kwa nini kesi zao huwa hazifiki Mahakamani.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Mhe. Shadya suala lake kama nimelisikia vizuri kwa kuwa ningependa sana Waheshimiwa Wawakilishi wanaposema wazungumzie kwenye spika hii ukigeuka kidogo hivi basi unashindwa kufahamu nini unachokisema.

Lakini kama nimemuelewa ni kwamba Jeshi la Polisi linakamata hawa watu na linavifikisha vitu mbali mbali vinavyohusiana na uhalifu huo Mahakamani na baadae Mahakama ima haichukui hatua zinazofaa kwa maana ya maelezo ya Mheshimiwa Mwakilishi, kwa kuwa chombo hiki hakiwezi kuingilia suala la Mahakama nataka kuwasiliana na Jeshi la Polisi nijue ni sababu zipi zilizofanya kesi hizi zinazokamatwa katika eneo hilo haziendelei, na vile vile nitahakikisha nimewasiliana na Jaji Mkuu ili baada ya kupata taarifa za Polisi kueleza hilo linaloendelea, kwa kuwa Chombo cha Mahakama haina uwezo wa kuingiliwa na Baraza hili.

Mhe. Naibu Spika, suala la mwisho dogo Mheshimiwa Rufai Said Rufai!

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Naibu Spika, nashukuru kupata nafasi hii, napenda kumuuliza suala dogo tu Mheshimiwa Waziri kama lifuatavyo:-

Kwa kuwa hivi karibuni misikiti ya Ijumaa uliyomo katika jimbo la Wawi waliandaa kwenda kulivamia eneo lile katika kuondosha tu haya mambo wanayoyafanya, lakini viongozi wakaliingilia kati suala lile na bado kunaendelea ukimya. Je, Mhe. Waziri huoni kimya hiki kinaweza kusababisha matatizo mengine makubwa zaidi.

Mhe. Waziri wa Nchi Afisi ya Makamo wa Pili wa Rais: Ni kweli vitendo kama hivyo vinaweza kusababisha wananchi kuchukua sheria mikononi mwao ambalo si jambo tunalotarajia lifanyike. Kwa hivyo ningewaomba sana wazee wangu wawe na subra wakati Serikali kupitia jeshi la Polisi tunalishughulikia jambo hili.

Nataka niwahakikishie kwamba nitahakikisha nimekwenda Pemba nipate taarifa za ziada kuhusu jambo hili, tushirikiane vizuri na jeshi la Polisi na vyombo vyengine vya ulinzi na usalama, ili tuhakikishe kwamba Mochwari hii tunaizika na haitokei kuharibu mila na dasturi na utamaduni wa nchi yetu.

Matengenezo ya Kipimo cha CT SCAN

Mhe. Saleh Nassor Juma (Kny.Jaku Hashim Ayoub) - Aliuliza:-

Mashine ya kipimo cha *CT Scan* kwa muda mrefu imekuwa na matatizo ya kiufundi na kulazimika wagonjwa kutafuta huduma hiyo nje ya Zanzibar na kusababisha kero na usumbufu mkubwa kwa wananchi wanyonge ambao hawana uwezo wa kumudu gharama za kutafuta huduma hiyo nje ya Zanzibar.

(a) Kama mashine hiyo bado ni mbovu lini itafanyiwa matengenezo ili huduma hiyo irudi tena na kupatikana kwa uhakika.

(b) Kwa kuwa tatizo hilo ni la muda mrefu bila ya kupatiwa ufumbuzi ni lini Serikali itatafuta ufumbuzi wa kudumu ikiwamo kutafuta mashine nyengine.

(c) Kwa kuwa Hospitali ya Mnazi Mmoja ipo katika mpango wa kuwa Hospitali ya Rufaa Zanzibar, mpaka hivi sasa ina wataalamu wangapi wa kusoma mashine hiyo na imejipangaje kuhakikisha vipimo muhimu vya kimaabara vinapatikana wakati wote.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya - Alijibu:-

Mhe. Spika, kwa ruhusa yako naomba kumjibu Mhe. Mwakilishi wa Baraza lako tukufu swali lake Nam. 68 lenye vifungu (a), (b) na (c) kama hivi ifuatavyo:-

a) Mheshimiwa Spika, naomba kulitangazia Baraza lako tukufu kwamba mashine ya *CT SCAN* tayari imeshatengenea na hivi sasa inafanya kazi. Hapo awali mashine haikuwa mbovu kwa sababu bado ni mpya na ipo katika upya ila vifaa vyake; kifaa kimoja cha ku-*print* zile picha kilikwisha wino ambao ni ghali sana, kama vile kwenye *printer* kuna *toner cartridge* basi na kifaa hicho pia kimo katika mashine ya *CT SCAN* wakati kinachapa zile

picha, na huwa kinakwisha kila baada ya *round* kama eflu kumi za picha zile huwa kinakwisha ule wino na kumalizika.

Na kifaa hicho bei yake ni kubwa sana yaani hiyo *toner cartridge* ni dola za kimarekani elfu thamanini na tatu, kwa hivyo huwezi kuweka *stock* au *spare* na pia zinakuwa na *Expire date*. Kwa hivyo naomba kulitangazia Baraza lako tukufu Mheshimiwa, kwamba Mashine ya *CT SCAN* imeshatengenea na wagonjwa tayari wameshaanza kupatiwa huduma hiyo.

(b) Kama nilivyoeleza hapo awali tatizo ni repressment na wakati mwengine hutokea tatizo la hapa na pale la kifedha kwa sababu pesa anazochangia mgonjwa kwenye ile mashine hazikizi haja hata kununua hii *toner*. Kwa hivyo makusanyo yote hayafikii kiwango kinachohitajika kwa *tonner* kwa sababu huduma zile zinachangiwa pia na Serikali.

(c) Mhe. Naibu Spika**,** napenda kuliarifu Baraza lako tukufu la Wawakilishi kwamba kwa hivi sasa Wizara ina wataalam 3, yaani *radio*graphers wa kusoma ripoti za mashine hiyo ya *CT SCAN*, wawili ni wazalendo na mmoja ni mtaalamu ambaye tunasaidiwa na Serikali ya watu wa China ambaye yuko pale anafanya kazi na hawa wazalengo na wakati huo huo akiendelea kutoa huduma hizo.

Radiographer ni *field* ambayo ghali kidogo na wanalipwa fedha nyingi duniani. Hawa *radiographers* waliokuwa wataalam, wakifikia kiwango cha juu kabisa wanaitwa *Consultant radiographers*. Sasa jitihada za kuwasomesha wengine kupitia misaada mbali mbali tunayopokea kupitia nchi mbali mbali zinaendelea na tunatarajia kwamba tutapata siku zijazo wawili ambao wataweza kusoma mashine kama hiyo na nyenginezo. Ahsante sana

Mhe. Saleh Nassor Juma: Ahsante sana Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana na yenye ufafanuzi wa hali ya juu aliyotoa Mheshimiwa Naibu Waziri, naomba kuuliza suala dongo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Kwa kuwa Wazanzibari tuliopo sasa *population density* yetu ni *nearly* 1.5 *million*, na kwa kuwa sote sisi tunahudumiwa na *CT SCAN* mmoja na kwa mujibu nadharia zinaonesha kwamba haya mambo ya *electronics* hususan haya mambo ya *radiation* haya yanayohusika na mambo ya mionzi yana nguvu za kufanya *radiation per unit time* na hivyo kuilazimisha *CT SCAN* kufanya kazi ya ziada ni kuunguza hiyo *tube* ya wino ambayo ni karibu milioni thamanini na tano. Je, ni lini Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar itaipunguzia kazi hiki kisiji-*scan* kimoja kilichopo hapa Mnazi Mmoja kwa kuweka *CT Scan* nyengine katika kisiwa kile cha Pemba, ili ile *queue* kutoka Pemba isiizidi nguvu hapa, watibiwe kule kule Pemba.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, nitaomba nirekebishe kidogo takwimu zake. La kwanza kabisa kutokana na sensa iliyomalizika wakaazi ama *population* ya Zanzibar yote ni 1.3 *million* sio 1.5 ni milioni 1.33. Kwa hivyo kidogo amezidisha wananchi kama laki mbili hapa ambao ni wengi zaidi kuliko sensa iliyofanyika.

Lakini la pili, naomba nimjibu pia kwamba *CT Scan* hii tuliyokuwa nayo bado haikuzidiwa na kazi, umenikumbusha sana lile suala la jana la hospitali ya wale wagonjwa wa akili wa kule Pemba, kwa sababu hakuna watu wenye matatizo ya ugonjwa wa akili au wendawazimu basi hakukuwa na haja ya kujenga. Kwa hivyo kwa *CT Scan* hii bado inatosheleza huduma zote kwa Unguja na Pemba na haijazidiwa bado.

Nimechukua mfano mmoja ambao nimeupata katika *research* ndogo nilichukua hospitali moja ya Apolo nchini India, ambayo ina uwezo wa kutibu wagonjwa elfu nane kwa siku. Wao wana *CT Scan* moja tu na sisi hatujafikia kiwango hicho hata kidogo.

Lakini jengine huduma za *CT Scan* hazihitajiki kwa kila mtu katika *population*. Kwa siku kesi za *CT Scan* zinakuwa baina ya kumi mpaka 20 kwa hivyo bado mashine haikuzidiwa. Lakini pia naomba nirekebishe kauli ya kwamba hii *tube* ya *toner tube* ilizidiwa, haikuzidiwa ilifikia wakati wake imeshatoa picha za kutosha. Kwa hivyo muda wake wa ku-*expire* au kwisha ule wino ulifikia na hapo ndipo ulipomalizika.

Sasa sisi tunatakiwa tu-*stock* kama *toner* mbili au tatu kama *spare* ili ikimalizika moja, unatumia nyengine. Lakini dola hizo elfu thamanini na tatu mara tatu nadhani ukipiga hesabu utapata karibu laki mbili na nusu dola, si rahisi ku-*stop* vifaa vyenye bei kubwa kama hiyo.

Kwa hivyo naomba nilihakikishie Baraza lako Tukufu kwamba *CT Scan* hiyo bado haijazidiwa na tunapokea wagonjwa mbali mbali kutoka Pemba ambao wanakuja pale. Itakapoonekana kwamba kuna ziada ya wagonjwa kutoka Pemba na itakapo-*justify* kuwa na *CT Scan* naamini wakati huo Wizara pamoja na Serikali itafanya maamuzi ya ku-*invest,* kwa sababu si *investment* ndogo ni *investment* kubwa. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Ali Salum Haji: Ahsante Mhe. Naibu Spika, wakati Mhe. Naibu Waziri anajibu swali lake mama alisema kwamba tatizo lililojitokeza katika mashine ya *CT Scan* ni kifaa hiki cha *toner tube* kumaliza muda wake. Swali langu liko hapa kwa kuwa Wizara inafahamu kwamba kifaa hiki kina muda wa ku-*expire*, mimi nilitaka kujua kwamba kifaa hiki kina uwezo wa kufanya kazi kwa idadi ya wagonjwa wangapi mpaka ku-*expire* kwake. Na ni kiasi gani cha fedha ambacho kinaweza kukusanywa kutokana na hiyo idadi ya wagonjwa ambao wanafanyiwa kazi katika kipindi hicho cha kuanza kwake mpaka ku-*expire* kwake.

Jibu (b) Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa Wizara inafahamu hili je, Wizara ina mikakati gani ya kutenga fedha ambazo zinaonekana kwamba zile zinazokusanywa hazitoshelezi ili kukabiliana na tatizo hilo.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, siwezi kusema wagonjwa wangapi kwa sababu ile *tube* haifanyi kazi kwa idadi ya wagonjwa, inafanya kazi kwa idadi ya picha. Kwa hivyo baada ya picha elfu kumi kwa sababu mgonjwa mmoja anaweza akapigwa picha tano, mgonjwa huyo huyo mmoja anaweza akapigwa picha kumi, inategemea zile *slides* za daktari anavyoagizia.

Kwa hivyo mgonjwa huyo huyo mmoja unaweza kukuta ana *slides* mpaka ishirini. bei ni hiyo hiyo ambayo inatozwa pale Mnazi Mmoja na kwa aliyekuwa hana uwezo tuna utaratibu maalum ambao upo pale umeandaliwa anakwenda anaji-*register* inathibitishwa kwamba huyu hana uwezo, pale Serikali inachangia huduma zile.

Kwa hivyo ni baada ya picha elfu kumi kama wino wa *printer* unavyokwisha vile basi na hiyo *tube* baada ya picha elfu kumi nayo inamalizika kazi yake. Yaani ishakuwa *over heated;* wino ushakwisha hata picha pale hazitokei vizuri zinatokea kama zinaungua. Kwa hivyo hilo nadhani sio wagonjwa bali ni idadi ya picha.

Makusanyo yote yanayofanyika pale ni kati ya milioni ishirini mpaka thalathini mpaka hiyo *tube* moja iishe. Ukipiga kwa hesabu ya dola ni takriban dola elfu ishirini haizidi dola elfu ishirini. Kifaa kile ni dola elfu thamanini na tatu mbali ya *services* ambapo ni kama dola elfu tano. Sasa Serikali inachangia takriban dola elfu sitini, yaani karibu milioni mia moja Serikali inachangia kwa wagonjwa wake. Kwa hivyo kinachokusanywa pale hakitoshelezi kabisa Mheshimiwa naomba nikuhakikishie kutokana na hali za wananchi wetu; hali zao kuwa duni wengine hawawezi ku-*afford* laki moja au laki moja na nusu kwa hivyo hilo halijawezekana kufanyika kwa sababu Serikali inachangia.

Wenzetu Tanzania Bara wao wana-*charge* na kidogo bei yao ni kubwa zaidi kuliko sisi hapa na utaratibu wa kule kupatiwa huduma ya bure kidogo mgumu zaidi kuliko ulivyo kwetu sisi hapa. Kwa hivyo naomba majibu hayo yakidhi kusema kwamba fedha tunazokusanya pale mashine ile haifanyi kazi kibiashara yaani kuwe na faida, inakusanya fedha lakini zile fedha hazitoshi kabisa na tunapeleka kunakohusika hizo fedha na baadae tunaomba huko huko.

Naomba nimshukuru sana Waziri wa Fedha Mhe. Omar Yussuf Mzee pamoja na Katibu Mkuu pamoja na wafanyakazi wote wa Wizara ya Fedha tulihangaika nao sana kupatikana dola hizi thamanini na tatu elfu baada ya uongozi kuingia tu na wao walitusaidia kwa karibu sana; ndio hicho kifaa kikapatikana. Na wale wanaotoa vifaa vile hawataki tena kutukopesha wanataka *cash*, ukiwapa pesa na wao wanakupa kifaa ni Kampuni Seamans. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Omar Ali Shehe: Ninashukuru Mhe. Naibu Waziri kwa kunipa fursa hii ili nimuulize Mhe. Naibu Waziri swali dogo la nyongeza kama ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, kwa muda mrefu hospitali zetu zimekuwa zikikabiliwa na matatizo makubwa ya kuharibika mara kwa mara kwa vifaa hivi vya kielektroniki, kama vile *CT Scan, EX Rays* na kadhaa wa kadhaa. Msingi mkubwa wa matatizo haya Mhe. Naibu Spika, ni tatizo la ama kukosa wataalam au kuwa na wataalam ambao wana ujuzi mdogo, uwezo mdogo kwa matumizi ya vifaa hivyo.

Swali langu ni hili, Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba tunakuwa na wataalamu wenye viwango vinavyoridhisha katika matumizi ya vifaa hivyo na vile vile Serikali ina mpango gani wa kuhakikisha kwamba wataalamu hawa watakaopatikana wanabakia katika matumizi ya vifaa hivyo kwa maslahi ya wananchi wetu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, naomba nikubali kwamba *diagnostic* yaani uchunguzi ule wa mgonjwa ni tatizo ulimwengu mzima, sasa hivi kwa sababu nusu ya matibabu kugunduwa tatizo, lile tatizo kugunduliwa ndio nusu ya matibabu. Matibabu yanayofuata baada ya hapo ni kutibu yale matatizo yenyewe.

Sasa tatizo la *diagnostic* sio hpa ni ulimwengu mzima na kila siku *research* zinaendelea kufanyika katika kugundua mashine mpya mpaka hizi za *nuclear technology* sasa hivi kuna mashine za *nuclear technology* za kutibu mifupa ama *cancer* ya mifupa; mionzi ambayo inafika kwenye mifupa moja kwa moja zinaendelea kufanyiwa *research* ulimwenguni.

Kwa hivyo kwa nchi kama yetu na uchumi wetu tatizo hilo lipo na tunaendelea kulifanyia kazi. Kwa hivyo njia ambayo imetumika sasa hivi ni katika hiki Chuo cha Afya cha Mbweni kuanzisha *course* mpya ya *technologist* yaani wale wanakuwa wana uwezo wa ku-*repair* vyombo vile vinapoharibika vya *loboratory* au vyombo vya *diagnostic course;* hiyo ipo na wataalamu saba wali-*graduate* hivi karibuni wiki iliyopita, katika mahafali yaliyofanyika pale Chuo cha Afya Mbweni.

Pili, wataalamu hao ni ghali sana mtu akishapelekwa kusoma akitua tu hapa Dar es Salaam au akitua Nairobi anapigwa *offer* mara tano zaidi ya Zanzibar. Sasa inataka moyo wa kizalendo kweli kweli kukataa *offer* ya mara tano ukakubali *offer* hii. Kwa hivyo mimi naomba niendelee kuwapongeza wataalamu wetu kwa moyo wao wa kujitolea, kwa kweli wanafanya kazi ya wito wa Mwenyezi Mungu mwenyewe, kwa sababu kile wanachokipata hakilingani kabisa na soko la afya linaoweza kuwalipa wao. Uwezo wao ni mzuri, hivi sasa tunasaidiwa na Serikali ya Norway, tunasaidiwa pia na Serikali ya Denmark katika *specialization training*.

Kwa hivyo uwezo wao ni mzuri wanakwenda katika nchi ambazo ziko kiwango cha juu kabisa katika sekta ya afya. Sina shaka ya uwezo wao ila tutaendelea kujitahidi kadri tutakapopata fedha na wao tuwaongezee, japo zile za muda wa *over time* na mambo mengine kama hayo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Nam. 84

Vifaa vya Uchunguzi na Utibabu wa Ugonjwa wa Figo

Mhe. Mussa Ali Hassan - Aliuliza:-

Kwa kuwa Ugonjwa wa figo umekuwa ukijitokeza kwa kasi kwa wananchi wa Zanzibar na Tanzania kwa ujumla. Aidha, Wagonjwa wengi wa maradhi haya hupata matibabu kama vile kusafishwa au kutolewa figo na kuwekwa figo jengine katika Hospitali mbali mbali za nje ya nchi kama vile India n.k

Na kwa kuwa Hapa Tanzania zipo baadhi ya Hospitali kama vile Muhimbili wanavyo vifaa vya kusaidia kuchuja na kusafisha damu "*dialysis*", kwa ajili ya kusaidia kurefusha maisha ya mgonjwa ambapo zipo mashine zisizopungua kumi.

(a) Je, mashine kama hizo zipo katika Hospitali zetu.

(b) Na kama zipo, Hospitali ya Mnazi Mmoja na Abdalla Mzee Pemba wanazo mashine ngapi.

(c) Kama hakuna, mashine hizo zitapatikana lini, kwa kuzingatia kuwa bajeti zetu mara kadhaa zimeweka sekta ya afya kuwa ni miongoni mwa vipaumbele vya Serikali.

Mhe. Naibu Waziri ya Afya - Alijibu:-

Mhe. Naibu Spika, naomba kumjibu Mhe. Mussa Ali Hassan wa Jimbo la Koani swali lake Nam. 84 lenye vifungu (a) (b) na (c) kwa pamoja kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, ninakubaliana nae Mheshimiwa kwamba ugonjwa wa figo sasa umekuwa ukijitokeza kwa kasi kubwa sana kwa wananchi wa Zanzibar, Tanzania na Afrika Mashariki kwa ujumla na wagonjwa hao hupelekea kupatiwa matibabu hapa ndani ya nchi pia na nje ya nchi.

Mhe. Naibu Spika, Wizara ya Afya imepokea mashine mbili za kusafishia figo lakini ni mashine tu hazina vifaa vyote vya kufungwa ambavyo vinatakiwa ule mfumo mzima wa kusafishia figo. Aidha, kupitia njia ya damu au njia nyengine. Mashine hizo bado hazijafungwa na Wizara kwa kushirikiana na Chuo Kikuu cha Haukland hivi sasa inajenga *facility* maalum kwa ajili ya mashine hiyo ambayo itakuwa ni hiyo wodi mpya ya watoto inayojengwa ambayo ndani yake itakuwa na wodi maalum, yaani eneo maalum la kusafishia mafigo. Kwa sababu wodi zile zinakuwa si za kawaida.

Wodi zile zinakuwa na *fitting* zake malum, zinakuwa na *sterile* kama Mhe. Saleh huwa anapenda kutumia *terminology* hizo, kuna *sterile environment* yaani hali ya kutengwa kwa usafi wa hali ya juu, pamoja na pipe mbali mbali za kutoa maji na kusafishia mashine hizo ambazo ni *fitting* zake maalum.

Ujenzi tayari umeanza mwezi Septemba, 2014 na unatarajiwa kumaliza baada ya mwaka mmoja na miezi 6 *inshaallah*. Baada ya kumalizika ujenzi huo tunategemea kupata mashine 10 kutoka Haukland University na Serikali ya Watu wa Norway za kusafishia figo pamoja na hizi zetu mbili zitakuwa kumi jumla yake, kule nane na hizi mbili ambazo tunatarajia kufunga hapo na huduma rasmi za kusafirishia zitaanza.

Kutakuwa hakuna tena haja ya wagonjwa kwenda Dar es Salaam kwenda kusafishia damu ama kuondosha *urea* na mambo mengine ya sumu katika damu kutokana na mafigo kutokufanya kazi.

Pia naomba kulijulisha Baraza lako Tukufu Mhe. Naibu Spika, tumepata fursa ya kusomesha wataalam wa kuziendesha mashine hiyo.

Tatizo la pili ilikuwa hatuna wataalamu wa kuziendesha mashine hizo kwa sababu mashine ni *very complicated* na hivi sasa wataalamu wetu wawili wako masomoni kusomea mashine hizi.

Wakati huo huo Mhe. Naibu Spika, Chuo Kikuu cha Haukland kama nilivyosema hapo awali kimetoa nafasi hizo lakini pia kupitia ushirikiano huo wa mafunzo wa wafanyakazi wetu, mafunzo haya yatafanyika hapa nchini na yanatarajiwa mafunzo mengine kuanza tarehe 3 Novemba, siku chache baada ya leo katika hospitali ya Mnazi Mmoja na Muhimbili. Pia kwa matayarisho ya kuanza kutoa huduma hizo rasmi hapa Zanzibar.

Mhe. Spika**,** kwa vile Wizara ya Afya na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar jukumu lake la msingi ni kuhakikisha kuwa wananchi wote wa Zanzibar wanapata matibabu kwa maradhi yote yanayowasumbua, basi Wizara inaendelea kuwapatia matibabu wananchi wake ndani na pale inaposhindikana nje ya nchi pamoja na kuagizishia dawa na vifaa tofauti kwa kadiri tunavyopata fedha za kufanya hivyo. Na wakati huo jitihada za kuongezea *specialities* yaani maeneo au taaluma maalum za maradhi mbali mbali yanaendelea ndani ya Wizara. Ahsante Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri ya Mhe. Naibu Waziri kuhusu suala hili, lakini hivi sasa Tanzania imetoa *figure* ya wagonjwa wasiopungua laki nne ambao wapo Tanzania Bara, naomba Mhe. Waziri aniambie kwa Zanzibar hivi sasa tuna wagonjwa wangapi na kwa mwezi wanakufa wangapi na mwaka mmoja wanakufa wangapi.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Ahsante Mhe. Naibu Spika, Mheshimiwa hili ni swali la takwimu na hivi karibuni wakati tunapitia katika ziara yetu rasmi ya Wizara ya Afya, hususan katika hospitali ya rufaa ya Mnazi Mmoja suala lililoguswa sana ni takwimu na ziko takwimu ambazo zinaweza kutolewa *in public*, ziko takwimu ambazo madaktari maadili yao hayawaruhusu kutoa takwimu hizo. Sasa naomba nilichukue suala hili niliulizie kwa wataalam kama wanazo *figures* hizo na la pili nitaulizia kutokana na maadili yao je, zinaweza kutolewa takwimu hizo kwa sababu

zinahusiana na mambo ya maradhi *specific* kwenda kwenye mafigo. Kama zinafaa nitaomba nipewe muda ili niziwasilishe Barazani kama itaruhusika takwimu hizo kutolewa. Na kama haijaruhusika pia nitalijulisha Baraza lako tukufu Mhe. Naibu Spika. Ahsante sana.

Mhe. Salmin Awadh Salmin: Ninakushukuru Mhe. Naibu Spika, kwa kunipa nafasi hii nimuulize Mhe. Naibu Waziri maswali ya nyogeza mawili kama hivi ifuatavyo:-

Mhe. Naibu Spika, pamoja na majibu mazuri sana ya Mhe. Naibu Waziri nataka kumuuliza kama ifuatavyo. Kwa kuwa maradhi ya figo yamekuwa yakiongezeka siku hadi siku hapa Zanzibar, Tanzania na Afrika Mashariki kwa jumla kama alivyoeleza na kwa kuwa mbali ya wagonjwa husaidiwa kuchuja na kusafisha damu yaani *dialysis,* lakini matibabu yake halisi hulazimika kubadilishwa figo na kuwekwa figo jengine nje ya nchi. Na kwa kuwa mgonjwa baada ya kuwekwa figo hulazimika kutumia dawa kila siku kwa muda wote wa maisha yake na kwa kuwa dawa hizo ni ghali mno ambapo wagonjwa wengi hawawezi kumudu kununua dawa hizo.

Swali je, Serikali ya Mapinduzi Zanzibar huwasaidiaje wagonjwa wa aina hii ili kuweza kumudu kuzipata dawa hizi.

Lakini pili, ni sababu zipi zinazosababisha maradhi haya ya figo yawe yanaongezeka siku hadi siku.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, maradhi ya figo siku hizi yanatokana zaidi kutokana na mwenendo wetu wa kimaisha, vyakula tunavyokula, kukosekana kwa mazoezi, *pressure* ya damu ikiwa *low* ama *high* inaathiri moja kwa moja viungo kama moyo na baadae kupelekea kuathiri figo. Lakini sukari ya damu, sukari ya mkojo vyote hivyo kwa sababu figo ni *filters* ni viungo ambavyo vinatumika kuchuja ile sumu ya ziada, sukari ya ziada mambo mengine yote ya ziada ndani ya mwili na kutoka kwa njia ya mkojo. Kwa hiyo, zaidi ni mwenendo wa kimaisha vyakula tunavyokula hapo awali wazee wetu walikuwa wanakula vyakula hivi vya asili zaidi. Siku hizi tunakula vyakula vya makopo na kadhalika, sasa nayo imechangia tunatakiwa turudi kwenye vile vitu vya asili.

Zamani mimi sikumbuki unasikia watu wanapata maradhi kama haya hususan wazee wetu walioishi miaka 80, wengine wamefika miaka 85 mpaka 90. Kwa hiyo, ni mwenendo wa maisha na tunatakiwa sana tubadilishe mwenendo wa maisha hata ukienda pale kwenye kliniki ya wagonjwa wa sukari ambao pia ni waathirika wakubwa wa mafigo, utapata taaluma ama elimu ya jinsi gani ya kubadilisha mfumo wa maisha na kufanya mazoezi ni muhimu sana. Wanasema asilimia 70 mpaka 75 kuepukana na maradhi haya ni mazoezi.

Lakini pili, naomba nikubaliane nae Mhe. Mwakilishi kwamba bado hapa hatujaanza kubadilisha mafigo hatujafikia taaluma hiyo, ila vikipatikana vifaa vyote vinavyohusika naamini mabingwa tunao wanaweza kufanya operesheni kama hizo. *Surgeon* tunao wazuri hapa Zanzibar lakini sio kufanya operesheni tu ni vifaa ndio vinavyotakiwa ili ile operesheni ama upasuaji ule uwe *successful*.

Ni kweli mgonjwa aliyebadilishwa figo anatakiwa atumie dawa maisha yake yote mpaka kufa kwake, na kuna dawa ambayo anapewa yule aliyetoa lile figo lake kumpa yule mgonjwa wa figo. Na ni kweli dawa hizo ghali, lakini sio ghali sana kama ulivyosema Mhe. Mwakilishi, kuna dawa mbali mbali ambazo zinatumika na hivi sasa Wizara ya Afya imo katika jitihada kuwasaidia hususan wale waliopitia njia ya Serikali kwenda kutibiwa na kupata *replacement* ya *kidney* kuna utaratibu wa kuwasaidia dawa hizo pale inapokuwa gharama kubwa.

Na naomba niseme pia kuna dawa zile *essential drugs* zile tunasaidiwa pia kupitia wafadhili; kuna *list* yake maalum ambazo huja dawa hizo ambazo ni muhimu kama hizi *insulin* za wagonjwa wa sukari, hizi huwa zinakuwa na unafuu wa bei yaani bei yake inakuwa nusu au chini ya bei yake ya soko. Kwa hiyo, tunaendelea na jitihada hizo na *inshaallah* Mwenyezi Mungu akitujaalia tutakuwa na nguvu zaidi ya kuwasaidia dawa hizo. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Naibu Spika ahsante sana, kabla ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametuwezesha siku hii ya leo kuwa katika hali ya afya na uzima.

Mhe. Naibu Spika, naomba nimuulize Mhe. Waziri kwa kuwa kila uchao unaokwenda sayansi na teknolojia inakuwa na inabadilika, na kwa kuwa katika jibu lake mama Mhe. Naibu Waziri amesema kwamba kuna mashine alizozipokea ambazo hazikukamilika.

Je, mashine hizo zitakapokamilika zitakuwa tena zinafaa au mashine hizo watajua vipi kwamba kwa sababu kitu chochote unapokiweka sana basi ujue kinapata uchakavu kabla hujakitumia. Sasa je, Mhe. Naibu Waziri haoni kama Serikali inaweza ikaja ikapata hasara ya mashine hizo zilizokuwa hazikukamilika hata akitaka yeye zikamilike Serikali ikipata pesa haoni kwamba kutakuja kuwa na mabadiliko makubwa.

Mhe. Naibu Spika: Kabla Mheshimiwa hujajibu Waheshimiwa Wajumbe, wenzetu wanaochukua picha hizi inakuwa maneno mengi sana sasa wanarikodi Mhe. Waziri mazungumzo yenu yanakuwa haileti raha kwa wasikilizaji. Kwa hivyo, naomba wanaotaka kuzungumza waende nje wakazungumza wakimaliza warudi, lakini hapa tusikilize masuala ya Baraza. Mhe. Waziri majibu.

Mhe. Naibu Waziri wa Afya: Mhe. Naibu Spika, naomba nikubaliane nae kwamba kweli kila uchao sayansi na teknolojia inapiga hatua inaendelea. Zamani Zanzibar nzima tulikuwa tunatumia TV za *Philips* na Hitach na TV zenyewe ukiangalia ni kubwa kuliko ili *desk* leo kuna *flat screen* kabisa ambayo ni nchi mbili tu. Kwa hiyo, ni kweli kabisa lakini naomba pia nimuhuhakikishie kwamba mashine hizo zimewekwa pahala pazuri bado ni mpya hazijatumika wala hazijafunguliwa zimo katika maboksi yake bado na maplastiki yake.

Pia naomba kumuhakikisha kwamba mradi huu wa **OAKLAND** unaofanyika wa kujenga hiyo wodi ya watoto kwa kuwa inahitaji sehemu maalum ya chumba cha kusafishia damu ya mgonjwa ambaye mafigo yake hayafanyi kazi, basi naamini ndani ya kipindi hicho nilichokitaja cha mwaka mmoja na miezi sita mashine hizo inshaallah zitakuwa bado hazijapata taathira yoyote zitafanya kazi vizuri na zitatumika vizuri ni mashine ambazo zimewekwa sehemu nzuri hazipigwi na mvua wala haziko juani. Ahsante sana Mhe. Naibu Spika.

HOJA ZA SERIKALI

Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 2014

(Kusomwa Mara ya Kwanza)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tawala za Mikoa namba 1 ya mwaka 1998 na kuanzisha upya Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo, usomwe kwa mara ya kwanza.

Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 2014

(Kusomwa Mara ya Pili)

Mhe. Waziri wa Nchi, Ofisi Rais, Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ: Mhe. Naibu Spika, Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tawala za Mikoa namba 1 ya mwaka 1998 na kuanzisha upya Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo usomwe kwa mara ya pili.

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha hotuba ya muhtasari wa Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 2014.

Utangulizi:

Mhe. Naibu Spika, awali ya yote nachukua fursa hii kumshukuru Mwenyezi Mungu mtukufu kwa kutujaalia afya njema na nguvu zilizotuwezesha kukutana tena leo katika Baraza hili tukufu kuendeleza majukumu yetu tuliyopewa kisheria.

Mhe. Naibu Spika, aidha nachukua fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa kukubali kunipa fursa hii kwa mara nyingine tena na kuwasilisha mswada katika Baraza lako tukufu. Mara hii ukiwa Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa Zanzibar ya mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, naomba pia niendelee kumshukuru Mhe. Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi Dkt. Ali Mohammed Shein kwa kuniagiza kuwasilisha Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa wa mwaka 2014 katika Baraza lako tukufu.

Aidha, nalishukuru Baraza la Mapinduzi kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kujadili na kumshauri vyema Rais wa Zanzibar na akaukubali mswada huu na maelekezo na miongozo yao imewezesha kufanikisha kukamilika kwa mswada huu na kuruhusu kuwasilishwa katika Baraza lako tukufu.

Mhe. Naibu Spika, napenda pia kumshukuru Katibu wa Baraza la Mapinduzi na Katibu Mkuu Kiongozi Dkt. Abdulhamid Yahya Mzee na Kamati ya Makatibu Wakuu kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuweka vyema mswada huu na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa Baraza la Mapinduzi juu ya mambo yaliyomo katika mswada huu.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu umejadiliwa na Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala chini ya Mwenyekiti wake Mhe. Ussi Jecha Simai, Mwakilishi wa wananchi wa Jimbo la Chaani. Kamati imefanya kazi kubwa ya kupitia mswada huu na kuufanyia marekebisho maeneo ambayo yalikuwa na mapungufu na kwa sasa nina furaha kuliarifu Baraza lako kuwa uko katika hali nzuri. Nawashukuru sana kwa michango yao ambayo imetokana na uzoefu, uelewa na umahiri wao.

Mhe. Naibu Spika, pia nachukua fursa hii kumpongeza Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar Mhe. Said Hassan na watendaji wa ofisi yake kwa kazi kubwa ya kufanyia marekebisho mbali mbali ya kitaalamu mswada huu ambayo yalikuwa ni muhimu kufanyika kabla ya kupelekwa Idara ya Uchapaji.

Mhe. Naibu Spika, vile vile napenda kutoa shukurani na pongezi kwa Katibu Mkuu Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Wakurugenzi, Kamati mbali mbali za wataalamu ambazo zilifanya kazi awali ya kuandaa rasimu ya awali, kuchukua maoni ya wadau mbali mbali hadi kupatikana Rasimu ya Mswada na kuanza hatua ya mwisho za ukamilishaji wa mswada.

Pia nawashukuru watendaji wote wa Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ kwani ushirikiano wao kwangu ndio chanzo cha mafanikio haya. Na mwisho lakini si kwa umuhimu niwashukuru wafanyakazi wa Idara ya Upigaji Chapa iliyo chini ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais kwa kazi kubwa waliyoifanya ya kuweza kukamilisha kazi ya upigaji chapa ya mswada huu. Nawashukuru sana.

Chimbuko la Mswada

Mhe. Naibu Spika, chimbuko la mswada huu ni haja ya kuwa na sheria mpya ya Tawala za Mikoa itakayoendana na mahitaji ya sasa na kwa mujibu wa sera mpya ya Serikali za Mitaa.

Madhumuni ya Mswada

Mhe. Naibu Spika, mswada huu unalenga kuweka mfuko wa kiutawala wa Serikali Kuu kuanzia ngazi ya shehia hadi Mkoa kwa kuzingatia mageuzi ya Serikali za Mitaa na kuondoa kasoro zilisojitokeza katika sheria ya sasa ya Tawala za Mikoa na kuweka mtiririko ulio bora zaidi kwa mujibu wa mahitaji ya sasa.

Aidha, madhumuni ya mswada huu ni kupata sheria itakayoonesha wajibu, muundo, kazi, uwajibikaji kwa kila ngazi ya Serikali Kuu kuanzia ngazi ya Mkoa, Wilaya na Shehia na kukuza uhusiano baina ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa.

Muundo wa Sheria

Mhe. Naibu Spika, Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa imegawika katika sehemu tano na vifungu 34 kama ifuatavyo:-

Sehemu ya Kwanza

Mhe. Naibu Spika, sehemu hii inajumuisha vifungu 3 ambavyo ni jina fupi la sheria, tarehe ya kuanza kutumika, eneo la matumizi ya sheria na tafsiri ya maneno muhimu.

Sehemu ya Pili

Mhe. Naibu Spika, sehemu hii ina vifungu 9 ambavyo ni kifungu cha 4 hadi cha 12 vinavyoelezea uwazishwaji wa Ofisi ya Tawala za Mikoa, uteuzi, sifa za Wakuu wa Mikoa, Wakuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mikoa na Wilaya, Masheha, ujazaji wa nafasi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya, sifa za kuanzisha Shehia, kuondoshwa kwa Sheha, kuanzishwa kwa Katibu wa Sheha na sifa za Katibu wa Sheha.

Sehemu ya Tatu

Mhe. Naibu Spika, sehemu hii ina jumla ya vifungu 8 kuanzia kifungu cha 13 hadi 20 ambavyo vinaelezea kazi, wajibu na uwezo wa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya, Makatibu Tawala wa Mkoa na Wilaya, Sheha na Katibu wa Sheha.

Sehemu ya Nne

Mhe. Naibu Spika, sehemu hii ina jumla ya vifungu 5 kuanzia kifungu cha 21 hadi 25 ambavyo vinaelezea uanzishwaji, muundo na kazi za Kamati za Maendeleo za Mkoa, uanzishwaji na sekreterieti ya Mkoa na uanzishwaji wa kazi za Baraza la Ushauri la Sheha.

Sehemu ya Tano

Mhe. Naibu Spika, sehemu hii ina vifungu 10 kuanzia kifungu cha 26 hadi 34 ambavyo vinaelezea uwezo wa Mhe. Rais kukasimu madaraka kwa Waziri na Mkuu wa Mkoa, viapo vya maofisa, usimamizi na utoaji wa fedha, mkutano wa Kamati, Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Mkoa, Wilaya, mwenendo wa sheria na Kanuni zake.

Hitimisho

Mhe. Naibu Spika, naomba kuwasilisha kwenye Baraza lako tukufu mswada huu kwa kufuata taratibu za kisheria na Kanuni za Baraza la Wawakilishi ili muupitie, muujadili, mtoe ushauri wenu na hatimae muidhinishe mswada huu na kuwa sheria.

Mhe. Naibu Spika, naomba kutoa hoja.

Mhe. Naibu Spika: Waheshimiwa Wajumbe, mswada ni mdogo naomba wenye nia ya kuchangia walete ili nijue vya kujipanga, mpaka sasa nina wachangiaji wawili baada ya Mwenyekiti kwa hiyo naomba sana.

Mhe. Ussi Jecha Simai (Mwenyekiti wa Kamati ya Katiba na Sheria): Nakushukuru Mhe. Naibu Spika, kunipa nafasi ya kutoa maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala Baraza la Wawakilishi kuhusu Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tawala za Mikoa namba 1 ya mwaka 1998 na kuanzisha upya Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza kabisa namshukuru Mwenyezi Mungu Mtukufu kwa kutupa uhai na uzima na kutuwezesha kukutana hapa kwa ajili ya kutekeleza shughuli mbali mbali tulizojipangia.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii adhimu kukushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuwasilisha maoni ya Kamati yangu kuhusu Mswada wa Sheria ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 2014 ambao kamati yangu pamoja na wajumbe tulipata nafasi ya kuchunguza kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Baraza la Wawakilishi, Tolea la Mwaka 2012.

Mhe. Naibu Spika, pia, niwashukuru wajumbe wa Kamati hii, pamoja na Makatibu Kamati kwa kazi waliyoifanya kwa muda wa siku mbili mufululizo hadi kuweza kumaliza kufanya kazi hiyo kwa mujibu wa Kanuni na hatimaye leo hii mswada huo upo mbele yetu kwa ajili ya mjadala na kuupitisha. Naomba kuwashukuru Wajumbe hao sana, sana pamoja na Makatibu Kamati.

Mhe. Naibu Spika, Kamati yangu imepata usaidizi mkubwa wakati wa kupitia Mswada huo kutoka kwa Afisi ya Baraza la Wawakilishi, kuanzia Katibu wa Baraza, Mshauri wa Sheria wa Baraza na Wanasheria wa Baraza. Aidha, msaada mkubwa wa ufafanuzi na maelezo Kamati ilipata kutoka kwa Mheshimiwa Waziri na Katibu Mkuu pamoja na Watendaji wao wakuu ambao walisadiana na Afisi ya Mwanasheria Mkuu kutoa maelezo hayo. Hivyo kwa

ujumla na kwa niaba ya wajumbe wa Kamati yangu naomba nitoe shukurani za pekee kwao kwa kazi yao kubwa waliyofanya wakati wote Mswada huu ulipokuwa mbele ya Kamati kuchunguzwa.

Mhe. Naibu Spika, katika kuchunguza Mswada huu kamati imeona kuwa yapo maeneo ya vifungu mbali mbali ambayo yangehitaji kufanyiwa marekebisho, hivyo Kamati inamshauri Mheshimiwa Waziri kukubali ushauri wa kamati wa kufanya marekebisho katika maeneo hayo ambayo nakala ya ushauri kwa marekebisho hayo imeshatolewa na kusambazwa kwa Waheshimiwa Wajumbe.

Mhe. Naibu Spika, nachukua nafasi hii kuwataka Waheshimiwa Wajumbe kutafakari kwa kina wakati wa kuchangia Mswada huu, kwani Mswada huu unatuvusha kutoka kwenye ile Sheria ya Tawala za Mikoa Nam. 1 ya mwaka 1998 inayofutwa, ambayo kama alivyotangulia kueleza Mheshimiwa Waziri, imeshapitwa na wakati.

Mhe. Naibu Spika, kwa vile kamati yangu imepata nafasi ya kupita Mswada huu kifungu kwa kifungu na kushauri marekebisho kadhaa kufanyika kwenye vifungu mbali mbali vya Mswada kama vinavyoanishwa kwenye Waraka wa marekebisho uliogaiwa kwa Waheshimiwa Wajumbe, naomba nijielekeze katika mchango wa jumla kuhusu namna nzuri ya kufanya Mswada huo utekelezeke mara tu baada ya kuwa Sheria.

Mhe. Naibu Spika, ili sheria hii ipate ufanisi wakati wa kutekelezwa kwake, ni vyema basi elimu kubwa itolewe kwa wananchi kupitia vyombo mbali mbali vya habari tofauti na kuelezwa kuhusu muundo, uwezo na majukumu mbali mbali ya Serikali za Mitaa. Kwa kufanya hivyo, tutawasaidia wananchi ambao wao ndio walengwa wa kubwa wa Sheria hii kuweza kushiriki harakati mbali mbali za maendeleo kuanzia ngazi za chini za serikali yaani Shehia.

Mhe. Naibu Spika, uwelewa wa wananchi katika sheria hii utasaidia kuzifanya Serikali za Mitaa kuanzia ngazi ya Shehia kuwa wenye ushiriki mkubwa wa wananchi wenyewe kama ilivyoainishwa katika kifungu cha 25 cha Mswada huu, ambacho kimetaja wajumbe watakaoingia katika kamati ya watu 10 au 15 kwa Baraza la Ushauri wa Shehia ambalo limezingatia uwakilishi wa makundi mbali mbali ya kijamii, jinsia na kimaeneo.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia inashauri kuwa katika utekelezaji bora wa Sheria hii, izingatie kuziwezesha Serikali za Mitaa kuwa na wataalamu wake ambao kamati ilipofanya ziara za kutembelea baadhi ya Halmashauri na Mabaraza ya Miji imegunduwa ukosefu wa wataalamu fani mbali mbali katika serikali hizo.

Kamati yangu inaamini kuwa, kupitishwa kwa Sheria hii kutawezesha Serikali za Mitaa kuajiri wataalamu hao na kuwatumia katika utekelezaji bora wa sheria hii kwenye maeneo mbali mbali.

Mhe. Naibu Spika, kamati pia inaitaka serikali wakati wa kuanza kutekeleza Sheria hii kuhakikisha kuwa inaharakisha kuimarisha Ofisi za Masheha kwa kuzitenganisha na makaazi yao au majumba yao. Kwa kufanya hivyo itaepusha shughuli za Kiserikali kufanyika nyumbani kwa mtu na kuhatarisha usiri na ufanisi wa utekelezaji wa Sheria, Kanuni na Maelekezo yatakayoelekezwa katika ngazi ya Shehia kwa mujibu wa Sheria hii.

Mhe. Naibu Spika, kwa mujibu wa kifungu cha 11 cha Mswada hu tunaokusudia kuupitisha hivi punde wa sheria hii, kutakuwa na Sekretarieti ya Shehia kwa maana ya Katibu wa Sheha ambaye atakuwa ni mtaalamu na atakuwa ni mwajiriwa wa Serikali. Hivyo basi, Kamati yangu inazidi kusisitiza umuhimu wa kuwa na Ofisi ya Shehia kwa vile kazi za katibu wa Shehia zitalindwa kwa mujibu wa masharti ya Sheria za Utumishi na Sheria nyingine zinazohusu utendaji kazi, utunzaji siri na uwajibikaji.

Mhe. Naibu Spika, ofisi za Mikoa na Wilaya zimekuwa ni kiungo kizuri katika uendeshaji wa Serikali za Mitaa, katika sehemu ya pili na ya tatu ya Mswada huu, kunaanzishwa Ofisi za Utawala katika ngazi za Mikoa, Wilaya na Shehia pamoja na kazi na majukumu yake. Kamati yangu haina tatizo na Muundo na majukumu hayo, isipokuwa inashauri kuwa, utekelezaji wa majukumu hayo lazima uendane na upatikanaji wa wataalamu wenye uwezo na elimu ya kutosha.

Mhe. Naibu Spika, nimelazimika kuligusia hilo kwasababu Kamati yangu imeona changamoto hizo katika baadhi ya Serikali za Mikoa na Wilaya ambapo baadhi wa maafisa muhimu wa kitaalamu wamekosekana na kusababisha kutofanyika kwa ufanisi kwa baadhi ya shughuli na majukumu ya serikali hizo.

Mhe. Naibu Spika, naomba kumalizia hotuba hii fupi ya maoni ya kamati kwa kuwaomba Wajumbe wa Baraza hili kujadili na kupitia kwa makini vifungu vya Mswada huu na kutoa ushauri wa kuimarisha vifungu vya Mswada huu hatimaye kupitisha kuwa Sheria.

Kamati yangu imeupitia Mswada huu pamoja na Wizara na Wanasheria wa Serikali kutoka Ofisi ya Mwanasheria Mkuu na Baraza la Wawakilishi na imepata maelezo ya kutosha, ya kuridhisha, ni imani yetu kuwa pamoja na ushauri uliotolewa na kamati katika kupendekeza marekebisho ya baadhi ya maeneo ya Mswada huu, Mswada huu utapitishwa na Wajumbe wa Baraza lako kuwa Sheria.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwa kumkushukuru Mhe. Waziri wa Nchi (AR) Tawala za Mikoa na Idara Maalum za SMZ, nimpe haki yake kuwa amekuwa ni msikivu pale Wajumbe wa Kamati wanapomshauri na tunapotofautiana kwa hoja za kistaarabu na kiungwana hatimaye tunakubaliana.

Mwisho kabisa niwashukuru pia watendaji wote wa wizara hii, kwa ushirikiano wa hali ya juu waliyoipa kamati yangu wakati wa kupitia Mswada huu. Kwa niaba ya wote nimtaje Katibu Mkuu, Ndugu. Joseph Meza ambaye amekuwa bila kujali majukumu mengi ya kiutendaji aliyonayo, amekuwa akitoa ushirikiano kamati yetu muda wote tukifanyaka kazi pamoja.

Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa nisiwe mwizi wa fadhila kwa niaba ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kuwashukuru Wanasheria wa Afisi ya Mwanasheria Mkuu ambao katika mswada huu pamoja na tulioupitisha jana, wamefanya kazi kubwa usiku na mchana kuhakikisha kuwa Miswada hii inafika hapa Barazani na kushirikiana na kamati katika kutoa maelezo ya ufafanuzi.

Mwisho kabisa nikushukuru wewe tena kwa kunistahamilia muda huu mdogo wa kuwasilisha maoni ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala. Mhe. Naibu Spika, naunga mkono hoja.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mhe. Mwenyekiti wa Kamati. Sasa baada ya hotuba ya Mwenyekiti tutaanza na Mhe. Ali Salum Haji, baadae Mhe. Makame Mshimba Mbarouk na Mhe. Mohammed Haji Khalid.

Mhe. Ali Salum Haji: Mhe. Naibu Spika, nikushukuru kwa dhati kwa kunipa fursa hii kuweza kuchangia Mswada huu wa Kuanzisha Sheria za Tawala za Mikoa kwa mwaka 2014.

Mhe. Naibu Spika, baada ya kukushukuru wewe kwa dhati pia nichukue fursa hii kumshukuru Mhe. Waziri kwa kuweza kutuletea mswada huu. Kwa kweli tunapaswa tutoe pongezi za dhati kabisa kwa Mhe. Waziri kwa miswada hii ambayo ameweza kutuletea kuanzia jana hadi leo. Kama kulikuwa kuna vilio vya muda mrefu basi vilikuwa vinatokana na sheria hizi mbili ambazo tunataka kuzitengeneza ile ya Manispaa ambayo tumeipitisha jana na hii ya Tawala za Mikoa.

Mhe. Naibu Spika, kwa bahati nzuri niseme, jana nilipokuwa nikichangia nilitamka kwamba nilikuwa mdau wa Baraza la Manispaa, lakini leo pia nataka niweke katika *hansard* ya Baraza kwamba pia nilikuwa mdau wa Sheha. Kwa sababu mwaka 1998 mwezi Julai baada ya kufariki Sheha wa Shehia ya Kwaalamsha Mhe. Sheha Khamis na kuteuliwa Sheha mpya Mzee Shafi, Sheha yule aliniteuwa kuwa ni miongoni mwa wajumbe wake 10 wa Baraza la Sheha na niliweza kutumikia kazi hiyo kwa muda wa miaka miwili na kabla ya kutumikia kazi ya udiwani. Sasa kama kuna mtu ambaye alikuwa anajua hasa matatizo au ugumu wa utumishi wa Sheha nina imani mimi ni miongoni mwao.

Mhe. Naibu Spika, katika mambo ambayo yalikuwa ni magumu sana katika masuala ya Sheha basi ni maeneo ya mipaka. Kwa nini niseme hivyo? Nasema hivyo kwa sababu nchi yetu ya Zanzibar sasa hivi imekuwa na ukuaji mkubwa sana; miji mipya kuingiwa na watu mbali mbali, miji ambayo tulikuwa tumeizowea kuwa na idadi ndogo ya watu. Lakini kwa kipindi kifupi sana ongezeko la watu limekuwa kubwa. Tatizo hili limepelekea kudumaa kwa shughuli za kimaendeleo na kiuchumi na kuleta baadhi ya kero katika maeneo hayo.

Sasa kuja kwa mswada huu imani yangu kwamba maeneo yale yamepata ufumbuzi. Kuna maeneo Shehia yake moja imekuwa na idadi ya watu karibuni sawa sawa na baadhi ya majimbo au zaidi ya majimbo na mfano mkubwa ni Shehia ya Pangawe katika Jimbo la Fuoni.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo lilikuwa ni tatizo katika utumishi wa Masheha basi ilikuwa ni suala zima la muingiliano wa mipaka na lilikuwa likileta switafahamu baina ya Sheha na Sheha. Hata mimi niliwahi kupata mtihani mkubwa sana na Sheha ambaye sasa ni marehemu wakati nikiwa katika shughuli zangu za utendaji wa Shehia, nikiweka namba za nyumba zile kuwatambua wakaazi wangu; Sheha wa Kwahani wakati huo Marehemu Bwana Almasi tulifika kuzozana akasema tunanyang'angiana nyumba. Anasema hizi nyumba zangu na sisi tunamwambia hizi nyumba zetu Shehia ya Kwaalamsha; suala ambalo lilitupa tabu lakini kwa hekima za Masheha, busara zao na utu uzima wao tulifika mahali tukaelewana.

Sasa niseme hili tatizo ambalo kwa kipindi kilichopita lilikuwa ni tatizo kubwa sana. Tatizo kama hilo pia nilikuwa nalo katika Shehia ya Kwaalamsha kwa upande wa Soko la Mikunguni, ambapo tumepakana na Shehia ya Mkele. Kama utakwenda hivi sasa ukiambiwa utofautishe nyumba zipi ni za Shehia ya Kwaalamsha na nyumba zipi za Shehia ya Mkele sijui kama utaweza kugawa mipaka yake. Kwa sababu mazingira ya nyuma ni kwamba eneo lile zamani palikuwa pana jaa, pana shimo na ndiyo uliokuwa mpaka wa baina ya Mkele na Shehia ya Kwaalamsha. Sasa shimo lile baada ya kufukiwa na kuweka makazi mapya unashindwa kutofautisha baina ya Shehia hizo.

Mhe. Naibu Spika, hayo ni baadhi ya matatizo tu ambayo nilitaka nielezee kwamba sheria hii sasa hivi labda inaweza kutuwekea mipaka mizuri, kuweka mazingira mazuri ili kuondosha switafahamu zile ambazo zilijitokeza huko nyuma na pia kuweka wepesi katika kuwatumikia wananchi wetu. Lakini pia watu kupata uelewa katika majukumu ya Sheha. Wengi walikuwa wakitafsiri kwamba labda Sheha anafanya shughuli za kisiasa lakini sivyo. Sheha alikuwa ni mtu wa karibu zaidi na jamii ili kuweza kurahisisha maendeleo ya kijamii katika maeneo yake ya mitaa kwa Serikali Kuu.

Mhe. Naibu Spika, sasa naomba niingie katika mswada wenyewe. Katika mswada huu Sehemu ya Pili kifungu cha 6(1), naomba ninukuu kinasema hivi:-

> "Endapo Mkuu wa Mkoa au wa Wilaya ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa muda kutokana na sababu ya kutokuwepo ofisini au kwa sababu ya maradhi au sababu nyengine yoyote ile, Rais atateuwa Kaimu Mkuu wa Mkoa au Wilaya kwa mujibu wa masharti ya Katiba".

Mhe. Naibu Spika, mimi hapa kidogo napata mashaka na ningemuomba Mhe. Waziri aliangalie hili suala kwa uzito kabisa. Sababu ya kusema hivyo ni kuwa na muda basi wa kuona namna gani ya maradhi vile hali ilivyo. Mheshimiwa hatupendi lakini ndiyo majaaliwa ya Mwenyezi Mungu, kwamba baadhi ya viongozi Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa huwa wanapata maradhi wanakaa vitandani kwa muda mrefu kupindukia pasipo na uteuzi wa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa mwengine.

Sasa mimi nahisi tungetafuta namna ya kuweka kwamba baada ya kuthibitika na daktari kutokana na maradhi yake kwamba hana uwezo wa kufanya kazi basi Mhe. Rais ateuwe Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa mwengine, kuliko kukaa muda mrefu halafu kuteuwa kaimu.

Mhe. Naibu Spika, lakini kama tunahitaji kaimu mimi nilitaka Mhe. Waziri anisaidie kwa nini kaimu asiwe Katibu Tawala wakati ambapo Sheha au Mkuu wa Wilaya anakuwa anaumwa? Kwa nini niseme hivyo? Sababu ya kusema hivyo Mhe. Waziri atakuja kunisaidia sana kwa sababu nilisoma katika ufafanuzi.

Mhe. Mwenyekiti, katika ufafanuzi Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa naomba nikisome kimoja tu cha Mkuu wa Mkoa. Ufafanuzi wa Mkuu wa Mkoa kinasema:-

> " Maana yake ni mtumishi wa umma ambaye uteuzi wa muda wa utumishi wake utafuata utaratibu uliowekwa chini ya Sheria ya Utumishi wa Umma ya Zanzibar huwa msaidizi Mkuu wa Mkoa".

Sasa kama kwenye ufafanuzi tumesema ni msaidizi, msaidizi anapoondoka basi kwa nini yeye asikaimu kwa kile kipindi mpaka tukapata, vyenginevyo Mhe. Naibu Spika, kama hatua iliyowezekana kisheria basi hili neno la kwamba msaidizi ndiye Mkuu wa Mkoa tungeliangalia kwa kina sana katika suala la ufafanuzi wa Katibu Tawala wa Mkoa na Wilaya. Lakini kama itakuwa inatafsirika hivi ni msaidizi basi mimi nafikiri tuna haja ya kulirekebisha katika suala la ufafanuzi namna tulivyomuweka kwamba Katibu Tawala atakuwa ni msaidizi wa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, chengine ambacho nataka nikichangie katika Mswada huu ni ukurasa wa 8, Uteuzi na Sifa za Sheha.

Mhe. Naibu Spika, katika sifa za Sheha kifungu cha 8(2)(c) kinasema, awe mkaazi wa Shehia husika kwa muda usiopungua miaka kumi na tano. Kama Mhe. Waziri atanikubalia, mimi muda wa miaka 15 nauona mdogo kwa Sheha kuwa mkaazi katika eneo lake. Nina sababu za msingi za kusema hivyo. Kwa sababu Sheha ana sifa nyingi ambazo zinamhitaji kuwa Sheha na zimeainishwa zote, awe ni mwenye kuheshimika, awe mtu aliyethibitika kwa uadilifu, lakini pia awe ni mtambuzi basi wa lile eneo ambalo yeye analiongoza na kufahamu tabia na silka za wale ambao anawaongoza. Sasa miaka 15 kwa mtu tu kwamba ameingia katika eneo miaka 15 kuishi halafu ukampe usheha, mimi naona ni muda mdogo kabisa.

Kuna kipindi nilipokuwa nikisoma huu mswada nilitafakari nikataka kusema hata wewe mkaazi wa kuzaliwa. Lakini nikaona itakuwa ugumu kwa vizazi vyetu ambavyo vimeshazowea tabia za kuhamahama miji, ambapo unaweza ukamkosesha mtu haki ya kupata kutawala. Nafikiri muda wa miaka 15 ni mdogo kama itakuwa inawezekana Mhe. Waziri basi nahisi iwe miaka 20 *reasonable* kujua mtu tabia zake, silka na kumjua huko alikotokea alikuwa na tabia gani na silka gani.

Kwa sababu tabia za watu wakati mwengine zinakuwa zinajificha kwa muda mfupi tabu kuzielewa kwamba huyu mtu alikuwa na tabia gani. Anaweza kujificha kwa kutaka kitu lakini baada ya kupata tabia zake zikaanza kufichuka kwamba alikuwa mtu si muadilifu.

Chengine ambacho nataka nikizungumze katika kifungu hiki;, nishukuru na nipongeze kwa sababu nimeona mabadiliko ya mswada ambayo nimeyapata pia. Kifungu (f) kwamba kimeamuliwa kufutwa kutokana na kwamba kifungu hicho kilikuwa kinasomeka kuwa Sheha awe mwenye cheti cha Kidato cha Nne au zaidi. Lakini nimpongeze Mhe. Waziri pamoja na wanasheria labda baada ya kukaa na kutafakari kuona kwamba hakuna haja.

Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu mimi nilikuwa napata kigugumizi kwamba leo hii Mwakilishi, Mbunge, Katiba inatutambua kwamba tujue kusoma na kuandika lakini mtu wa Serikali za Mitaa chini anayetumikia wananchi ndiyo tuanze kumuwekea ngazi za kisomo. Sasa hili lilikuwa linanipa mashaka. Mimi nafikiri kama taaluma basi angalau tungeweka awe na taaluma za kidini na uchamungu. Kwa sababu hawa watu wanatakiwa wawe waadilifu na ukaribu zaidi katika kuwatumikia wananchi kuliko elimu za kisayansi ambazo zinahitaji mambo ya kitaalamu.

Mambo haya ya skuli ni mambo ya kitaalamu katika masuala ya kiutendaji, lakini mambo ya Sheha zaidi ni mambo ya tabia na silka za mtu nzuri. Sasa labda tungeweka taaluma za kidini ingekuwa ni nzuri zaidi Mhe. Naibu Spika. Lakini kwa sababu Mhe. Waziri ameliona hilo na amelifuta nishukuru na nimpongeze kwa hilo na imani yangu kwamba Wajumbe wote watakubaliana na hilo.

Mhe. Naibu Spika, jengine katika kifungu hicho hicho cha 8(3) ningeomba ninukuu halafu kuna jambo nataka Mhe. Waziri aje anisaidie hapa. Kinatamka kwamba:-

> "Kutakuwa na Naibu Sheha katika kila Shehia ambaye atateuliwa na Mkuu wa Wilaya kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Shehia baada ya kupokea pendekezo kutoka kwa Mjumbe wa Baraza la Shehia husika".

Naomba niendelee na 8(4) halafu ndio nitoe ufafanuzi wangu.

Kifungu cha 84 kinasema kwamba:-

> "Endapo Sheha aliyeteuliwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa muda kutokana na sababu ya kutokuwepo ofisini au kwa sababu ya maradhi au sababu nyengine yoyote ile, Mkuu wa Mkoa atateua Naibu Sheha kuwa Kaimu Sheha".

Sina tatizo na kifungu cha 8(4) kwa Naibu Sheha kuwa Kaimu wa Sheha. Lakini tatizo ninalolipata katika Mswada huu kumetajwa sifa za Sheha. Lakini sifa za Naibu Sheha sijaziona kwamba labda na Naibu Sheha awe na sifa ambazo zinalingana na Sheha kwa sababu huyu mtu anakuja kukaimu hii nafasi. Lakini tukiendelea zaidi pia

unaambiwa kwamba kifungu cha 5 kinasema kwamba kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Masharti ya Sheria ya Utumishi na Kanuni zake Mkuu wa Mkoa atamthibitisha na kumteuwa Kaimu Sheha kuwa Sheha.

Sasa mimi nafikiri hapa kuna haja basi angalau na Naibu Sheha nae anateuliwa kwa kupitia Mabaraza basi angalau na yeye tungempa na yeye sifa zinazostahili kuwa Naibu Sheha. Si lazima zikaendana na zile za Sheha lakini angalau zioane ili pale atakapokaimu basi na yeye aweze kufanya kazi zake kwa mujibu wa utaratibu uliokuwa mzuri na uadilifu kabisa, kuliko kuwa hana sifa kabisa halafu unakuja kumpa nafasi ya Ukaimu na Ukaimu wenyewe hautakuwa muda mferu.

Chengine Mhe. Naibu Spika, nilikuwa naomba nisome katika kifungu cha 9 ambacho kinasema:-

"Kuondolewa Sheha katika Ofisi".

Sasa zimetajwa sifa za kuondolewa kwa Sheha katika ofisi ziko karibuni 4 lakini nilitaka kupata maelekezo kwa Mhe. Waziri kwamba sijaona kitu ambacho kimemzungumzia Sheha muda wa kustaafu haya majukumu ambayo amepewa. Sasa hivi tunajua kwamba wana vipindi maalum vya kustaafu. Lakini inaonekana inahitajika kwa Sheha yule kuendelea na muda basi anakuwa anaengezewa muda wa vipindi tofauti. Sasa ningetaka kujua kwamba Sheha huyu atatumikia hii nafasi ya Sheha kwa muda gani na kama kutakuwa kuna ridhaa ya kumuongezea vipindi, kwa sababu na zaidi tukiangalia kwamba Sheha anaingia katika majukumu haya akiwa na umri wa muda mrefu yaani anaanza kazi hii ana miaka 40.

Sasa miaka 40 anayoitumikia labda tuseme kwamba atakapofikia miaka 60 basi suala la Usheha pia linaweza likakoma kutokana na umri na sababu ya msingi ya kusema hivyo ninayo, kwamba sasa hivi tunao baadhi ya Masheha ambao umri wao unakuwa mkubwa, lakini unahisi uwezo wa kufanyakazi anao lakini namna ya kujituma kutokana na hali yake ya kiafya au umri inakuwa hayuko katika mazingira mazuri, sasa nahisi tungeweka suala hilo wazi.

Mhe. Naibu Spika, pia nilikuwa naomba nizungumzie katika kifungu cha 11(d). Kifungu cha 11 sifa za Katibu wa Sheha. Hapa nilikuwa naomba nitoe pendekezo katika moja ya sifa za Katibu wa Sheha katika kifungu (d) kimeandikwa kwamba awe mwenye cheti cha ngazi ya kidato cha sita au zaidi. Lakini hii nafikiri ilizingatia zile sifa za Sheha mwazo kabla ya kuondosha ile elimu baada ya kwamba Sheha awe kidato cha nne tukaona angalau katibu wake angalau awe kidato cha sita na Elimu ya Juu.

Sasa mimi Mhe. Naibu Spika, kifungu hiki nilikuwa napendekeza ishuke kutoka kidato cha sita basi tuje mpaka kwenye kidato cha nne. Kwa nini niseme hivyo Mhe. Naibu Spika? Niseme kwamba hii kazi tunahitaji watu wengi waipende na kazi hii ya Katibu wa Sheha mara nyingi ni kazi ya jamii na imekaa kama kazi ya kujitolea. Sasa sitegemei kama watu wengi ambao wamesoma kada kubwa watapendelea kufanya maombi katika suala la kutaka ukatibu wa Sheha.

Sasa nafikiri tunaweza tukafikia pahala tukawa tunahitaji watu kuwa Makatibu wa Masheha wakawa hawataki ama kutokana na mazingira ya kazi yenyewe au ama kutokana na maslahi ya hiyo nafasi yenyewe. Vyenginevyo kama kutakuwa na maslahi mazuri mimi nahisi vijana wanaweza kwenda. Lakini kwa hili nahisi tungepunguza elimu kutoka kidato cha sita kuja kidato cha nne ili *at list* tupate vijana wengi kuweza kuitumikia hii kada.

Chengine Mhe. Naibu Spika, nilitaka tuongeze kutoka (d) kuja (e) pamoja na kwamba Katibu atakuwa ni muajiriwa wa Serikali lakini kutokana na *nature* ya kazi yenyewe ya katibu kuwa ndiye mratibu wa Sheha. Sasa mimi nilikuwa nahisi tungeengeza na sifa nyengine kwamba basi huyu muajiriwa awe ni mkaazi wa eneo husika, ili katika wepesi wa utendaji wa kazi zake awe karibu zaidi na Sheha wake. Kuliko kuwa muajiriwa wa Serikali lakini akakaa Kidoti kaajiriwa Muungano. Sasa hili kidogo litaweza kuleta ugumu.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo katika sehemu ya 3 kifungu cha 12 (3) pana neno dogo limeingia lilikuwa linanipa ukwasi wa kufahamu kiswahili chake hakijakaa sawa na sijui kama kuna marekebisho kinatamkwa kwamba:-

"Kufuatia kusimamia au kuwajibika katika kutekeleza wa kazi za Serikali katika Mkoa wake".

Mhe. Naibu Spika, kidogo haisomeki vizuri sasa hii "wa" sijui inaleta tafsiri gani na nilijaribu kuangalia huku sikuona marekebisho. Kama yapo marekebisho basi sina tatizo na hilo.

Mhe. Naibu Spika, naomba niendelee katika ukurasa huu wa 229 katika kifungu cha 18 kazi na majukumu ya Sheha (c). Mhe. Naibu Spika, imetaja kwamba ni kuweka kumbukumbu za nyaraka zote zinazohusiana na usajili wa ndoa, talaka, vizazi na vifo, vibali vya ngoma, na usafirishaji. Hapa pana jambo tu nilikuwa naomba niongeze baada ya vibali vya mtaa ningeomba kiongezeke kitu na mali asili. Na siwezi kuvitamka kwamba ni kitu gani kwani maliasili kidogo inaleta tafsiri ya mazao mengi ya vitu vingi zaidi kuliko kuwa tunataja kimoja kimoja *specific*.

Mhe. Naibu Spika, kwa kuendelea ukurasa wa 210 kifungu cha 19 (4) pana mamlaka ya Sheha. Lakini katika kifungu hiki Mhe. Naibu Spika, mwisho kabisa kimesomeka kwamba Sheha yeyote atapokea taarifa kwamba mtu yeyote katika Sheha yake ametenda kosa anaweza kuamrisha mtu huyo kukamatwa na kuwasilishwa katika kituo cha Polisi kilicho karibu na yeye haraka iwezekanavyo. Iwapo haitowezekana kufanya hivyo anaweza kutaka mtu huyo kuwekwa katika kizuizi kilicho salama kwa muda usiozidi masaa sita kabla ya kuwasilishwa Polisi. Lakini naona kumepunguza nguvu za Sheha kwa sababu tunajua Sheha ana-*deal* na watu wenye matatizo mbali mbali.

Sasa na Sheha atakapokuwa na nguvu kisheria kidogo jamii inakuwa inamughofu katika suala zima la uwajibikaji wa kazi zake. Sasa tunapompa nguvu hii tu kwamba ya kumuweka katika maeneo kwa muda usiozidi masaa sita kabla ya kuwasilishwa Polisi; sasa ningehisi na ule uwezo tuliokuwa tumempa nadhani katika Sheria ya sasa uwezo tuliompa wa kumuweka mtu ndani kwa muda usiozidi masaa 24 mimi nahisi pia ile nguvu yake Sheha angerejeshewa, ili kumpa nguvu katika utendaji wa majukumu yake.

Vyenginevyo mtu anakuwa anajua tu aah, hana la kunifanya masaa sita anaenda Polisi na Polisi anafanya mambo yake kazi imemalizika. Lakini tutakapompa na ule muda wa kumuweka kizuizini kwa muda usiozidi masaa 24 kama kuna suala la kufunguliwa mashtaka basi atafunguliwa mashtaka. Mimi nafikiri nguvu ile ya kisheria Sheha tungeweza kumrejeshea.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia kabisa nakuomba niende kwenye ukurasa wa 215 kiapo au tamko linalofanywa na Sheha. Mhe. Naibu Spika, mimi kidogo hapa nataka Mhe. Waziri atakapokuja anisaidie kiapo kimeanza na "mimi tunaenda na jina lakini naapa kwa *Allah*". Sasa mashaka niliyokuwa nayo tutakuwa tuna Masheha waislamu watupu? kwa sababu itakapokuwa tayari Sheria imeshatamka kwamba naapa kwa "*Allah*" . Sasa mimi nahisi Mhe. Naibu Spika, hapa tungeiweka na *strok* aidha mtu anaweza akaapa naapa kwa "*Allah*" au unaweza ukaapa kwa "Jina la yesu Kristo" kwa imani ya dini yake.

Kwa sababu huwezi kumlazimisha mtu mkristo ukamlazimisha kuapa kwa "*Allah*". Sasa mimi nafikiri kwamba vyenginevyo kama tutakuwa tuna Masheha waislamu watupu sina tatizo na Sheria ilivyowekwa. Lakini kama tutakuwa tuna watu ambao ni mchanganyiko kama imani za nchi yetu zilivyo kwamba nchi yetu haina dini kila mtu ana dini yake, kila mtu ana imani yake kila mtu anaweza kuapa kwa kiapo anachokiamini. Basi ningeomba na hapa pafanyiwe marekebisho ili mtu aape kwa imani ya dini yake anayoiamini. Baada ya mchango huo Mhe. Naibu Spika, nakushukuru na kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa jimbo la Kwahani naunga mkono Mswada huu. Ahsante sana.

Mhe. Makame Mshimba Mbarouk: Mhe. Naibu Spika, kwanza na mimi nishukuru kwa Mwenyezi Mungu *alhamdulillah* kuwa leo hii mpaka sasa hivi dakika hizi nimo kwenye manusura ya uhai wenye salama.

Mhe. Naibu Spika, nianze kidogo na mimi nimeshituka kumsikia mwenzangu hapa aliposema kuwa kiapo hiki kimeanza na naapa kwa "*Allah*". Mhe. Naibu Spika, tafsiri ni nzuri sana lakini kwa sote tuliopo hapa tunaemuona ni huyu mmoja tu. Kwa hiyo, mimi ningeomba kidogo kwa wazee tunaona hapa wa kuweza kutusaidia zaidi kuweka Sheria ya kuweza kuweka vizuri katika kiapo. Kwa sababu hapa Mhe. Naibu Spika, alisema Mjumbe wangu swahiba wangu katika kifungu kile cha kumuweka Sheha na kumuondolea elimu alisema kuwa angalau huyu awe na elimu ya *qur-ani* ya kutosha. Sasa naomba na hapa tuweke sawa.

Mimi naomba tuweke mtu ambaye anaejua kusoma tu kwa sababu tukisema tumuweke mtu mwenye *qur-ani* ya kutosha katika Usheha ndiyo hii itabakia pale pale. Kwa hiyo, naomba sana waziri na wanasheria wengine wataalamu wa lugha ili waweze kunisaidia na mimi katika fikra hizo kuweka sawa, nilitaka nianze hapo.

Mhe. Naibu Spika, jana mimi mara nyingi sana huwa nikisema jambo, kwanza huwa nafanya *research* ya lile jambo au mara nyingi sana huwa naoteshwa usingizini kutokana na hali halisi ilivyo na uchungu wa nchi katika mambo haya. Mhe. Naibu Spika, nilikataa sana kifungu kile cha kuwa Mhe. Waziri asiweze kuwaapishaWakurugenzi pamoja na Makatibu wake na nilisema kwa nia nzuri tu. Sasa naomba leo nitoe ushahidi tosha.

Naomba Mhe. Naibu Spika, uniridhie nisome barua ili waziri.. pia waziri wangu namuamini Mheshimiwa wangu kwanza hasa nimpe sifa moja ni jasiri mzuri sana, ni mtekelezaji na hii wizara kwa kusema ukweli sasa hivi imejaa ghilba yeye mwenyewe *alhamdulillah* unavyomuona mtanashati mzuri, na wizara imejipamba vizuri sana. Kusema la ukweli na hasa katika vikosi humo ukiangalia sasa hivi ukimtaja waziri kwa ubaya unapigwa kibao kutokana na anavyojitahidi. Lakini mambo mengine namuomba Mhe. Rais amkubalie waziri ayatekeleze kwa sababu mambo mengine yako kwenye jukumu la Rais kumpa amri yeye kuyatelekeza, lakini wizara anaimudu.

Kwa hiyo, Mhe. Naibu Spika, na hili nitakalolisema si dhani kama itafika mchana leo Mhe. Naibu Spika, hataweza kulifanikisha. Mhe. Naibu Spika, nina mwananchi wangu amedhulumiwa, amedhalilishwa na nitasoma barua hali halisi ilivyojitokeza. Mhe. Naibu Spika, huyu ndugu anaitwa Juma Fadhil Juma barua inatoka katika Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" kusimamishwa kazi.

"Tafadhali rejea kichwa cha habari cha barua hii kama inavyosomekana hapo hapo juu. Afisi wa Halmashauri ya Wilaya ya Kaskazini "B" Unguja imeamua kukusimamisha kazi ndugu Juma Fadhil Juma, mwenye anuani namba haikuonekana ya muajiri kama inavyosomekana hapo juu ambaye ni mlinzi wa Ofisi hiyo hapo Kinduni. Kuanzia tarehe ya barua hii ofisi imeamua kumsimamisha kazi kwa kosa la kushindwa kukamilisha kiwango cha maadili ya kazi ambapo ni sawa na Kanuni ya Utumishi wa Umma 2014 kifungu cha 31(f) kinaeleza kwamba yafuatayo:-

> "Kwa kuzingatia kiwango cha juu cha maadili kuwatii viongozi wa Serikali iliyoko madarakani ambapo imepelekea kuvunjika heshima na kuishushia hadhi ofisi hii ambapo pia ni kwenda kinyume na kifungu cha 32 cha Sheria hiyo hiyo ya Kanuni za Utumishi wa Umma na kinachoeleza miiko ya Watumishi wa Umma na mkataba wake unaruhusiwa kuwajibishwa kwa kukupa adhabu yoyote itakayoonekana inafaa ndani ya miezi mitatu ya awali baada ya kujazwa kwake ikiwa ni kipindi cha majaribio iwapo itaonekana ukiukwaji wa maadili katika kazi kwa viongozi".

Kutokana na sababu hizo ofisi imefatilia imeridhishwa vya kutosha na inakusimamisha kazi rasmi na mara tu baada ya kupokea kwa barua hiyo ofisi itakulipa mshahara wa mwezi mmoja ikiwa kwa ajili ya majukumu ya ndani ya mwezi mmoja kwanza na utumishi ukiwa hapo kazini.

Tunakutakia kila la kheri".

Mhe. Naibu Spika, hakuna karipio, hakuna barua ya kumwita kwa kuona..yale utafiti wa waliojinasibu humu kuwa umefatilia na kuweza kumpa ni kumuonea na kumnyanyasa. Mhe. Naibu Spika, tunatakiwa tuwe na maadili mazuri na tunapokuwa na maadili mazuri binaadamu kukosea hapa na pale mahaluku tabu, tumepewa hilo suala na binaadamu kukiri nalo. Kifungu hiki amepewa kuweza kukiri kutokufanya jambo lile au amelifanya jambo lile.

Mhe. Naibu Spika, hili nilitakaa kwa sababu hata katibu huyu Madiwani wengi walimkataa kaekwa pale kwa shindikizo tu, ni mambo mengi tu nitakuja kuyasema huko mbele au niite mimi nitakwambia ninayo mengi kuliko haya. Sasa na yeye aajibishwe si kakiuka maadili yapo mengi ya kukiuka maadili. Lakini kwa kuwa kiongozi amekamata rungu kumnyanyasa yule mnyonge, masikini, yatima ana watoto wa kuongoza. Sasa mimi naomba Mhe. Naibu Spika, hili nakuamini waziri wangu, mjasiri kabisa, naomba. Nimesema mimi sitounga mkono wala sitotamka baada ya kupata jibu zuri ya hili.

Hilo naomba, shemegi naomba radhi sana nataka nikuungie mkono kweli kweli. Lakini limeniuma ndani ya moyo, nimekonda dakika kusikia mwananchi wangu amedhalilishwa kiasi hiki bila la kupewa onyo lolote, au karipio lolote W*h*y tunakwenda wapi?

Sasa ndio jana nikawa mkali sana katika kifungu hiki. Kwa sababu huyu angeapishwa na Rais angekumbuka uso wa Rais Dr. Ali Shein angeogopa kufanya manyago kama hayo. Ninaomba Mheshimiwa nisaidie kwa hili nikuungie mkono, tena nitakuungia mkono kweli kwa sababu kitu ulichokifanya kizuri katika hii historia yangu mimi sijapata

kuona kuletwa Mswada kama huu tangu nianze kazi hii. Ahsante sana kwa ushujaa wako. Mhe. Naibu Spika, nianze kuchangia sasa.

Mhe. Naibu Spika, sina haja tena kumwagia sifa waziri wangu, nimeshamalizia. Sasa naingia katika vifungu ambavyo Mheshimiwa nimeona nisaidie sana. Mheshimiwa ni kweli tunataka kuleta Tawala za Mikoa. Mhe. Naibu Spika, Wakuu wa Mikoa wetu kwanza hawana hizi fani, hawana fedha hapa mimi kidogo napata mashaka na laiti ingelikuwa Bajeti yetu hii inawapelekea kikamilifu fedha za kukidhi mambo ya kuleta maendeleo kwa wananchi, basi mimi ningesema *alhamdulillah* hasa kwa Sheria hii. Lakini nasikitika sana sijui waziri utapata wapi pesa za kuwapelekea hawa wakamilishe malengo hayo waliokusudia.

Kifungu cha 203 Mhe. Naibu Spika, niende (c) moja kwa moja umesema uzoefu. Mimi nakubaliana nao uzoefu huu sipingi basi hata kijishahada hakioneshi humu, uzoefu sawa naomba kidogo angalau shahada basi iweko ya aina yoyote ili tumpambe vizuri huyu Mkuu wa Mkoa wetu. Naomba sana Mheshimiwa kifungu hiki kiangalie Mheshimiwa wangu na Mwanasheria kwa sababu Mwanasheria mzuri nakupenda sana Mwanasheria wangu na wewe *alhamdulillah*. Lakini kuna mambo mengine tusaidiane maarifa kwa sababu kuna vitu ambavyo ni *totally experience*. Huku nyuma kulikuwa hakuna, sasa hivi unaleta *new* kama ukileta *new* basi kuna sentensi lazima zibadilike.

Sasa naomba sana kuna *hansard* nyengine kwa mzee wangu Mhe. Ali Mzee Ali sijaziona zile kabisa katika historia ya vitabu vya nyuma, lakini hivi vitu vipya. Sasa mimi naomba tulete na vitu vidogo tumsaidie Mkuu wa Mkoa kutokana na hali halisi *at least* basi kiwepo na kifungu kinasema awe na Shahada yaa.. Mheshimiwa hapo nimalizie wewe naomba niwekee sawa ili tuweze kufanya kazi vizuri.

Lakini Mhe. Naibu Spika, nikiingia ukurasa wa 204. Hapa kuna mambo ambayo yameingiliana na suala la vigezo vya Sheha. Mhe. Naibu Spika, ninasema ninakubaliana nalo. Anasema kwamba kwa madhumuni ya ubora na ufanisi wa utekelezaji wa Serikali hii katika ngazi za Shehia, Waziri kwa kushauriana na Mkuu wa Mkoa anaweza kupendekeza kwa Rais kuanzisha Shehia. Ni kweli Mhe. Naibu Spika, hiki kifungu ninakubaliana nacho, ni sawa kwa sababu yule ni *President*. Haina utata sheria hii hapa Mhe. Naibu Spikia, lakini kuna kitu kitakuwa kina-*delay time* hapa, kwa makusudi sijui hebu nitaomba hivi ili iwe sheria, *how many people* wanatakiwa pale. Mimi sioni kutokana na kuambiwa hivyo, tunaambiwa mgao wa idadi ya watu tu, watu gani ili kuweza kutengeneza Shehia.

Kwa maana hiyo mambo mengine sheria hii tuiangalie vizuri baadae atatokea mjanja atakuja kutupiga *qualified* kitu hapa. Sharti tuangalie tuone hii sheria inatwambiaje, tusione taabu kuweka ili hii sheria iweze kukata mipaka iambiwe Shehia kuwe na watu kadhaa.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana hili suala kwa sababu inapokuwa Shehia imetimilia kwa mujibu wa sheria ambazo utakuja kuniambiwa wewe, basi pale ni kweli maendeleo yanapatikana kwa urahisi. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, kuna Shehia nyengine kwa mfano kama Jimbo letu la Kitope ni kubwa; sehemu ya Kipandoni pale wanataka Sheha na wanajitahidi kuleta maendeleo lakini yenyewe Sheha mmoja ana maeneo makubwa. Sasa tumsaidie, mimi naomba tumsaidie sana. Tulijaribu sana ku-*fight* hili suala lakini kwa kuwa unaleta sheria sasa na wewe linakukamata hilo suala. Ni vizuri sana kuwa kinakuja kitu na *memory* yake inakuja ndani yake.

Sasa ndio maana nikasema kuwa hapa nisilipigie debe sana pengine pale watu namba ndogo, nikaonekana mimi sieleweki na ndio maana ninalitia kidogo kidogo, hatukuliona ile hali halisi. Kwa sababu pale wanataka maendeleo wananchi wa Kipandoni na wanajitahidi sana Mhe. Naibu Spika, naomba sana na wao wajinafasi, wajisikie raha katika tunda hili la mapinduzi linawafikia pale watu wa Kipandoni kwa kupata Sheha yao.

Namba itakuwa kubwa, utajua wewe mwenyewe, wapi utafanya nini. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, hilo suala liweze kukubalika kwa mujibu wa sheria wa kifungu hiki wapi utaliweka. Ninakuomba sana Mhe. Naibu Spika.

Mhe. Naibu Spika, lakini kifungu cha 8. Mwenzangu alikizungumza sana, mimi ninakwenda kwa ufanisi.

Mhe. Naibu Spika, hii (f) sifa ni sifa, tukubaliane hilo. Mimi ninakubali kuna wazee wengine wanasoma Kiarabu kina muda mrefu ambacho kina ujuzi zaidi. Sasa hivi kina taaluma hasa unapata vyeti mpaka unafika diploma, *certificate* na kuendelea. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, lakini mimi sisemi kama lazima awe na kidato cha nne, hapana. Mimi ningeomba angalau ajue kusoma na kuandika katika haki zote anazozijua yeye za kuweza kutafsiri kwa misingi ambayo dini inavyoonesha sehemu zote. Ninaomba sana kiwekwe hicho ili aweze ku-*run* pale kuweza kuhukumu vizuri.

Mhe. Naibu Spika, Sheha ni mtu mkubwa sana, si kitu cha masikhara. Sheha anapeperusha bendera, mimi Mwakilishi sipeperushi. Kwa kuwa Sheha ni mtu mzito sana. Sasa si rahisi tu tuchukue Masheha, tuokoteokote tu tuseme tuweke Masheha, hapana.

Mhe. Naibu Spika, halafu ninataka nikusaidie tunapowachagua Masheha lazima tuwaelimisha sheria. Mhe. Naibu Spika, *experience* yangu hasa katika jimbo langu, Masheha wangu wengi ninakubali sheria hawazitambui kwa ukamilifu, ninakubali hilo. Ningekuwa na fungu la fedha kama mungenipa basi ningewasomesha sheria kwa sababu mimi mwenyewe ninaipenda sana sheria na sipendi sana Sheha wangu aweze kufanya kitu ambacho kilichokuwa hakina msingi kabisa kuweza kutoa hukumu kwa jamii. naomba sana hilo tuweze kusaidiana katika utekelezaji wetu mzuri sana.

Mhe. Naibu Spika, nikiingia katika ukurasa huo huo wa 205, kuna suala hili la kushauriana na Wilaya na Waziri bila ya kuathiri sheria kama ataondolewa kazini Mkuu wa Mkoa. Maana yake hii ameshindwa utekelezaji, hapa hakumuona uzuri. Sheria hii hii inakwenda kwa Mkuu wa Mkoa. Sheria hii hii inakwenda kwa Mkuu wa Wilaya, hebu naomba jamani nisikilizeni vizuri. Ninatoa ushauri wa bure mimi hapa. Ameshindwa utekelezaji wa majukumu yake kutokana na uzembe au matatizo ya kiafya.

Mhe. Naibu Spika, binadamu mimi ninaomba hii isiwe ndio *issue* ya kuweza kumuondoa mara moja, kwa sababu naomba nikitafsiri tena.

> "Bila ya kujali masharti ya sheria hii, Sheha ataondolewa kazini na Mkuu wa Mkoa husika baada ya kushauriana na Mkuu wa Wilaya na kuthibitishwa ikiwa..."

Mhe. Naibu Spika, tutaondoa Masheha wengi, ninakubali kiwepo lakini *action* yake inakuwa ndogo, *why*, tatizo lipo wapi.

Mhe. Naibu Spika, Masheha wengi *failure*, hiyo niseme ukweli wala tusifichane. Kwa matatizo tu haya haya ya uzembe mdogo mdogo, yanatufikisha kutuweka pahala pabaya. Sheha wengine wanahatarisha vijiji na vijiji kugombana au vijiji pale wenyewe wananchi wa pale vijijini wanafika kugombana wao wenyewe kwa wenyewe. Sasa Mhe. Naibu Spika, kama kweli kweli hasa tutakuwa hatuna Masheha. Masheha hawa watakuwa hawana *time* ya kukaa, mara leo mutawaondoa, keshokutwa mutawaondoa. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, hii adhabu hii ninakubali asilimia mia kwa mia lakini i-*take action* kwa wakati unaotakiwa, tusichukue muda mrefu.

Lakini tatizo letu Mhe. Naibu Spika, tuna muda mrefu utapelekewa malalamiko kwa Sheha fulani hatumtaki na *reason* inakubalika na wanatoa vielelezo wananchi. Kwa sababu mwananchi ndiye mwenye kukupa heshima wewe Sheha, mwananchi ndiye mwenye kukulinda wewe Sheha na wewe Sheha inatakiwa mwananchi umlinde kwa sheria, umuelimishe afahamu nini anachotakiwa pale. Mhe. Naibu Spika, hawajui kuwa Sheha ile ni *Local Government* pale ya kushushia maendeleo kutoka kwa Wilaya, wakati Mkoa inaleta maendeleo kwa Wilaya na Wilaya inamshushia Sheha. Mhe. Naibu Spika, Masheha wengi hawafahamu kazi zao namna hiyo.

Mhe. Naibu Spika, utakuta na kwa sababu unapofanya kazi vizuri Sheha unamsaidia Mhe. Mbunge, unamsaidia Mhe. Mwakilishi, lakini hebu uliza wewe lini Sheha angalau umempigia simu Mhe. Mwakilishi au Mbunge kumwambia kuna tatizo moja, mbili, tatu. Sheha anapopita mkono wa kushoto, Mwakilishi au Mbunge anapita mkono wa kulia. Sasa mimi naona Mhe. Naibu Spika, hawafahamu kabisa, yeye mtu akishaambiwa Sheha anaona mimi Sheha basi ndio Sheha tu.

Sasa mimi naomba Mhe. Naibu Spika, tuwe *alert* sana waifahamu hii sheria. Sasa haina mzaha kabisa na tutaipitisha hapa, *wallahi* tutaipitisha wala usiwe na wasi wasi Mheshimiwa wangu kabisa, hasa mimi nitaipitisha sana baada ya kunifurahisha, sina tatizo na wewe unanijua mimi. Jana nimekupitishia dede na sisi wengine ni Masharifu, mimi sijasema hata siku moja mdomo wangu ukaanguka pabaya, hata siku moja. Ninalosema *alhamdulillah* Serikali inatekeleza, mambo mengi tu, nikiondoka hapa *alhadulillah* nimeweka historia katika Baraza hili, amini kabisa Mheshimiwa.

Mhe. Naibu Spika, ninataka kukwambia kitu kimoja, kwani kusoma ndio kutambua mengi, haiwezekani, Mheshimiwa wangu mimi na wewe ni sawa sawa hatujui, hatukusoma lakini tunafanya kazi vizuri. Nitakupa mfano wengine kuwa ni Kiingereza, kwani nikitoa mfano wa Kiingereza mtu hawezi kufahamu. Nikisema kuwa *attention please, all passengers boarding pass for nine three but come back go*, nani hajafahamu kiswahili, eeh! sio kuzungumza. Sasa mimi ninaona Mhe. Naibu Spika, hiyo ni moja katika *just* kuona mtu jinsi gani ambavyo anakwenda. Hii ni moja katika bashrafu ya kuendelea na Mswada huu uwe mzuri. *(Kicheko/Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, nimesema kuwa kifungu hiki ni lazima tukirekebishe. Sasa ninaingia katika ukurasa wa 206. Mhe. Naibu Spika, halafu ubaya zaidi hapa katika huu ukurasa wa 12 Majukumu ya Mkuu wa Mkoa. Mhe. Naibu Spika, hapa ninataka nimsaidie Mhe. Rais kidogo. Mhe. Naibu Spika, tunakuwa na muda mwingi sana wa kuteuliwa Wakuu wa Mikoa, lakini mimi ningeomba Mhe. Mwanasheria Mkuu, naomba sana kungekuwa na kifungu ambacho kikaonesha utaratibu jinsi ya kumrahisisha Mhe. Rais, kuweza kupata Mkuu wa Mkoa kwa haraka. Kwa sababu Afisa Tawala wa Mkoa ana *experience* tosha, hakuna haja tena ya kutafuta mtu mwengine.

Hebu tuone kifungu hiki Mhe. Naibu Spika, tumsaidie Rais, mambo mengi haoni, isipokuwa ndio maana tukaitwa Wawakilishi na ndio maana pakawepo na Mawaziri, ndio maana wakawepo Makatibu, na ndio maana kukawepo wanasheria. Sasa mimi ninaomba hili ili Rais asipate taabu, avute tu aangalie sheria aah! Kuna Afisa Tawala kule tayari amesoma vizuri, tayari ana *experience*.

Mhe. Naibu Spika, ninaomba sana ili kuweza kufanikisha vizuri haya malengo na kuweza kufikisha hapo. Naomba sana kifungu hicho ili kiweze kufanikisha kupata maana nzuri sana. Kwa hivyo itakuwa ni utaratibu mzuri wa kumrahisishia kazi Mheshimiwa wangu Rais wa Zanzibar kwa kuweza kuvuta ili kuweza kutufikisha pahali pazuri sana. Mheshimiwa naomba hilo na kwa uwezo wa Mwenyezi Mungu atufikishe pahali pazuri sana. Kwa sababu Mhe. Naibu Spika, ili kuweza kufanikisha Mkuu wa Mkoa tusichukue muda wa kuweza kumpatia pale, kwa sababu huyu Afisa Tawala anafanya kazi za Mkuu wa Mkoa, ana umri wa Mkuu wa Mkoa, ana elimu nzuri, ana muda tosha wa kuweza kufanya kazi pale.

Sasa naomba Mhe. Naibu Spika, aniwekee vizuri kifungu hicho ili kuweza kufanikisha suala hilo kwa kuweza kumpachika huyo mtu, kuweza kufanikisha masuala ambayo yanaleta heri na baraka. Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna suala hili la kumuweka mtu ndani. Kuna mtu tu unaweza ukafanya kwa makusudi kumuonea, basi unaweza ukachukua muda uka-*timing* Ijumaa ukamuweka ndani *over*, wakati inatakiwa ukimkamata tu *faster* Mahakamani. Sasa niambie Ijumaa umemuweka ndani, Jumamosi, Jumapili Mahakama ipo wapi.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba na hilo lipunguzwe ukali wake, kutiwa ndani wajibu wakati ni mkorofi lakini tujaribu kukimbiza muda ambao *time* zile za wakati uliokuwa hakuna kazi, tutamu-*affect* sana yule mtu. Naomba sana Mhe. Naibu Spika, hii tujaribu kuitengeneza vizuri. Mimi ninachoomba kuwa tuwe na lengo la kumkamata wakati wa kazi ili kwa kuweza kufanikisha kazi yetu iende vizuri na yule mtu aweze kujua kama sasa kuna dola.

Kwa sababu kuna watu kwa makusudi wanakuja kukuchezea chezea, wanachezea chezea tu. Sasa wanapokuwa wanachezea kuona kweli sheria ina makali basi muweke ndani sawa, lakini tuangalie muda ambao wa kumuweka ndani vizuri wakati ule wa kazi, umtafutie *time* za Jumatatu, mkamate pale pale anaangukia Mahakamani, Mahakamani rumande mchezo umekwisha.

Mhe. Naibu Spika, ningeomba hapa kidogo nimeingiwa na wasi wasi sana kuwa mtu anaweza akatengeneza sheria yake.

Mhe. Naibu Spika, namalizia kwenye 209. Hapa Sheha atawajibika kwa Mkuu wa Wilaya. Hapa Mhe. Naibu Spika, mimi sina tatizo nalo lakini atawajibika vipi. Tafsiri mimi naomba sana hapa kuwajibika kwake kivipi. Kuwajibika kwake kuwa hatoweza kutenda kazi mpaka akamuone Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Wilaya atashuka chini kwa kwenda kumwambia fanya hili moja. Hebu kidogo hapa tuweke vizuri sentesi hii, kwa sababu hapa kuwajibika au atakwenda kutii amri tu kwa Mkuu wa Wilaya kila siku, kuripoti kila siku.

Sasa kidogo hebu tuweke vizuri hii tafsiri, kuwajibika kivipi, kiutendaji, akusanye maendeleo, akusanye nini halafu akapeleke kule au *daily report* aende kila siku pale kuripoti kwa Mkuu wa Wilaya. Sasa mimi naomba hapa kidogo niwekewe tafsiri vizuri sana.

Lakini Mhe. Naibu Spika, kuna kifungu hiki cha (c) kuweka kumbukumbu za nyaraka. Mhe. Naibu Spika, Sheha hana ofisi, Sheha ana nyumba. Sasa Mhe. Naibu Spika, mimi ninaamini kitu chochote kipya kiendane na mazingira mapya. Kuwepo na kumbukumbu ninakubaliana nalo kuwepo na vitabu ambavyo vya kumbukumbu na kweli kumbukumbu zozote Mhe. Naibu Spika, zitokane na huku chini, halafu ziende juu. Mhe. Naibu Spika, mimi naomba sana hicho kitu, Mhe. Waziri jaribu kuwa *modern*.

Waheshimiwa Wawakilishi hatujapata ofisi lakini sawa, lakini Sheha muhimu, mimi wala simuonei choyo, Sheha ukimjengea ofisi sioni taabu kabisa kwa sababu yeye ndivyo inavyotakiwa yule afanye kazi kwa umakini na kwa umahiri kabisa, ajue watu wake wangapi katika ile Shehia yake, leo ataweka wapi. Vijumba vyenyewe hivi mara vinaripuka moto, hebu niambie. Mtu unamuona yupo kule Sheha unamuona yupo ndani mwake. Naomba na hili Mhe. Naibu Spika, kwa kupitia mkono wa Serikali Kuu tuwasaidie Masheha kupata na wao ofisi zenye mantiki nzuri.

Wenzetu Wabunge ofisi wanazo sawa, sioni wivu kwa kuwa ndio wajibu wao, ndio fungu lao wameekewa. Sasa na sisi angalau Sheha wetu awe na ofisi ijapokuwa kichumba kimoja na ukumbi. Mimi ninaamini Mhe. Waziri wangu shupavu hilo suala utaweza kufikisha na kuweza kuwaletea maendeleo watu.

Mhe. Naibu Spika, kuna neno hapa kuwa Kamati za Maendeleo. Kamati hizi za Maendeleo kifungu cha 2 kuna neno la wazee, hebu naomba kidogo wazee, kutakuwa na wazee. Hii hebu nisaidie wazee watu wazima. Ninajua watu wazima kuna *level*, hata mimi sasa hivi ni mtu mzima kwa sababu nina miaka arobaini naa, tayari sasa hivi ninaweza hata kuwa Rais kwa mujibu wa sheria. Lakini alivyokusudia huyu mzee wa aina gani au hirimu gani. Hivi vitu naomba jamani kidogo Mhe. Waziri tusividharau. Ni vitu unaviona vidogo vidogo au utaona mimi ninafanya uchepe, sio uchepe kwa sababu ni moja katika mantiki ya sheria; sheria haitaki mchezo wala mzaha. Sheria jambo dogo tu linakutia makosani.

Mhe. Naibu Spika, mtu anaweza akakuuliza tu, wewe siku hiyo mimi nilivaa shati la aina gani na kifungo kilikuwa rangi gani. Utapotea *steps* tayari yule anachukua *points*, kumbe maskini ya Mungu shati alilovaa lilikuwa jeusi na vifungo rangi kijani, wewe umekwenda kusema vifungo vyekundu. Sheria tayari imeonekana kama wewe unasema uwongo. Kwa hivyo Mhe. Naibu Spika, naomba hapa nisaidie sana kwa sababu wazee ni kitu muhimu, wazee ni muhimu ninakuunga mkono *totally*. Lakini mzee siye miye usinichukue miye. Sasa mimi naomba hapa niweke ule umri wa wale wazee uliowakusudia wa kuweza kuweka katika kadhia hii uliyokusudia hapa. Naomba sana Mheshimiwa tuweke suala hilo na mimi ninakukubalia kabisa.

Mhe.Naibu Spika, nishuke chini, hapa kuna tafsiri ya 29, hebu nisaidie Baraza la Wawakilishi litatenga fedha kwa kila sekretarieti ya Mkoa kuwezesha kukidhi matumizi ya kukabiliwa. Mhe. Naibu Spika, Baraza la Wawakilishi, sasa ninajiuliza Baraza la Wawakilishi linatokana na bajeti yenyewe tunavyoletewa na Waziri au Baraza la Wawakilishi litakuwa na *special* fungu. Maana yake hii sijui tafsiri ikoje.

Kwanza ninajua kuna mambo mengi, mimi bwana alivyonifundisha Maalim Abdalla Mwinyi shurti ufahamu uzuri lugha zile, lugha zinakuwa na tafsiri zaidi ya tatu. Utakapokuja umekosea kidogo tu, utakwa umetukana au umejitukana au umejishitaki.

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi naomba kifungu hiki nina wasi wasi sana isijekuwa sisi Baraza la Wawakilishi ndio tutakuwa na fungu la kuwatengenezea hawa sekretarieti yenyewe. Kama ni hilo, sisi wenyewe Wawakilishi hatuna hapa, sasa sijui itakuwaje Mhe. Naibu Spika, hapa sijui. Maana yake huo Mswada wenyewe Wawakilishi sijui kama umeshapita ule, kama umepita ule sawa tunakubaliana nalo tutakuwa na vifungu tunaweza kuwasaidieni. Lakini mswada wenyewe mpaka leo unapigwa danadana, hatujui tukoje Mheshimiwa tunaelea tu.

Sasa mimi nafikiria tuangalie vizuri Mhe. waziri, nisaidie tafsiri hii, ili niweze kukusaidia zaidi katika ufanisi uliokuwa mzuri sana. Lakini suala la Katibu wa Sheha, mimi kuwa *Form VI* wala sioni tatizo, nakuunga mkono asilimia mia kwa mia, hili sina tatizo. Kwa sababu katibu huyu ndiye atakayemsaidia huyu sheha ambaye niliyekuwa nimeshamnyima mabanda humu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, huyu katibu ndiyo ataweza kumsaidia huyu sheha ambaye niliyekuwa nimeshaanza kumnyima mabanda, kwa maana hiyo sidhani kama huyu katibu atakuwa na *Form VI* yake aende akaitupe ovyo mule katika shehia, sidhani kitu kama hivyo. Basi mimi naomba kwa kumlinda *Form VI,* tumuweke angalau Darasa la 12.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana tumnyang'anye hiyo *Form VI* tumuwekee Darasa la 12 safi tunaanzia hapo, naomba tuanzie hapo ni *fresh* kabisa hiyo. Tuanzie hapo Darasa la 12 na katibu wa sheha awepo, *Wallah* tutakuwa *wonderful,* kwa sababu mtu *Form IV* tayari akili zimeshakuwa katika hali ya kujijenga vizuri sana. Naomba hapo, halafu yule yule sheha ataweza ku-*plan* mambo ambayo ni ya utekelezaji mzuri.

Mhe. Naibu Spika, namalizia dakika tano kwa kusema kuwa wakuu wa mikoa, mimi sijaona kifungu cha kupewa *power* ya kuweza kufanya miradi yao na kuipeleka sehemu, aidha kwa mwanasheria kutafuta wawekezaji, humu sijaona hatujawapa *power* hiyo, tunawanyima baadhi ya mambo ya haki, kwa sababu mikoa na wilaya ndiyo yenye watu.

Sasa hivi mimi sioni kwa sababu ninachochelea sasa hivi kila kitu ikiwa wizara moja kufanya maendeleo hatufiki na ndio maana Zanzibar leo ni ndogo tu, ukiiweka kwenye mkono hapa kwangu mimi haienei, lakini tunashindwa kuleta maendeleo. Sasa tuwe wawazi na tuwe wakweli tusiwe na choyo, tuwapende wakuu wa mikoa ili waweze kutafuta wawekezaji.

Mimi nataka kusema *Wallah Laathim* simpendi mtu, nampenda mtu kwa tabia zake na vitendo vyake. Mhe. Mkuu wa Mkoa wangu wa Kaskazini Mhe. Pemba, kaondoka ametuachia mradi wa gesi kule *deep sea* inatengenezwa wakati wowote, ndio tunavyotaka tena mradi mkubwa sana. Wakati wowote pale panahitajika watu 300 kupata kazi. Sasa mimi nafikiria mambo kama hayo waengezwe wapewe *power*.

Mhe. Naibu Spika, naomba sana suala hili tuoneshe katika sheria hii, tuwaruhusu. Sheria kama haipo ndio tunaunda sisi hapa, sisi ndio waundaji sheria na hii tumeletewa mpaka sasa hivi ni kitu ambacho hakijakamilika ndio maana tukaletewa mswada, mswada uliokuwa haujakamilika, sisi ndio tuukamilishe. Kwa sababu waliokaa ni watu na sisi tunaochangia ni watu. Kwa hivyo, mimi naomba kuwa tuwape meno wakuu wa mikoa kwa kutafuta wawekezaji nje na ndani, ili kufanikisha malengo yao

Mhe. Naibu Spika, Serikali Kuu haitakuwa na shida kwa sababu tukikaa kwa kungoja Serikali Kuu, inategemea kuna wengine wanakuwa wanaona uchungu wa kuleta maendeleo, lakini wengine mpaka leo mtu anazubaa, mtu anashindwa kusaini barua tu. Mimi naomba tuwape fursa hiyo na tuwape heshima hiyo.

Mhe. Naibu Spika, kwa kumalizia nasema kuwa Mhe. waziri, jemedari wangu, njoo unijibu na mimi unifurahishe Mhe. waziri, ninakupa asilimia 50 na 50, naitia mfukoni unipe maneno matamu sana. Ila sio lazima uje unijibu kwenye ukumbi hapa, aah! niite pembeni tu, ukiniita pembeni basi *automatically* nakumalizia asilimia 100, kwa sababu itakuwa imeshajiingiza naweka kwenye *Hansard* kabisa hapa. Akiniita pembeni sina haja tena ya ku-*review* kusema nairudisha, itakuwa imeshaingia *automatically*. Akiniita tu pembeni basi naunga mkono kutokana na suala hili. Ahsante sana.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Mhe. Naibu Spika, kwanza nianze kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuniwezesha asubuhi hii kusimama hapa mbele ya Baraza lako tukufu kuweza kutoa mchango wangu mfupi sana kuhusu mswada huu uliopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, pia, nikupongeze wewe kwa kunipa nafasi ya tatu ya kuwa msemaji katika mswada huu.Mimi kidogo nimepata hofu ndogo kuwa wakati tunaanza mkutano huu tulikuwa tunakuja na miswada miwili; mswada mmoja ulikuwa ni wakunga na waunguzi na mmoja ule wa maadili ya viongizo. Lakini huu mmoja baadae kwa sababu moja au nyengine ulitoweka na hatimaye ukaingizwa mswada mwengine wa kuanzisha shirika la nyumba. Baadaye imekuja miswada miwili kwa Shahada ya dharura, ambapo mmoja ulijadiliwa jana na mmoja ndio tunaujadili hapa leo.

Sasa aliyefanya hivyo ni haki yake, niseme hivyo. Lakini miswada miwili ya dharura kuja kwa mpigo, yaani kwa wakati mmoja, kidogo nilikuwa na wasi wasi fulani isijekuwa kuna kitu nyuma yake. Nilisoma kitabu kimoja kinasema, kuna hadithi mbele ya kila kitu ikiwa kila mmoja anajua hivyo. Kuja kwa miswada hii miwili kwa pamoja, *there is a story behind it. As there is a story behind everything if only one knows.* Mimi sijui, lakini itakuwa

kuna kitu maalum, ndio maana miswada hii miwili ambayo inafanana kidogo ikaletwa kwa hati hiyo katika kipindi hiki kwa pamoja.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu unaonekana ni mdogo, lakini ni miongoni mwa miswada mikubwa sana.

Mhe. Naibu Spika: Mhe. Mjumbe, ngoja nikuweke sawa kidogo, hebu kaa kitako. Mswada wa Maadili ya Viongozi Kamati ya Baraza la Wawakilishi ndio iliyozuwia kutokana na bado haujawa sawa, walipendekeza Serikalini ukarekebishwe halafu utaletwa. Haukuondoshwa tu, Kamati ya Wawakilishi baadhi yenu walikaa na wakaona bado haujakaa vizuri urejeshwe ili kikao kijacho uletwe, haukuondoshwa bila ya sababu. Endelea kuchangia.

Mhe. Mohammed Haji Khalid: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, nakushukuru. Kwa hivyo, kuja kwa miswada hii miwili kwa mpigo kidogo imenipa wasi wasi. Mswada huu kwenye karatasi unaonekana kuwa ni mdogo sana kuliko miswada mingi. Lakini ni mswada mkubwa sana na wenye mambo makubwa sana kuliko miswada mingi na pindipo mswada huu tutauidhinisha kwa sheria na vifungu vyote kama vilivyo, kutakuwa na athari ya baadhi ya vifungu kwa wananchi wetu.

Mhe. Naibu Spika, labda itokezee bahati nzuri baadhi ya vifungu vipingwe na vikubalike huwenda ukawa mzuri. Lakini kama tutavipitisha vifungu vyote viliomo humu kama vilivyo, hofu yangu inaweza kuwa ni ya kweli.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu ni wa Tawala za Mikoa na watu wote waliotajwa humu, wametajwa kuwa ni watumishi wa umma na kama ni watu ambao kimtazamo ni miongoni mwa watumishi wa Serikali Kuu katika daraja yao, kwa sababu Rais katika mkoa anawakilishwa na mkuu wa mkoa, Rais katika wilaya anawakilishwa na mkuu wa wilaya na katika shehia anawakilishwa na sheha aliyeteuliwa na Mhe. Mkuu wa Mkoa.

Kwa hivyo, watu wote waliomo humu sheha na naibu wake mkuu wa mkoa na katibu tawala wake, mkuu wa wilaya na wengineo ni watu wakubwa sana na kazi zao ni muhimu kweli kweli. Lakini baadhi ya mamlaka tu waliopewa ndio kidogo yananitia hofu.

Mhe. Naibu Spika, nianzie na ukurasa wa 203, kifungu cha 4(3)(a) hadi (c), kinasema; "Kutaanzishwa Afisi ya Tawala za Mikoa katika kila mkoa na wilaya ndogo na shehia, kwa lengo la utekelezaji wa majukumu ya kazi za Serikali Kuu". Ina maana hawa ni watekelezaji wa kazi ya Serikali Kuu kwa kupitia ngazi zao.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu (c), kinasema; "Afisi za Tawala za Mikoa zitaongozwa na Mkuu wa Mkoa katika Mkoa, Mkuu wa Wilaya katika wilaya na sheha katika shehia". Katika mfumo huu wa kiutawala, viongozi wote waliotajwa ni kama watumishi wa umma. Kwa hivyo, uongozi wao unahitajika uwe wa hekima, busara na uajibikaji kwa sababu moja kwa moja wanawatumikia wananchi. Hawa wote ni wateule kila mmoja kwa ngazi inayohusika.

Mhe. Naibu Spika, lakini sheria hii pengine ni ya marekebisho au inafuta sheria nyengine. Ukiacha wakuu wa mikoa, wakuu wa wilaya na afisa tawala, hawa Waheshimiwa masheha ambao ndio watumishi wa mwanzo, mimi naita wa mwanzo na wengine wataita kuwa ni wa mwisho, lakini wote ndio watumishi wa msingi tunaowaona huko chini. Hawa tunawaita kuwa ni watumishi wa umma kulingana na sheria hii ikiwa sheria na ndio maana ikawa wanachaguliwa.

Mhe. Naibu Spika, je, hawa wanateuliwa kwa vigezo gani, pengine humu vitakuwa vimetajwa. Kwa sababu hawa wanaitwa kuwa ni watumishi wa umma kuoneshea kuwa hawana msimamo wa chama cha siasa. Je, hivyo ni kweli, kwa sababu Zanzibar hii ni wa kuchagua aliyekuwa hana chama cha siasa tena vile vyama viwili vilivyokuwemo humu ndani, ni wa kutatufa, yaani ni adimu na nadra kumpata.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, hawa wanateuliwa masheha na Mhe. Mkuu wa Mkoa, baada ya kushauriana na Mhe. Mkuu wa Wilaya husika. Hivi ninavyofikiria mimi hakitokuwa ni kigezo, lakini ninavyoamini ni moja katika vigezo vya kuwapata hawa Waheshimiwa masheha. Nasema hivyo kwa sababu katika jimbo langu nina masheha saba, wote ni wa upande mmoja tu, ingawaje tunasema hatuhutubii siasa, lakini ni kwa mdomo kiukweli hawa wanateuliwa kwa imani zao. Moja ya kigezo ni imani yao ya kisiasa.*(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, haya mamlaka aliyopewa Mhe. Sheha ya kuweza kumkamata mtu. Kwa sababu wote hawa kuanzia Mhe. Mkuu wa Mkoa, Mhe. Mkuu wa Wilaya, Mhe. Sheha, wote mamlaka haya ya kuwakamata watu wamepewa. Kuna kipindi kitafika watu watakamatwa kwa sababu ambazo hazijulikani.

Prof. Makame Mshimba pale kasema, mtu anaweza kuamka vibaya tu kwa mtu mwengine kwa sababu amri hiyo anayo, basi akatoa amri akamatwe mtu fulani. Kwa hivyo, ningeomba kifungu kile mamlaka makubwa kama yale ambayo Rais ndio anayamiliki, haya ningeomba yasikasimiwe kwa watu wengine.

Mhe. Naibu Spika, miongoni mwa sifa za sheha ile iliyoondolewa ya kielimu, mimi sioni kwa nini iondolewe, kwa kigezo kuwa Mbunge na Mwakilishi anatakiwa ajuwe kusoma na kuandika tu. Mbunge na Mwakilishi ni kiongozi wa kisiasa, hawa tunasema kuwa ni viongozi wa utumishi wa umma. Kwa hivyo, kwa hali yoyote awe na elimu inayojulikana na ile ya kidato cha nne iliyoondolewa ningeomba irudishwe, si unatakiwa ufanisi wa utendaji wa kazi, kwa hivyo, awe na elimu na elimu hii ya Darasa la 12...kwa watu wenye umri wa miaka 40 mpaka zaidi ya hapo, elimu hii sio adimu ipo.

Kwa hivyo, kuiondoa kwa sababu yoyote ile sio haki, kwa sababu huyu ni mtumishi wa umma tena wa karne hii tuliyonayo leo, tunasema tunakwenda katika utendaji bora. Kwa hivyo, ningeomba hiki kiwango cha elimu kilichoondolewa kirejeshwe, ili kupata masheha ambao watashirikiana na makatibu wao kuleta ufanisi katika shehia zao.

Mhe. Naibu Spika, hivyo hivyo kwa Mhe. Mkuu wa Mkoa na Wilaya na miongoni mwa zote walizopewa ziweko sifa za kielimu, lakini isiwe sifa kuwa mzoefu wa miaka 13 tu, yaani isiwe ana uzoefu wa miaka 13 iwe ndio kigezo kikubwa cha sifa ya kuweza kupata hiyo nafasi.

Kwa hivyo, lazima na sifa nyengine ya ziada ya kielimu iwe ipo kwa kiwango gani kwa kuwa sheha katakiwa awe angalau elimu ya *Form IV* na katibu wake awe angalau kidato cha sita, basi angalau awe na *diploma*.

Mhe. Naibu Spika, nitazame kidogo kifungu ambacho nilikizungumza bila ya kukiangalia kifungu cha 13(1) ilioko kwenye ukurasa wa 206, ambacho kinasema hivi "Mkuu wa Mkoa anaweza kutoa amri ya kukamatwa mtu yeyote endapo ana sababu za kuamini kwamba hapa yametajwa mambo na anatakiwa aamini kwamba huyo mtu anayo;

(a) "Mtu huyo anaelekea kuvunja amani au kuchafua utulivu wa wananchi".

Sasa hapa atakuwa na kigezo gani cha kumjua mtu kuwa huyu sasa ameelekea katika kuvunja amani.

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli hapa kifungu hiki naomba kifutwe cha 13 na wala sio kirekebishwe. Kuna mahali tukifika watu watafanya shughuli zao kihalali na kutokana na zile harakati zao na watu wengine kuona kwamba huyu atatufanyia hivi, basi itatoka amri kwa mkuu wa mkoa, yaani *so and so* muhifadhi, nadhani na hili ndio lengo lake peke yake, yaani ni moja nafikiria hivyo. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika, itafika wakati kifungu hiki kitumike kinyume na utaratibu kwa kufikiria tu kwamba huyu anakusudia kufanya hivi muweke pale, nadhani tusirudi huko tena. Kwa hivyo, kifungu hiki ningeomba kifutwe na kama kuna chengine ambacho kitakuwa kizuri kwa wananchi basi kiwekwe badala yake.

Mhe. Naibu Spika, sikukusudia niseme maneno mengi. Lakini haya machache niliyosema kwamba hivi sasa siungi mkono mswada huu hadi pale ambapo nitapata ufafanuzi wa baadhi ya vifungu kwamba lile lengo, nia, madhumuni na dhamira yake ya kuingizwa hapa.

Mhe. Naibu Spika, katika viongozi waliotajwa naibu sheha hakutajwa na sifa yoyote amewekwa tu kwamba kutakuwa na naibu sheha. Sasa sijui naibu sheha na yeye atakuwa ni muajiriwa kama alivyo sheha au ni mtu ametajwa tu kama na yeye atakuwa yumo katika msururu wa viongozi. Kwa hiyo, naomba nijue na yeye ni muajiriwa au yeye anakaa pale kama naibu wa sheha tu.

Mhe. Naibu Spika, katibu wa sheha ni mtu ambaye ana elimu inayofikia kidatu cha sita, ni wazo zuri, kwa sababu kuna vijana wetu wengi hawana kazi na nchi hii ina shehia nyingi basi angalau hao vijana maalum wataweza kupata kazi kupunguza mrundikano wa vijana ambao wanazurura ovyo bila ya kazi yoyote.

Mhe. Naibu Spika, kuhusu ugawaji wa shehia pamoja na mambo mengine, kwamba Mhe. waziri, atamshauri Mhe. Rais juu ya ugawaji wa mipaka ya shehia. Kisiwa chetu ni kimoja na watu wetu ni wa aina moja, muingiliano wetu ni mkubwa sana baina ya hapa na pale, sijui kigezo cha shehia sehemu hiyo ina sifa gani, ili iweze kupata sifa kwamba hapa sasa tuanzishe shehia mpya.

Je, itategemea idadi ya watu, ukubwa wa eneo au kutegemea nini, ili kuona kuwa Mhe. waziri, hapa kunastahiki sasa kuwe kuna shehia nyengine baada ya shehia hii iliopo. Kwa kweli, sio kama kuna mpango wa kuona kwamba ndogo tupunguze shehia.

Lakini kwa maoni yangu shehia itapanuliwa au itaongezwa, kwa sababu masheha kama mawazo yangu yalivyo ni watu maalum na kuna kipindi watakuwa wanafanya kazi maalum, kwa hiyo, hawa watakuwa hawapunguzi isipokuwa wataongezwa, kwa ajili ya kukidhi yale matakwa maalum.

Mhe. Naibu Spika, kama nilivyosema kwamba sina mchango mkubwa, ningeomba nimalizie hapo na ninasema kwamba nakushukuru kwa kunipa nafasi. Ahsante sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante na wewe nakushukuru. Sasa nafasi tunampa Mhe. Hamad Masoud Hamad na baadae Mhe. Panya Ali Abdalla na baada ya hapo afuatie Mhe. Mohammed Mbwana Hamad.

Mhe. Hamad Masoud Hamad: Mhe. Naibu Spika, na mimi nikushukuru kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia mswada huu ambao hivi sasa uko mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, nakwenda kwenye kifungu 6(2) kinasema; "Kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake, Rais atamthibitisha na kumteua Kaimu Mkuu wa Mkoa au Wilaya kuwa Mkuu wa Mkoa au Wilaya".

Swali langu kwa Mhe. mwanasheria mkuu na zaidi Mhe. waziri, ambaye ameleta mswada huu, ni kwamba kwa ufahamu wangu mimi Rais atamthibitisha na kumteua kaimu mkuu wa mkoa. Maana yake hapa Rais analazimishwa, kwa sababu ukeshakuwa kaimu mkuu wa mkoa ufahamu wangu mimi ni kwamba Rais akuthibitishe, je, hapa huwezi kuwa kaimu mkuu wa mkoa, lakini Rais akaona hufai atateua mtu mwengine kuwa mkuu wa mkoa, nafikiri hilo swali limeeleweka.

Vile vile, kwenye kifungu cha 8 kuhusu Uteuzi na Sifa za Sheha. Sikubaliani na mapendekezo ya Kamati ya Katiba, Sheria na Utawala kufuta kifungu 8(2)(f) mwenye cheti cha kidato cha nne au zaidi. Sheha tumesema ni muajiriwa wa Serikali na matangazo yote ya waajiriwa wa Serikali tunasikia alete kitambulisho cha Mzanzibari na alete cheti halisi sio nakala ya mafunzo hayapungui *Form IV* wala sijasikia *Form III*, *Form II* wala *Standard VIII*.

Mhe. Naibu Spika, wanaoajiriwa siku hizi ni kuanzia darasa la 12 na hawa ni waajiriwa wa Serikali na wala sio viongozi wa kisiasa, kwa sababu sio Mbunge wala Mwakilishi kwamba ukeshakujua kusoma na kuandika wewe sawa sawa na profesa, lakini hawa ni waajiriwa wa Serikali. *(Makofi)*

Sasa inakuwaje hawa uwajiri wao unakuwa tofauti na wengine na ingekuwa hakuna watu wa darasa la 12, ni adimu sawa, lakini kuna maelfu kwa maelfu, yaani watoto wetu waliomaliza darasa la 12 wanaweza kuandika na kusoma na wana maarifa mazuri, kwa nini hatuwapi fursa hizi?

Kwa hivyo, mimi mapendekezo ya Kamati nimeyasoma hapa kwamba kifungu hiki kifutwe na iwe anajua kusoma na kuandika tu na wametoa mfano kwamba Mbunge, Mwakilishi na hata Mhe. Ali Salum Haji, kwamba Mbunge na Mwakilishi musimfananishe na muajiwa wa Serikali.

Mhe. Naibu Spika, kwa ufanisi wa shehia zetu kiwango cha elimu kwa sheha kina umuhimu wake na sheria hii ilipotungwa naamini kwamba watu walizingatia uzoefu wa watu uliopita. Kwa kweli, masheha hawakuanza jana na wameanza tangu 1995 kama sikosei, yaani tuna zaidi ya miaka 20, sasa matatizo ya masheha wasiojua kuandika na kusoma yanajulikana, leo kwa nini unarudia kule kule, watoto wa *Form IV* wapo na ni wanetu, yaani ni Wazanzibari halisi.

Kutokana na hali hiyo, nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, kwamba sheha aekewe kiwango na hichyo kiwango ambacho kimewekwa kinatosha, yaani darasa la 12 tena awe na cheti.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha 8(5) ni kama vile ambavyo nimezungumzia kuhusu kuteuliwa na kuthibitishwa hapa inazungumza kwamba kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya Utumishi wa Umma na Kanuni zake Mkuu wa Mkoa atamthibitisha na kumteua kaimu sheha kuwa sheha, swali langu liko pale pale.

Kwa kweli hii maana yake ni kwamba ukeshakuwa kaimu sheha lazima uwe sheha au unaweza kuwa kaimu sheha na halafu mkuu wa mkoa anaona wewe hufai kuwa sheha na akachagua au akateua sheha na wewe ukaendelea kuwa naibu sheha.

Kwa hivyo, nasema kukaimu isilazimike kwamba lazima uwe cheo kile, nakusudia kukaimu usheha si lazima uwe sheha, yaani sio lazima uthibitishwe, isipokuwa aachiwe mkuu wa mkoa kama wewe amekuchagua kuwa kaimu, basi anaweza kuteua mtu mwengine yeyote anayefaa zaidi kuliko wewe.

Mhe. Naibu Spika, kifungu 9, kinasema; "Bila ya kujali masharti ya sheria hii, sheha ataondolewa kazini na mkuu wa mkoa wa mkoa husika baada ya kushauriana na mkuu wa wilaya na kuthibitishwa na waziri ikiwa;

(a) "Ameshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na uzembe au matatizo ya kiafya".

Mhe. Naibu Spika, haitoshi kwa sababu kuna masheha ibada yao ni ukorofi na mimi nitakupa mfano hapa hapa. Kwa mfano mimi jimbo langu lina shehia saba, yaani ninao masheha saba na leo sitaji majina, lakini naamini kwa sababu mswada huu unaendelea na mkuu wa wilaya ya Wete yupo na mkuu wa mkoa wa Kaskazini Pemba yupo. Sasa huko nyuma na mpaka kesho wengine wameshtakiwa polisi linasomwa shtaka Mahakamani unashtakiwa kwa kosa la uzembe na ukorofi, sasa uzembe na ukorofi ni vitu viwili tofauti.

Mhe. Naibu Spika, anapokwenda mtu kwa sheha na kila anachotakiwa awe nacho kama vile cheti cha kuzaliwa, uthibitisho kwamba yeye amekaa pale kuliko huyo sheha na halafu sheha akamwambia sasa hii ofisi yangu haifanyikazi usiku, anakwenda asubuhi sheha hayupo, mchana sheha hayupo, anapokwenda magharibi sheha hayupo na ukenda saa mbili sheha anakwambia aaa! Ofisi yangu mimi hivi sasa haifanyikazi njoo kesho asubuhi na ukenda asubuhi hayupo.

Kwa maana hiyo, kuna watu wamehangaishwa na wanaendelea kuhangaishwa, kuna vijana zaidi ya 60 wamekwenda kwa masheha hawa na hii ni wiki ya tatu, mmoja amenipigia simu na kuniambia kwamba sheha kaniambia hivi sasa tunakwenda kwa vingi, ili tupate vitambulisho kwa ajili ya Kura ya Maoni. Sasa huu ni ukorofi, uzembe ama afya, maana yake pengine akili yako haiko sawa.

Mhe. Naibu Spika, moja katika jambo kubwa la masheha wengi ni ukorofi na ukorofi unathibitika kwa vitendo wanavyofanya. Kwa mfano mimi mwenyewe tukimaliza Baraza nimeamua kwenda jimboni kwangu na vijana wangu wote kwa masheha wanipe sababu kwa nini wamewahangaisha wiki ya tatu hii na mwengine anasema aaa! Mimi habari hii musije ila Ijumaa, yaani sheha anasema yeye siku yake ya kufanya kazi kutoa fomu na hiyo ni kutoa fomu tu, ili uweze kupata kitambulisho cha Mzanzibari unakwenda kwa sheha anakupa fomu na habari ya vyeti vya kuzaliwa hamuhusu sheha, ndivyo tulivyokubaliana hapa.

Kwa kweli tulikubaliana wakati wa ziara yetu na aliyekuwa waziri anayehusika na vitambulisho Mhe. Dkt. Mwinyihaji Makame Mwadini na tumekwenda wilaya zote Pemba na wakaelezwa vizuri suala la kudai vyeti halikuhusuni nyinyi, basi pale pale kama huna cheti fomu hakupi na suala la vyeti vya kuzaliwa ni wilayani.

Lakini masheha hao wa ukorofi wao ndio maana nasisitiza suala la ukorofi liwemo humu na sio afya na uzembe tu isipokuwa ukorofi ndio ibada yao baadhi ya masheha wengi na nimesema leo sitaji majina, isipokuwa nawapa nafasi wakuu wa wilaya na wakuu wa mikoa walirekebishe hili, vyenginevyo, hatua za kisheria zikiongozwa na mimi mwenyewe zitachukuliwa.

Mhe. Naibu Spika, kwa hivyo, kwamba ukorofi uwekwe kwamba ni moja katika vitu ambavyo sheha vinaweza vikamuondoa madarakani au katika nafasi ile ikithibitika na ithibati itakuwa ni vielelezo vya vitendo ambavyo amefanya kwa muda mrefu.

Vile vile, kifungu cha 11, kuhusu sifa kidato cha sita au zaidi, ndiyo yale yale kiwango cha elimu na huo ni ukurasa wa 205. Nawaomba Waheshimiwa Wajumbe, tusisitize kiwango cha katibu wa shehia kisipungue, anakuwa ni mtendaji na sheha tumeambiwa ana mambo chungu nzima ya kufanya akiwa na Katibu mzuri kwa maana ya uadilifu na hata kiwango cha elimu basi kazi nyingi za sheha zitafanywa na yeye. Katika sheria iliyopita na hata zoezi la sasa hivi hatuna katibu wa shehia hii ni nafasi mpya wapewe vijana wenye uwezo wako wengi hatuna hata pa kuwaajiria, yaani uajiri haupo, kwa hivyo, hiyo ni moja na hawa nasema tena ni wafanyakazi wa Serikali, hawa si viongozi wa kisiasa. Kwa hivyo, sifa ya kwamba ajue kusoma na kuandika hapa hai-*apply,* kwa hivyo, ibaki hivyo hivyo kidado cha sita.

Kifungu cha 13 ukurasa wa 206, kuhusu Mamlaka ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya. Kifungu cha (a) "Mkuu wa Mkoa anaweza kutoa amri ya kukamatwa mtu yoyote endapo ana sababu za kuaminika kwamba mtu huyo anaelekea kuvunja amani au kuchafua utulivu kwa wananchi". Mimi nipo hapa kwenye mtu yoyote nichukue mfano tu kwa Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi, Wajumbe wa Baraza la Wawakilishi si mtu yoyote na hata kukamatwa kwake kuna *procedure* hii.

Sheria si kila mtu ataifahamu kama tunavyoifahamu sisi hapa, wala usishangae kwamba Mkuu wa Mkoa mwenyewe sheria hii hatoifahamu. Sheria hii itakuja kuchafua amani tena kwa makusudi kwa sababu inapita hapa saa hizi, mimi mkuu wa mkoa akitoa amri nikamatwe, pana kazi ndio na inaweza kuwa ni binaadamu pengine ana chuki zake, je, pengine tumekosana, je, huko mitaani.

Sasa mimi nafikiri kifanyiwe marekebisho hiki kifungu, isiwe mtu yeyote labda iwekwe kwa sheria nyengine ambazo mtu huwezi tu kwenda kumkamata, kwa hivyo, nasema nimetoa mfano Mwakilishi, Mbunge si mtu yeyote hapo, mfanyiwe marekebisho.

Jengine kifungu cha 14, Kamati ya Sheria wameongeza hapa 14(1), kuna (a)(b)(c) mpaka (i) wakasema kwamba iongezwe (m) na hiyo ambayo iongezwe inasema. Kutoa vibali vya mkusanyiko, mikusanyiko mengine yoyote ambayo sio ya kisiasa, kidini na utamaduni. Jamani mkuu wa wilaya, *of course,* ni ofisa, lakini atoe vibali, unaponambia mkusanyiko, hata semina ni mkusanyiko. Sasa mkuu wa wilaya atoe vibali, hebu iangalieni vizuri hapa au tuiangalie vizuri zaidi, kwani sasa hivi sheria iliyokuwepo ina tatizo gani au utaratibu uliopo una matatizo gani kwa nini tunaingiza utaratibu ambao huko mbele utakuja kutuletea matatizo.

Kuna kifungu kimoja yupo hapa sheha katika majukumu yake anatakiwa kupokea taarifa ya mikutano hadhara, kupokea au asipopokea, je, huo mkutano wa hadhara haupo, ndio maana yake au sio chango nyengine hiyo ni *pressure* nyengine. Waheshimiwa, nataka kutoa *challenge* hapa, Mhe. waziri, ataniambia sheha mmoja tu sitaki wawili hiyo kazi itakuwa kubwa kwa waziri mmoja tu ambaye si CCM. Nasema vipi kwa sababu nataka niambiwe sheha huyu mmoja, Pemba kuna masheha ambao ni CCM kuliko hapa Unguja. (*Makofi*)

Kwa ufupi hakuna sheha ambaye si CCM, sasa unaposema apokee taarifa ya mkutano wa hadhara, yaani nasema mkutano wa CUF unafanyika na sheha sikumpa taarifa, ni moja katika majukumu yake akiita polisi wakija wakipiga watu virungu na wakirusha mawe wakipigana si uvunjifu wa amani, kwa nini tunajiingiza mambo ambayo wala sio ya lazima? Mhe. Waziri, akija hapa kama nilivyosema jana alisema mswada huu hauna hadaa, sasa hujasema hadaa lakini mambo yaliyomo humu ndio yanaonyesha kama kuna hadaa.

Sasa hii ya sheha kupokea taarifa ya mikutano ya hadhara, mimi naomba iondolewe haina tatizo lolote tunafanya mikutano yetu tangu vyama vingi vimeanza hakuna tatizo, *of course,* ile ni heshima tu kumwambia sheha kwamba tuna mkutano wa hadhara sawa, lakini isiwekwe kwenye sheria ikawa yeye anatumia sheria sasa hivi kufanya mambo yake na ku-*apply* ukorofi wake na haya yatatokea tu.

Kifungu 19(4) kinaelezea sheha yeyote atakayepokea taarifa kwamba mtu yeyote katika shehia yake ametenda kosa la jinai anaweza kuamrisha mtu huyo akakamatwa na kuwasilishwa katika kituo cha polisi kilichopo karibu nae, huyu sheha nani atakayemuamrisha? Sheha atamuamrisha polisi amkamate mtu, ndio apelekwe kituo cha polisi.Kwa hivyo, hapa tupaangalie vizuri sheha atamuamrisha nani amkamate mtu na huyo mtu baadae ndio apelekwe polisi.

Kwa hivyo, lazima tupate mtu wa kumkamata hapa, mtu anayekamatwa na polisi hakuna matatizo, lakini wewe tu uone watu njiani wanapita na shughuli zao uwaambie jamani ee, nikamatieni, yule akipigwa mapanga maana wengine watakaokamatwa pengine ni walevi wako chakari. Kwa hivyo, nafikiri hivi vitu tungeangalia, ni utaratibu gani utumike wa sheha kumuamrisha mtu amkamate mtu na hiyo sheria iwe inakubalika?

Kifungu cha 22 kinahusu Kamati ya Maendeleo ya Mkoa itatekeleza kazi zifuatazo, nimezisoma zote (a),(b),(c),(d),(e),(f) mpaka (J), lakini kuna kazi humu nadhani kwa mawazo yangu ni muhimu sana kimesahauliwa, kwa hivyo, naomba nipendekeze na hiyo iwemo, kubuni na kuandaa waraka au nyaraka kwa kuomba au kutafuta miradi kwa maeneo mbali mbali katika mkoa wake.

Mhe. Naibu Spika, tulikwenda kutembelea Mkoa wa Kigoma kwenye Kamati ya Mawasiliano na Ujenzi mwaka 2008, tuliyoyakuta kule ni kwamba ule mkoa wenyewe una timu ya kuandaa, kubuni na kuandaa miradi na wanaomba miradi na inakuja kwenye Serikali ya Tanzania, lakini chanzo na chem chem ya mradi ule inatoka pale kwenye mkoa, sasa Kamati ya Maendeleo ya Mkoa isiwe tu ni kufuatilia sera na hivi na hivi. Lazima kuwe na kitengo cha kubuni na hata kuandika miradi kwa ajili ya maeneo mbali mbali ya mkoa ule.

Kwa hivyo, nilikuwa napendekeza kwamba hiyo nayo iwe ni miongoni mwa kazi, si lazima upate mradi, lakini ukifanya mtihani kuna mambo mawili utafeli au utapasi ukipasi ndio umepita, lakini kama hukufanya mtihani maana yake wewe umefeli, sasa ukiandika mradi ukaomba, una *two possibilities* unaweza ukapata ndio utakuwa umeshapata tena hiyo na ukikosa hakuna hasara hawa watu wameajiriwa kwa ajili ya kufanya kazi. Kwa hivyo, hiyo nilikuwa naomba sana kabisa iingizwe katika hilo.

Mhe. Naibu Spika, kifungu cha mwisho ambacho nataka nimalizie mchango ni kifungu cha 34 kinahusu kufuta na kubakiza, Sheria ya Tawala za Mikoa namba 1 ya mwaka 1998 inafutwa, lakini kifungu cha pili 34(2), kinasema; "Bila ya kuathiri kufutwa kwa sheria hiyo jambo lolote lililofanywa chini ya masharti ya sheria iliyofutwa zitaendelea kutumika mpaka tarehe ya kuanza kutumika kwa sheria hii na litachukuliwa kama kwamba limefanywa chini ya masharti ya sheria hii hadi litakapofutwa au kubadilishwa".

Sasa ufahamu wangu pengine wanasheria hapa huu mswada umeletwa kwa hati ya dharura na kuna sheria nyingi Waheshimiwa tunazipitisha hapa, lakini kutumika kwake kunachukua muda mrefu, mfano sheria hii tukiipitisha na labda pengine Rais akachukua ule umuhimu wa dharura, akaisaini na sidhani kama Rais anasaini hapa, ila ni waziri.

Ninavyofahamu mimi ni kwamba masheha walioko hapa mfano tukikubaliana au sheria hii ikipita kwamba kiwango cha chini cha elimu cha sheha ni *Form IV* na sheria hii baada ya wiki mbili ikawa tayari kwa sababu ya udharura, ufahamu wangu mimi kwa kifungu hichi ni kwamba ni mpaka sheha huyo afutwe, yule aliyekuwepo sasa hivi aliye na elimu ya ngumbaro na kuwepo udharura wa sheria hii, siuwoni kuwa utakuwepo. Mimi napendekeza kwamba kwa sababu ya udharura wa sheria hii, basi mara itakapotiwa saini iwe ni Rais au waziri vile alivyosema hapa basi *immediately* musiwaache watu kwa maslahi ya kundi fulani wakabaki hapo mpaka yale malengo yakatimia.

Mhe. Naibu Spika, lakini jengine katika hizi nafasi maana yake humu kila kitu kuteua kuteua, hatukatai uteuzi lakini uteuzi ufuatane na vigezo na vigezo utavipata wapi visitoke tu akilini au kichwani mwako kwamba fulani anafaa, watu waombe mfano katibu wa shehia *Form VI* wako wengi tu, kwa nini watu wasiombe, kwa hivyo, mimi napendekeza kwamba uteuzi si tatizo, lakini kuwe na vigezo, huyo waziri atakayeteua mkuu wa wilaya, basi itangazwe, tunatangaza nafasi ya katibu wa shehia fulani viwango ni hivi; awe ni Mzanzibari, awe na kidato na kadhalika, basi patapatikana wengi kabisa, wakishapatikana wengi hapo ndio waziri ateue isimtokee tu kichwani mwake kwamba fulani pengine anafaa apelekewe watu ambao wameomba.

Mhe. Naibu Spika, baada ya mchango huu nasubiri majumuisho ya waziri ili niseme naunga mkono au siungi mkono mswada huu nakushukuru sana. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa sasa ni zamu ya bi Panya Ali Abdalla, baadae Mhe. Mohammed Mbwana Hamad na muda ukibaki Mheshimiwa Abdala Juma Abdala.

Mhe. Panya Ali Abdalla: Ahsante sana Mhe. Naibu Spika, awali ya yote sina budi kuchukua fursa hii na mimi kumshukuru Mwenyezi Mungu *subhana wataala* ambaye ametujaalia kuweza kukutana hapa na kuweza kutekeleza

majukumu yetu ambayo tumetumwa na wananchi wetu, lakini pia, nichukue fursa hii kukushukuru wewe kwa kunipatia na mimi nafasi hii niweze kusema machache katika mswada huu. Lakini tatu, nimshukuru sana Mhe. waziri na mwanasheria mkuu ambao wamejitahidi katika kuandaa mswada huu ili uje uwe manufaa kwa Taifa letu.

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu nilitaka nianze katika kifungu namba tatu kwenye ufafanuzi ambapo kunaonekana kuna Katibu Tawala, kwa upande wetu hapa tulizoea neno hili kuwa Afisa Tawala, kwa hivyo, mimi nilikuwa bado napendekeza neno "Afisa Tawala au Afisa Tawala Mkoa au Wilaya" bado liendelee kutumika badala ya Katibu Tawala.

Mhe. Naibu Spika, pia, niendelee na mchango wangu katika kifungu namba 8(2)(f) ambacho kinaonekana kuna elimu ya sheha ambapo mwanzo imependekezwa iwe kidato cha nne, lakini baadae ikafutwa na kuwekwa kujua kusoma na kuandika, halafu tukienda mbele kule kuna Katibu huyu ambaye atakuwa katibu wa sheha katika kifungu cha namba 11 ambacho kinatakiwa yeye awa na elimu ya kitado cha sita au inayofanana na hicho kitado cha sita.

Mimi hapa nilikuwa nataka ufafanuzi tu Mhe. waziri anijuulishe kwamba naelewa sheha atakuwa ndio mkubwa wa kuongoza hawa Wajumbe wengine waliobaki, sasa elimu ya katibu hii ikija ikiwa kubwa nataka kujua mshahara wao utakuwaje kati ya sheha na huyu katibu, maana yake hofu yangu usije ukawa katibu kutokana na elimu yake anapata mshahara mkubwa halafu ikawa asiweze kupokea yale majukumu atakayopewa na bosi wake kama sheha kwa sababu ndio kiongozi wake mkuu.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kifungu namba tano ambacho kinaeleza na naomba nikinukuu "Kwa mujibu wa masharti ya sheria ya utumishi wa umma na Kanuni zake mkuu wa mkoa atamthibitisha na kumteua kaimu sheha kuwa sheha.", pia, hili nilitaka kujua huu uteuzi au kuthibitishwa huku kunaweza kuchukua muda gani, kwa sababu tumekuwa tukishuhudia watu wengi wanakaimu nafasi kwa muda mrefu kabisa bila kuweza kuthibitishwa au kuteuliwa katika nafasi hizo.Lakini pia, nilitaka kujua kwamba, je, atakapokuwa anakaimu hataweza kulipwa, pia, hilo nilitaka kulielewa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kifungu cha namba 18(2)(c), pia hapa naomba nikinukuu hichi kifungu kinaeleza kwamba; "Kuweka kumbu kumbu za nyaraka zote zinazohusiana na usajili wa ndoa, talaka, vizazi na vifo, vibali vya ngoma, usafirishaji wa mazao, mifugo, vibali vya mkaa na mengineyo kama itakavyoagizwa mara kwa mara na taasisi husika kupitia wilaya husika".

Mhe. Naibu Spika, haya mengine yote sina matatizo nayo tatizo langu niko kwenye hii nyaraka hizi kumbu kumbu za ndoa na talaka, nilitaka kujua kwamba hii kumbu kumbu ya ndoa na talaka itakuwa kumbukumbu pale kwa sheha baada ya mtumiaji husika akeshalitumia maana anajua ndoa na talaka zinashughulikiwa na mashehe au makadhi. Sasa nilitaka kujua labda ile kumbukumbu inakuwa kama ni mrejesho baada ya yule kulitumia lile buku ili lirejeshwe kwa sheha ili iweze kupatikana kumbukumbu ya ndoa na talaka katika ile shehia yake, nilikuwa naomba ufafanuzi juu ya hilo.

Mhe. Naibu Spika, pia, katika kifungu hiki cha 18(e) mimi napendekeza hiki kifungu kupokea taarifa ya kufanyika kwa mikutano ya hadhara kutoka mamlaka husika kifungu hiki kiendelee kuwepo na kiendelee kuwepo kwa sababu gani. Huwezi kuingia katika mtaa wa mtu au nyumba ya mtu bila ya kupiga hodi.

Mhe. Naibu Spika, hiki naomba kiendelee kuwepo kwa sababu unaweza ukafanya mkutano wako na ikawa salama, lakini kama haikuwa salama utaanza kuuliza wewe mwenyewe mtaa huu hauna sheha. Kwa hivyo, kifungu hiki kiwepo kwa sababu ni jana tu tumepitisha mswada ambao unaoeleza kugatua madaraka katika Serikali Kuu na kuzileta katika Serikali hizi ndogo za miji na vijiji. Sasa kugatua kwa madaraka haya basi tayari kuzipa nguvu hizi Serikali za chini kuonekana nazo zina uwezo basi wa kufanya lolote katika shehia yao kwa mujibu wa sheria ilivyowekwa.

Mhe. Naibu Spika, niende tena katika kifungu (h) cha hiyo hiyo 18(2) kinachosema; "Kutekeleza kazi nyengine zozote atakazopewa na mkuu wa wilaya kwa mujibu wa sheria. Hapa mimi nilitaka kuongezeke maneno ambayo isionekane huyu sheha kwamba akipewa agizo na fulani tu ndio aweze kulitekeleza na pengine akipewa na kiongozi mwengine basi asiweze kulitekeleza". Ilikuwa yaongezeka maneno na isomeke; "Kutekeleza kazi nyengine zozote atakazopewa na mkuu wa wilaya na viongozi wengine wa juu huko kwa mujibu wa sheria". Kwamba iwapo atakuja

mkuu wa mkoa au atakuja kiongozi mwengine yeyote wa juu kwa sheha akatoa maagizo ambayo yapo kisheria basi aweze kuyatekeleza.

Mhe. Naibu Spika, niende tena katika kifungu cha 18(3) kwa madhumuni ya kumuwezesha sheha kuhifadhi kumbukumbu za wakaazi wake, mtu yeyote ambaye anakusudia kukaa kwa kudumu katika shehia atalazimika ndani ya siku 30 kujiandikisha kwa sheha husika.

Mhe. Naibu Spika, hapa mimi pia napata wasiwasi na wote na mitaa yetu sasa ilivyoharibika basi nilikuwa napendekeza pia kuwepo hata kama atakaa wiki au wiki mbili lazima akatoe taarifa yoyote kwa sheha kuepusha kwamba inawezekana mtu huyo amefanya kosa kwengine na akikimbilia katika shehia nyengine. Sasa atakapojiorodhesha pale kwa sheha akatambulikana kama kuna mgeni fulani ameingia na hana matatizo yoyote, basi inaweza pia kuhakikisha usalama wetu na wa kwake.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kifungu cha 20(2) ambacho kilikuwa kinaeleza kama kile kifungu chengine ambacho nimekikariri muda mfupi uliopita cha 18(3) kwamba yaongezeke yale maneno ambayo niliyataja na viongozi wengine wa juu pale atakapokuwa sheha anapokea maagizo.

Mhe. Naibu Spika, niende tena katika kifungu cha 22(1)(d), naomba pia nikinukuu kifungu hiki kinasema; "Kuhamasisha watu kushiriki, kuchangia na ikiwezekana kusaidia matumizi mazuri ya raslimali, kulinda mazingira kwa maendeleo mazuri na katika kazi zote za maendeleo ya kitaifa".

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa kazi zinazosisitizwa hapa ni nzuri za raslimali kulinda mazingira na maendeleo mazuri nilikuwa naomba hili neno ikiwezekana basi nalo liondoke ili kwa sababu isiwe kuchangia na ikiwezekana maana yake iwezekane kuyalinda mazingira yetu na kuleta maendeleo mazuri katika shehia zetu.

Mhe. Naibu Spika, katika kifungu cha 22(1)(b) pia kuna neno hapa, naona hili litakuwa *typing error*, naomba nalo lingerekebishwa, kusimamia kazi za maendeleo na mikakati ya mkoa imeandikwa sambasamba, lakini nadhani itakuwa ni sambamba na mpango wa maendeleo kwa Taifa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika jadueli la kiapo, hapa pia mimi nilikuwa napendekeza hili neno "naapa kwa *Allah"* lingeondoka, kwa sababu kama sisi tulivyoapa viapo vyengine basi hatukuweka neno hili, isipokuwa tuliapa pengine naapa kwamba, nathibitisha itakuwa hivi hivi hili, neno "*Allah"* lilikuwa halipo na iwe "naapa kwa dhati na unyenyekevu..." yaendelee na haya maneno mengine na huku mwisho iwe "...ewe Mwenyezi Mungu nisaidie". Tayari ukishathibisha hilo maana yake itakuwa tayari umeshamshirikisha Mwenyezi Mungu katika hicho kiapo chako na hichi naona kwa kuwa wote waumini hata wa dini nyengine wanamuelewa Mwenyezi Mungu, kwa hivyo, wote tunapoapa tunaweza kulitumia neno "ewe Mwenyezi Mungu nisaidie" Kwa hivyo, hapa na badala ya kuwa "ewe Mungu nisaidie" iwe "ewe Mwenyezi Mungu nisaidie".

Mhe. Naibu Spika, mimi mchango wangu ulikuwa si mkubwa, yaani mchango wangu ulikuwa juu ya maneno hayo tu, kwa hivyo, naunga mkono mswada huu kwa asilimia 100 na naomba Mwenyezi Mungu aujaalie mswada tuukubali na tuupitishe kwa maslahi ya Taifa letu.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Mhe. Naibu Spika, awali ya yote na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kujaalia mchana huu kuwepo hapa katika kutekeleza majukumu yetu ambayo yapo mbele yetu. Lakini pia, nichukuwe nafasi ya kumpongeza Mhe. waziri, kwa uwasilishaji wake, lakini pia, nimpongeze Mhe. Mwenyekiti, pia naye kwa uwasilishaji wake uliokuwa wa muda mfupi, lakini uliofafanua vitu vingi.

Mhe. Naibu Spika, baada ya utangulizi huo, naomba kuchangia angalau kwa muhtasari Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tawala za Mikoa, namba 1 ya mwaka 1998 na kuanzisha upya Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza mimi nianze na jadueli katika ukurasa wa 215 unaohusiana na kiapo. Kiapo hiki kimeanza na huyo muhusika sheha;

> "Naapa kwa *Allah* kwa dhati na unyenyekevu, natamka kwamba bila ya woga au upendeleo na kwa upeo wa uwezo na maamuzi yangu".

Mhe. Naibu Spika, neno "maamuzi yangu" yaondoke kwa sababu kinachofuata hapa ni sheria, si maamuzi yake, kwa hivyo, neno hili la maamuzi yake yaondoke. Halafu anasema;

> "Nitaitumikia Zanzibar kwa uadilifu na kwa moyo wangu wote na kwamba nitailinda na kuitetea Katiba ya Zanzibar kwa mujibu wa sheria zilizotungwa".

Mhe. Naibu Spika, sasa kwa kuwa kiapo hiki anaapa sheha wa shehia, mimi naomba nitoe marekebisho na kiapo hiki kiwe kama ifuatavyo;

> "Mimi sheha huyo, ninaapa kwa jina la Mwenyezi Mungu kwamba bila ya woga nitaitumikia kazi yangu ya usheha kwa uadilifu na uaminifu na kwa moyo wangu wote na kwamba nitailinda na kuitetea Katiba ya Zanzibar kwa mujibu wa sheria zilizopo".

Nimeleta marekebisho haya kwa sababu kiapo hiki kinahusu sheha katika mazingira yake ya usheha, lakini kwa sababu Katiba ipo Zanzibar nzima ndani ya shehia zote na nyumba zote, kwa hivyo, anawajibika kuilinda hii Katiba katika hali yoyote.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu, niende katika kifungu nambari 7, kuhusu vigezo vya kuanzisha shehia. Hapa nataka niende nambari 7(3), vigezo vya kuanzisha shehia vitakuwa kama vifuatavyo;

(a) "Urahisi wa kiutawala, uongozi na upatikanaji wa huduma, maeneo yenye huduma za pamoja na mgao wa idadi ya watu".

Mhe. Naibu Spika, kwa kweli baadhi ya maeneo ya shehia ni makubwa sana, inawezekana kwamba sheha mmoja anaweza akalimiliki eneo la kukabili masheha wawili. Kwa hivyo, niungane na wenzangu waliotangulia, Mhe. waziri atufafanulie atuwekee wazi ni idadi gani ya watu ambao wanalazimika ikibidi kuanzisha shehia yao. Kwa hivyo, ninamuomba Mheshimiwa hapa atuwekee wazi, kwa sababu kuna maeneo makubwa na yana sheha mmoja, eneo ambalo linaweza likamilikiwa zaidi ya masheha wawili.

Mhe. Naibu Spika, uteuzi na sifa za sheha. hicho ni kifungu namba 8(1), kinasema; "Kutakuwa na sheha ambaye atakuwa ni mtumishi wa umma atakaeteuliwa na mkuu wa mkoa kwa kushauriana na mkuu wa wilaya husika na kuthibitishwa na waziri kwa ajili ya kutekeleza majukumu na kazi zilizoainishwa na sheria hii au sheria nyengine yoyote zinazotumika Zanzibar".

Mhe. Naibu Spika, kwa kuwa sheha atakuwa ni mtumishi wa umma basi mimi naomba ngazi ya usheha iombwe kama ambavyo wanaomba watumishi wa umma wengine, haidhuru kutakuwa na maombi mengi; mkuu wa wilaya, mkuu wa mkoa au kitengo husika cha kuwafanyia usaili watu hawa wanaweza wakapeleka matokeo ya usaili uliofanywa mkuu wa wilaya na mkuu wa mkoa akaangalia nani ambaye ana sifa zinazostahiki kwa kufuata vigezo vile vya maombi na sifa za maombi kama ambavyo zimetajwa.

Mhe. Naibu Spika, jengine ambalo nataka kulichangia hapa ni hicho hicho kifungu nambari 8(2)(d). Kifungu hiki kinasema kwanza nambari (2), kinasema;

> "Mtu hatateuliwa kuwa sheha isipokuwa ni..."

Sasa naenda kifungu (d) kwamba;

> "Mtu aliyethibitika kwa uadilifu".

Mhe. Naibu Spika, naomba kumuuliza Mhe. waziri, ni nani atakayemthibitisha sheha kuwa muadilifu na vigezo gani ambavyo huyu mthibitishaji ataviangalia kwa sheha huyu naomba Mheshimiwa hapa anipe maelezo ili tuangalie kwamba ni vigezo gani vya uadilifu ambavyo vitafaa kumchagua sheha.

Mhe. Naibu Spika, kifungu chengine ambacho nitakichangia ni kile nambari (2)(f) ambacho kimeeleza, lakini kimefutwa mwenye cheti cha kidato cha nne au zaidi. Kifungu hiki kimefutwa lakini kwa mujibu wa wakati wetu wa sasa kwa kweli kufuta kipengele cha kuwa na kiwango cha elimu bado hatujatenda haki.

Kipengele hiki na mimi napendekeza kirejeshwe kwa sababu tuna vijana wetu wengi wenye umri wa miaka 40 na zaidi na wao wananyemelea kazi hii. Lakini sasa mbali ya kuwa na cheti cha darasa la 12 kungeangaliwa na sifa nyengine miongoni mwa sifa nyengine, kwa kuwa kuna vipengele mbali mbali ambavyo miongoni mwa kazi zake sheha ni kusuluhisha migogoro mbali mbali ikiwa ni pamoja na migogoro ya kijamii, kindoa na mengineyo basi sheha awe angalau na sifa za kiustadhi ustadhi kiasi fulani. Kwa hivyo, sifa hii nayo ingekuwepo ikawa inampamba sheha.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu, niende katika kifungu namba 9, kinasema;

> "Bila kujali masharti ya sheria hii, sheha ataondolewa kazini na mkuu wa mkoa".

Hapa pana mkuu wa mkoa, kwa hivyo, naomba marekebisho yafanywe na mkuu wa mkoa husika baada ya kushauriana na mkuu wa wilaya na kuthibitishwa na waziri ikiwa ameshindwa kutekeleza majukumu yake kutokana na uzembe au matatizo ya kiafya.

Mhe. Naibu Spika, masheha wengi wana tabia ya kiuzembe, kwa nini nikasema wana tabia ya kiuzembe, watu wengi, yaani vijana wengi wanaotaka fomu ofisini kwa masheha kwa ajili ya vitambulisho masheha wanawapangia kalenda kesho, keshokutwa, Jumatano, Ijumaa, huu ni uzembe. Kwa hivyo, suala la neno "uzembe" liekewe nafasi kubwa na jengine ambalo nataka nilizungumzie hapa inapaswa kabisa kabisa masheha wapewe taaluma tosha juu ya kugawa majukumu yao na kusimamia majukumu yao vizuri.

Mhe. Naibu Spika, inasikitisha sana kuona kwamba masheha wanawanyima baadhi ya watu haki zao baadhi ya masheha sio masheha wote, lakini baadhi ya masheha wanawanyima baadhi ya wananchi wao haki zao hili ni tatizo. Kwa hivyo, naomba sana suala hili lipewe nafasi ya kupewa taaluma tena taaluma endelevu, taaluma hii iwafanye masheha kugawa majukumu yao pamoja na haki za wananchi wao bila ya upendeleo wa aina yoyote kwa mujibu wa kiapo walichoapa.

Mhe. Naibu Spika, kuna neno nimelisahau kidogo kule kwenye kiapo na nimelikumbuka hapa. Mimi naiomba Serikali hasa kwa jumla wale wote walio na nafasi za uteuzi na wakalazimika kiapo basi wapewe semina maalum kabla ya kiapo au baada ya kiapo ili kuelekezwa athari za kiapo ukikengeuka au faida za kiapo ukitekeleza kama vile ambavyo umeapa.

Mhe. Naibu Spika, niende katika kifungu cha 9(c), naomba ninukuu;

> "Sheha anaweza kuondolewa ikiwa amefanya kitendo chochote kinyume na maadili ya uongozi".

Mimi napenda nimuulize Mhe. waziri, je, hayo maadili ya uongozi hawa masheha wanayajua na kama maadili ya uongozi hawayajui hili litatekelezeka vipi na hatua gani za dharura zichukuliwe kuelekezwa masheha maadili ya uongozi na si masheha tu pamoja na viongozi wengine ambao wanapaswa kutoa haki katika jamii.

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu, niende katika kifungu nambari 10(2), kinasema;

> "Katibu wa shehia atakuwa katibu wa shehia na atatekeleza majukumu yote ya kisheria na kazi atakazopewa na sheha na mwajiri wake. Hapa kuna sifa za katibu wa shehia. Sifa za katibu wa shehia mimi naziunga mkono kabisa na hiki kifungu (d) ya kiwango cha elimu kwa kweli ina-*matter* sana kwa sababu katibu huyu atakuwa ndiye mtendaji mkuu katika shughuli zote zinazohusiana na shughuli zile ambazo zipo pale kwa sheha".

Mhe. Naibu Spika, nikiendelea na mchango wangu niende katika kifungu nambari 18, kifungu nambari 18 kinasema;

> “Kila sheha atawajibika kwa mkuu wa wilaya”.

Lakini nambari 18 (2) kuna msururu wa maelezo hapa;

"Kila sheha atakuwa na dhamana katika eneo la mamlaka yake kufanya majukumu yafuatayo. Niende nambari (c) kwanza kuweka kumbukumbu za nyaraka zote zinazohusiana na usajili wa ndoa, talaka, vizazi, vifo mpaka mwisho".

Lakini inasikitisha kwamba masheha ofisi zao ni mikoba na nyumba zao kumbukumbu hizi zitakuwa na usalama gani ikiwa masheha hawana ofisi?

Kwa hivyo, niiombe wizara inayohusika tutakapopitisha mswada huu basi kuwe na adhima ya makusudi juu ya suala zima la kuwapatia masheha ofisi kwa ajili ya kutunza kumbukumbu. Lakini nikienda na hicho hicho kifungu 18 (e) kinasema hivi; "Kupokea taarifa za kufanyika kwa mikutano ya hadhara kutoka mamlaka husika".

Hapa naomba ufafanuzi ili huko mbele kusije kukatokea migogoro isiyokuwa ya lazima.

Mhe. Naibu Spika, mwisho wa mchango wangu ni nielekeze katika mikoa. Mkuu wa mkoa amepewa nafasi kubwa na ni wajibu wake kupewa nafasi kubwa, lakini naomba katika kuchangia nafasi hii ya mkoa kwanza ni vyema wakuu wa mikoa nao kuainishwa angalau vigezo vya kielimu wasiachiwe tu kwamba uzoefu wa miaka 13 na mkuu wa wilaya miaka 10 ikawa ndio tu, lakini kuwepo na vigezo vya kielimu.

Mhe. Naibu Spika, lakini pamoja na hayo kuna maelezo ambayo napenda hapa kuyaeleza kwamba kutakuwa na...wakuu wa mikoa kwa ufupi kama ni watumishi wa umma na tunaambiwa kwamba hawa hawahusiani na masuala ya siasa.

Mhe. Naibu Spika, hili mimi siliamini moja kwa moja, kwa sababu kuna baadhi ya wakuu wa mikoa na wakuu wa wilaya walikuwa ni wanasiasa, Wabunge na Wawakilishi, huyu utamuepushaje na siasa. Ni kigezo gani kitachotumika ili kumtumia mkuu wa mkoa kama ni mtumishi wa umma na kumtoa moja kwa moja katika siasa.

Lakini jengine ambalo napenda kulizungumza hapa ni ile nafasi ya mkuu wa mkoa kwamba kumkamata mtu yeyote, yaani kuruhusu mtu yeyote kukatwa yule ambaye ataona mkuu wa mkoa kwamba anahatarisha amani.

Mhe. Naibu Spika, rungu hili kwa kweli unafika wakati kamata kamata inaweza ikawa kubwa sana, nakuomba Mhe. waziri, hili uliangalie kwa upeo sana na kifungu hiki kinaweza kikaja kikatumika vibaya hasa katika vipindi tunavyokwenda vya kisiasa na kampeni. Mkuu wa mkoa anaweza kuona tu kuna mkutano mahali fulani, lakini sipendi kwamba mkutano ule uwe, anapiga simu polisi Kamanda wa Polisi peleka jimbo fulani askari wako kuna kiongozi fulani mkamate na mtie ndani.

Mhe. Naibu Spika, suala hili kwa kweli linapaswa kuangaliwa kwa makini sana, tupo Zanzibar na kuna Serikali ya Umoja wa Kitaifa tuondoeni zile athari ambazo zinaweza kutokea. Unaweza kusema kwamba, aah, hilo haliwezi kutokea, nataka nitoe kisa kimoja hapa, kulikuwa na urafiki wa simba…

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, ukishakutoa kisa umalizie.

Mhe. Mohammed Mbwana Hamad: Haya, kulikuwa na urafiki wa simba, mbwa na mbweha, hawa walikwenda porini kuwinda, walipokwenda porini kuwinda wakakamata wanyama watatu na hawa walikuwa watatu; walikamata mbuzi, kuku na sungura, mpaka umefika wakati wa kugawa simba kama mfalme wa pori akamwambia mbwa gawa. Sasa mbwa aligawa hivi, akamwambia mbuzi wako, sungura wangu, kuku wa mbweha, alichokifanya simba alimpiga kibao mbwa alikufa pale pale, mbweha akenda mbio akamwambia njoo, mbweha akaja anatetemeka akamwambia gawa.

Sasa jamani mbweha akajiuliza nigawe vipi, mbwa ameshakufa hapa hivi sasa kwa kugawa na mimi si naendelea kwenye kifo. Akamwambia sikiliza; mbuzi chakula chako cha asubuhi, huyu sungura chakula chako cha mchana na kuku chakula chako cha usiku, akamwambia nani aliyekufundisha kigawanyo hiki? Akamwambia nimejifunza kigawa hiki baada ya mauti ya mbwa. Namaliza maneno yangu kwa kusema kwamba tumejifunza mengi katika vipindi vilivyopita, amani tuliyonayo tuilinde, tuihifadhi, iwalinde Wazanzibari. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Saleh Nassor Juma: Mhe. Naibu Spika, ahsante sana kwa kujali muda, naomba nifanye mambo yafuatayo.

Kwanza kumshukuru Mwenyezi Mungu kutujaalia kuwa hai, pili vile vile na wewe kama sikufanya hivyo, nitakuwa sikukutendea haki kukushukuru kwa kunipatia nafasi, naambiwa ya upendeleo hapa ya kuweza kutoa mawazo yangu kuhusu hoja iliyopo mbele yetu.

Mhe. Naibu Spika, mswada huu uliokuja kinadharia ni mzuri sana, kinadharia kwa wale watu ambao wanataka kuimarisha utawala bora pamoja na demokrasia na katika hili katika utawala bora huwezi kuwa na utawala bora kama hukuimarisha Serikali za Mitaa, ili Serikali Kuu iwe madhubuti, makini na mahiri katika kusimamia wananchi wake, lazima Serikali za Mitaa ziwepo na ziwe makini mno.

Mhe. Naibu Spika, inaonekana kwamba Serikali imeleta mswada huu sidhani kwamba ni katika misingi ya kuimarisha hizi Serikali au na wao waambie tu kwamba wameleta Serikali za Mitaa katika nchi hii.

Mhe. Naibu Spika, ukiangalia katika kifungu Nambari 7 cha mswada kipo katika ukurasa 204 imezungumzia vigezo vya kuanzishwa kwa shehia. Nilipoangalia vigezo vya kuanzishwa kwa shehia, roho ilinipasuka kwanza nikajiuliza mara mbili, tatu katika nafsi yangu kwamba leo hii kwa kifungu cha 7 (1), naomba kunukuu anasema;

> "Kwa madhumuni ya ubora na ufanisi wa kutekeleza kazi za Serikali katengeneza shehia, waziri kwa kushirikiana na mkuu wa mkoa anaweza kupendekeza kwa Rais kuanzisha shehia na maeneo ya utawala chini ya ngazi ya shehia kama inafaa".

Mhe. Naibu Spika, sasa mimi napata tatizo kidogo, shehia zikishafika mbili au tatu unatakiwa uwe na wadi, ukishakuwa na wadi zaidi ya mbili unatakiwa uwe na jimbo. Sasa mambo haya yananipa wasi wasi kuwaachia watu wawili, yaani waziri na mkuu wa mkoa kutugaia mipaka ya shehia na idadi ya shehia, jambo ambalo tutaathiri hata idadi ya wadi na majimbo.

Sisi kuna jambo tumelifanya katika kutunga sheria mpaka sasa hivi roho ilipo inatukwama sisi wengine, tumeiachia Tume ya Uchaguzi kuipa dhamana ya kuongeza idadi ya majimbo, leo hii Tume ya Uchaguzi inafanya inavyotaka na ni wengi, ni makamishna zaidi ya wa ngapi na Sekretarieti kubwa leo wanawachezea, wakati mwingine wayachezee hivi majimbo, kesho wayachezee vile, keshokutwa wayachezee hivi na sheria nini?

Sasa tunachukua shehia tunawapa watu wawili tu mkuu wa mkoa pamoja na waziri waweke idadi ya shehia katika nchi *this is a political case* na sio kuimarisha demokrasia, yaani hii sio katika kuimarisha demokrasia kabisa, kwa sababu unapoanzisha Serikali za Mitaa ukiangalia *administrative high rack*, yaani kutoka Rais kuja mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya, diwani hapa mpaka kufika sheha, ukiangalia hii *trend decision makers* ni hawa wa chini katika *root*, yaani katika sheha na shehia.

Ni kwamba idadi ya shehia zipangwe na watu wawili, mipaka ya shehia ipangwe na watu wawili halafu ndio wakamueleze Rais, watampotosha Rais wetu. Mimi naamini katika hili mkuu wa mkoa na waziri tu peke yao wanaweza kumpotosha Rais wetu na kama tuseme ni kuimarisha demokrasia kwa nini *decision making* ya idadi ya shehia wasiachiwe wawakilishi wa wananchi. Lazima wa wawakilishi wa wananchi baada ya kukaa na kutafakari kwa kina kwamba kwa mujibu wa vigezo hivi panataka kuanzishwa shehia nyingine, waamue Wawakilishi wa wananchi, aidha iwe ni Baraza hili la Madiwani au Baraza hili la Wawakilishi ndio wafanye hivyo. Lakini kwa kuendelea kuwaachia mkuu wa mkoa na mkuu wa wilaya, mkuu wa mkoa na Rais wataiendesha nchi hii kama Tume ya Uchaguzi ya Zanzibar inavyoyachezea majimbo na kuwatekenya hapa na pale, wayatekenye huku huku watafanya hivyo.

Mimi nadhani katika hili, kipengele hiki lazima kifanyiwe marekebisho, kama ni lengo la mswada huu ni ku-*decentralize* demokrasi. Kama ni ku-*decentralize* demokrasi, basi lazima *decision makers* wawe katika *root* huko kwenye shehia ya wananchi na wananchi wanao wawakilishi wao japo sio wote, lakini wanao wawakilishi wao kupitia Mabaraza ya Miji na madiwani walioko katika Halmashauri ya Wilaya hata kupitia wawakilishi wetu katika Baraza la Wawakilishi ndio wao na *political mandate* ya ku-*decide* kwamba idadi ya shehia hizi hizi Unguja na Pemba ziongezwe zifanywe hivi, zifanywe hivi.

Baadae kugawa mipaka iachiwe ofisi inayohusika na Tawala za Mikoa watendaji wao wakagawe mipaka, lakini wakuu wa wilaya wasiende wakamshauri Rais na waziri wake, kuna siku wanaweza wakatoka chama kimoja

pamoja na mkuu wa mkoa, Rais na waziri wanaweza wakatoka katika chama kimoja wakazichezea shehia wanavyotaka wao kwa mujibu wa matakwa ya kisiasa, hili ni tatizo.

Hili ni tatizo na mimi kwa niaba ya wapiga kura makini, mahiri na walio na umakini mkubwa sana wa Jimbo la Wawi, kwa hili siliungi mkono hili.

Mhe. Naibu Spika, kama ni kuimarisha demokrasia sasa, basi nashauri kwamba ofisi inayohusika na mambo ya Tawala za Mikoa wao wakagawe mipaka tu, lakini *decision makers* katika idadi ya shehia, wadi iwe ni ya wawakilishi wa wananchi, aidha hili Baraza letu la Wawakilishi au huko kwenye Manispaa na maeneo mengine ya Halmashauri za Wilaya.

Mhe. Naibu Spika, sasa nije katika kifungu Nambari 8, kinazungumzia Uteuzi na Sifa za Sheha. Lengo ni ku-*strengthen Government powers*, sio ku-*minimize Government powers*. Leo huku sheria inakwambia kwamba kifungu Nambari 8 kuhusu Sifa za Sheha, kutakuwa na sheha ambaye atakuwa ni mtumishi wa umma aliyeteuliwa na mkuu wa mkoa kwa kushirikiana na mkuu wa wilaya husika na kuthibitishwa na waziri kwa ajili ya kutekeleza majukumu ya kazi zake. Sasa atakuwa ni mtumishi huyu wa umma, sasa leo unatwambia sheha atakuwa ni mtumishi wa umma, *okay*.

Ukienda katika sheria za utumishi wa umma viko vigezo, sifa na miongoni mwa sifa ni *academic performance* za watumishi wa umma ni pamoja na hali ya kielimu. Hivi sasa tuna tatizo Serikali zetu huko shehia zetu zina mashaka sana, sheha analojua ana koti lake na muhuri wake tu. Ukitaka kugongewa muhuri barua, hebu ile barua ya juzi nilitee, hajui hata tarehe ngapi imeandikwa, unaona, anatia mkono mfukoni yeye anatoa muhuri anagonga pale. Pengine ni barua tangu ya wiki na wala haikuhusiana na jambo lile.

Sasa mimi nadhani katika hawa kama ni watumishi wa umma basi wanapata malipo hawa kutoka pesa za walipa kodi wa nchi hii, wafuate vigezo vya utumishi wa umma ikiwa ni pamoja na elimu, kabisa kabisa tuachane na ule mfumo wa sasa wa kutembea na mkoba na muhuri tu, wanamtafuta katibu au amtafute Juma, hebu niletee ile barua yangu ya juzi, eti, aletewe barua ya juzi akija anaitizama pengine ni ya mwezi uliopita, hajui kusoma hata ile tarehe pale. Yeye ana muhuri wake mkobani anatoa na kugonga tu, mzee sio hii, hii ni ya Mwashamba binti Jape kumbe yeye ni Salim Juma yule. Hii haitoshi kabisa, hii haitoshi na ni mbaya sana na ndio hii inatupa tatizo.

Mhe. Naibu Spika, masheha wanakuwa jeuri,yaani sheha anaranda na muhuri tu anakwenda zake huko bandarini, watu huku wanatafuta samaki umuendee kule kule anakokwenda kununua samaki akakugongee barua.

Sasa kuna haja sasa ya ku-*strengthen supremacy* ya *Local Government* na hii *Central Government* kwa kuweka watu makini wenye taaluma angalau ya *Form IV* kabisa kabisa. Kama hawa ni viongozi wa kisiasa basi isemwe tu hatutong'ang'ania hapa, ikiwa ni viongozi wa kisiasa Mhe. waziri, mimi nitakuta hoja yangu hii, lakini kama ni watumishi wa umma lazima *academic performance* yao, *at least* iwe *Form IV level* na hii itasaidia kupunguza ukiritimba na mambo mengine zaidi na tutawapa nguvu hawa jamani, sio tu kwamba wao kazi yao ni kugonga muhuri, lakini na zile barua waweze kuandika.

Sheha anaandikiwa na katibu wake ndio akaweke muhuri ukimkutia hapo hajui kuandika hata ile barua, jamani hilo ni tatizo. Masheha kutoka Bogoa kule sehemu za Nanguji huku ndio kabisa hawajui kuandika hata barua! Wawekeeni hawa, hawa wawekeeni.

Mhe. Naibu Spika, wawekewe kabisa elimu ya *Form IV* kusudi waweze kuwa watumishi wa umma. Lakini kama ni *political leaders*, aa, mimi sisemi Mhe. waziri, aa, wabakie kama sisi Wawakilishi na Wabunge waweze kusoma na kuandika tu kama hivi sisi. Wao kama ni watumishi wa umma wafuate vigezo vya utumishi, lakini kama ni viongozi wa siasa kama sisi, aa, mwenzangu na wabakie tu hivi hivi ukishajua kusoma a, e, i, o, u, kama hivi mimi muachie awe sheha, lakini kama ni watumishi hawa tunawalipa pesa kutoka mifukoni mwetu, sio iwe kazi yao ni kugonga mihuri tu watutumikie kwa dhati.

Mhe. Naibu Spika, hilo sijui ni la kwanza *Yarabi toba* Mungu wangu! Lakini jengine kuna tatizo hapa, naangalia pale kwenye kifungu cha 8 kwamba kutakuwa na naibu sheha katika kila shehia ambaye atateuliwa na mkuu wa wilaya kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Ushauri la Sheha, baadae kupokea mapendekezo kutoka kwa Mjumbe wa Baraza Kuu la Shehia husika.

Sasa mkuu wa wilaya kapewa nguvu ya kumteuwa naibu sheha, lakini mkuu wa wilaya ikiwa sheha hayupo hawezi kumu-*uphill* naibu sheha kuwa kaimu sheha. Sasa hii una-*minimize*, kuna kitu kinaitwa *supremacy*, unampunguzia nguvu yule mkuu wa wilaya na lazima tukubali hawa masheha *every time* wanakuwa *very closed* na hawa ma-*DC* na sizaidi kuwa *closed* na mkuu wa mkoa, yaani wanakuwa *very closed* na ma-*DC* na wanafanya kazi pamoja sana na ma-*DC*. Sasa ikiwa yeye mkuu wa wilaya ana uwezo wa kumteuwa naibu sheha kwa nini asiwe na uwezo wa kumteua kaimu sheha, watakuwa hawawaheshimu hawa masheha, watakuwa hawawaheshimu vizuri wakuu wa wilaya kwa sababu watakuwa wanawajibika zaidi kwa mkuu wa mkoa tu kuliko kwa mkuu wa wilaya.

Mimi nadhani kwa hili la ukaimu sheha wapewe nguvu hawa wakuu wa wilaya kusudi na wao wapate angalau heshima kidogo kwa hawa masheha. Lakini mimi katika hili pamoja na ushauri huo nafuta hiki kipengele, kifutwe.

Mhe. Naibu Spika: Mheshimiwa, bado dakika tano.

Mhe. Saleh Nassor Juma: Nataka nizitumie vizuri sana hizo. Hiki kipengele naomba kifutwe cha uteuzi kuhusu kuteuliwa teuliwa tu masheha, ni *connective link* baina yao na wananchi mmoja mmoja huko na huo unyambi aliozungumza Mhe. Mohammed Mbwana Hamad, hapa asubuhi wa masheha unatokana na kiburi kwamba wao ni wateule na wana-*deal* zaidi na watu waliowateuwa na kuwaheshimu zaidi wakuu wa mikoa na wilaya na sio kuwaheshimu wananchi.

Hebu tuangalieni sisi hapa tulipo sasa hivi jinsi tulivyo na heshima kwa wananchi, sisi Wawakilishi na Wabunge pale tuna heshima kubwa kwa wananchi na tunawaogopa kwa sababu bado kidogo tu siku za kutuchapa, zishaanza kukaribia, yaani siku za kutuchapa tutakuwa na heshima kubwa, lakini masheha wanakuwa na kiburi chao.

Mimi nina sheha wangu, huyo kazi yake ni kuchomelea tu, mwembamba lakini kwa kuchomelea ni hatari, ukitaka kwenda kupata barua hakupi hata siku moja ya kugongea muhuri. Sasa huyu bwana sheha ambaye kazi yake ni kuchomelea tu angepunguza jeuri kama angechaguliwa na wananchi huyu, yaani nakuhakikishia angepunguza jeuri kama angechaguliwa na wananchi.*(Makofi)*

Sasa katika kutunza heshima na nidhamu na katika kuimarisha demokrasia na utawala bora ni aibu sana kuona kwamba masheha wanateuliwa hapa, wachaguliwe. Hebu tuangalieni, lazima uangalie katika maeneo ya nchi, ukitaka kuangalia utaratibu wa nchi angalia nchi nyengine twendezetu hapo Tanganyika tu kidogo, hebu angalia hapo Tanganyika zitume fikra zako, pale kuna watendaji wa vijiji na mitaa, hawa wote wanachaguliwa na wananchi ambao nafikiri Afisa Mtendaji wa Kijiji ni karibu na sheha kwa cheo huyu na anachaguliwa na wananchi na nidhamu waliyonayo hatari kubwa hasa.

Siku hizi nao wamechomoka kwa sababu uchaguzi wao ndio siku za karibu hao. Afisa Mtendaji wa vijiji Serikali za Mitaa huko Bara karibu wanafanya, basi nakwambia ukienda wewe humtafuti anakutafuta wewe Afisa Mtendaji wa kijiji, anakutafuta wewe. Leo sisi tunamtafuta sheha na anakukimbia kwa sababu hachaguliwi.

Mimi naomba kwamba ili kutunza nidhamu, ili kuimarisha utawala bora na demokrasia katika nchi, basi masheha ili wawe na adabu, wawe na nidhamu nzuri kama hivi, sisi basi naona wachaguliwe tu moja kwa moja katika shehia zao tena kupitia *secret ballot*, kupitia kura za siri kabisa.

Mhe. Naibu Spika, nimalizie kwamba katika kijifungu cha 18(e) kilichomtaka sheha apokee taarifa za mikutano, aah! Hii aibu. Sheria Nambari 5 ya mwaka 1992 imeiweka nchi katika *multiparty system*, *this is broaden and democracy*, unachotakiwa wewe uende tu kwa polisi pale ukawaambie una mkutano, waje wakulinde huku ukijitamba katika jukwaa, leo umpelekee na Unyeke sheha wangu, barua ataikimbia hiyo na milele sitafanyapo mkutano mimi pale, hilo nakwambia ulijue na ikiwa ataniruhusu nitafanya na ikiwa hakuniruhusu, mimi nitafanya zogo litaanza hapo na sheria hii itakuwa tatizo sasa.

Sasa ikiwa mnataka muulishe watu nyinyi Serikali nawaambia Mhe. waziri, ikiwa wanataka kuulisha watu basi na hiki kipengele kiachiwe hivi hivi na utakuja kuniuwa mimi, Vitongoji pale katika kijiji cha Umangani nikihutubia huku Unyeke hajatoa ruhusa ya kuhutubia. Kwa mnasaba huo, siungi mkono hoja hii mpaka yale mambo yote niliyoyasema yapigwe X, hivi yatolewe ndiyo nitaunga mkono. Ahsante sana Mhe. waziri na nasubiri majibu. *(Makofi)*

Mhe. Naibu Spika: Ahsante Mheshimiwa, sasa nilimruka mchangiaji mmoja yupo nampa Mhe. Abdalla Juma Abdalla, wale niliowataja wataanza jioni. Mhe. Marina Joel Thomas, Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi na Mhe. Salim Abdalla Hamad, mje mapema muanze jioni.

Mhe. Abdalla Juma Abdalla: Mhe. Naibu Spika, nakushukuru kunipatia nafasi hii na mimi bila ya kufanya dibaji refu kwa sababu muda wenyewe ni mfupi sana na nina mambo mengi ya kuzungumza, naomba nianze moja kwa moja na nitaanza kwa kifungu cha 4(1). Kifungu hiki kinasema kunaanzishwa au kwa marekebisho yaliyofanywa kunaanzishwa ofisi ya Tawala za Mikoa katika kila mkoa, wilaya, wilaya ndogo na shehia.

Sasa mimi hapa nina tatizo kidogo la lugha tu, kwa sababu ukisoma hii Sehemu ya Pili inasema; kuanzishwa kwa Ofisi za Utawala katika Ngazi za Mikoa, Wilaya na Shehia. Kwa hivyo, kunaanzishwa ofisi za utawala. Sasa kwenye kifungu kidogo cha (1) kinasema;

> "Kunaanzishwa ofisi za Tawala za Mikoa".

Nilikuwa naomba irekebishwe nazo ziwe vile vile kunaanzishwa ofisi za utawala katika kila mkoa, wilaya, wilaya ndogo na shehia; hapo itakuwa hiki kifungu kidogo cha (1) kinaoana na hii *heading* ya sasa juu.

Vile vile, katika kifungu kidogo cha (2), pia kuna maneno hayo yanajirudia Tawala za Mikoa naomba pia nayo iwe utawala ulivyotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1). Ukisoma kifungu kidogo cha (3) kinasema;

> "Ofisi za Tawala za Mikoa zitaongozwa na..."

Mimi naomba iwe hivi;

> "Ofisi za Utawala zilizotajwa chini ya kifungu kidogo cha (1) cha kifungu hiki, kitaongozwa na..."

Marekebisho ya hicho kifungu kidogo cha (3), nafikiri tukiweka hivyo ndio itakuwa inaleta *fence* hasa ya vile ilivyokusudiwa.

Mhe. Naibu Spika, nikiondoka hapo niende kwenye kifungu cha tano (5), kinasema;

> "Mkuu wa Mkoa na Wilaya kwa nafasi zao watakuwa watumishi wa umma watakaoteuliwa na Rais kwa mujibu wa masharti ya Katiba".

Ukisema tafsiri Rais hapa ni Rais wa Zanzibar na Katiba ni Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984. Nasema nafurahia sana hiki kifungu, Mhe. waziri, hiki kifungu usijekifuta hata siku moja.

Mhe. Naibu Spika, tukitoka hapo niende kwenye *sub-section (2)* ya kifungu cha tano. Pale pana sifa za mtu atakayekuwa mkuu wa mkoa imetajwa, awe Mzanzibari, awe Mtumishi Mwandamizi wa Umma, sijui ambayo kwenye Kamati ilifutwa ilikuwa inasema awe na uzeofu katika utawala wa umma kwa muda usiopungua miaka hiyo hapo.

Sasa hapa mimi kidogo nina tatizo na tatizo langu ni kwamba mkuu wa mkoa ni mtu mkubwa, ni mwakilishi wa Serikali katika mkoa mzima. Mkuu wa Mkoa anaongoza taasisi nyingi katika ule utaratibu wa ugatuzi wa madaraka mikoani, anaongoza taasisi nyingi sana za Serikali. Sasa hakuna sifa yoyote nyengine ya kielimu iliyowekwa hapa na hii ambayo angalau ina uzeofu imefutwa. Mkuu wa mkoa atapata wageni siku nyengine kutoka Uchina, Ujerumani, sijui kutoka wapi.Sasa hakuna sifa yoyote ya kielimu iliyowekwa hapa, matokeo yake tunaweza tukapata mkuu wa mkoa kwa mwanya huu tulioutoa atakaekuwa akipwaya sana katika hii ofisi anayoifanyia kazi.

Sasa mimi nilikuwa naomba sana na hasa kwa sababu sasa mkuu wa mkoa ni mtumishi wa umma, maana yake pale juzi mkuu wa mkoa alikuwa ni mwanasiasa hakuwekewa masharti haya, alikuwa akishajua kusoma na kuandika basi tunakuwa naye. Lakini sasa ni mtumishi wa umma na mtumishi wa umma katika ngazi kubwa kama hii, halafu usimuwekee sifa ya kielimu, nafikiri tutakuwa hiyo sisi hatujaitendea haki. Kwa hivyo, nilikuwa naomba sana

angalau awe na *degree* ya *human resource management*, kwa sababu anataka kuongoza watu tena taasisi pana kabisa. Nilikuwa naomba sana hilo tusiiache tu ovyo ovyo.

Mhe. Naibu Spika, nikitoka hapo sasa niende kifungu cha 8. Kifungu hiki kina uteuzi na sifa za sheha. Kwanza nimkumbushe Mhe. waziri na watendaji wake kwamba huu mswada mzima una watu watatu, mna mkuu wa mkoa, mkuu wa wilaya na masheha; watu watatu tu waliozungumzwa katika mswada huu. Sasa wote hao, zimeelezwa sifa na kazi za mkuu wa mkoa na mkuu wa wilaya, lakini sheha hakuna kazi za sheha katika mswada huu. Sasa mawili ama tufute hii *post* isiwepo au kama iwepo tufanye marekebisho makubwa ya kuweka kazi za masheha ziwepo hapa.

Mhe. Naibu Spika, mimi nakumbuka kidogo kule nyuma, nina miaka 50 na zaidi sasa hivi. Kule nyuma kulikuwa na masheha kabla ya hawa masheha ambao tumewaanzisha mwaka 1990, wale masheha na nimewahi kusema mara nyingi humu, masheha wale walikuwa wakitafutwa wenye sifa maalum katika jamii, sheha anakuwa mtu mzima mwenye umri, ule umri wake peke yake unamfanya aheshimiwe. Sheha alikuwa na taaluma angalau ya mambo ya dini pengine hata Msikitini walikuwa wakipenda sana kumuweka Imamu, ile sifa ya kuwa Imamu ni sifa nyengine ya kuheshimiwa katika jamii ya watu kama hao Wazanzibari. Sheha alikuwa ana kila sifa ya kuwa kiongozi wa jamii na kwa kweli watu wengi sana walikuwa wakimaliza shida zao na migogoro yao kwa masheha.

Sasa lakini bahati mbaya, tena mbaya sana, tulipokuja kurejesha tena mfumo wa masheha miaka ya 1990 hatukuzingatia hizo sifa, matokeo yake tumepata masheha ambao kwa uzoefu wa miaka hii michache tuliyokuwanayo wamesababisha matatizo mengi sana na ndiyo hayo ambayo mpaka leo tunaandaa hizi sheria za kurekebisha ili kuondoa changamoto kama hizo.

Mhe. Naibu Spika, kwanza masheha wetu hawa walikuwa ni masheha wanaoegemea upande mmoja wa kisiasa, halafu ni masheha ambao kwa kweli hawakuwa waadilifu au sio waadilifu maana yake mpaka leo tunao. Kwa sababu hiyo basi, mtu akishakuwa amekosa sifa ya uadilifu hata kama ni baba hawezi kuheshimiwa na watoto wake tena. Kwa hivyo, masheha wa sasa kama mtagundua nyinyi ni kwamba wamepoteza ile heshima yao kwa jamii, unamkuta mtu anaweza akamtolea maneno sheha anavyopenda mwenyewe siku nyengine anakaribia kumpiga kabisa mpaka inabidi sheha sasa awekewe ulinzi.

Sasa kutokana na changamoto hizi, mimi nilikuwa nadhani hizi sifa za kuwa mtu awe sheha tuziangalieni vizuri na sio kuziangalia tu, halafu tuwasimamie watekeleze hizi sifa. Kwa mfano Mzanzibari mimi sina tatizo nayo, mwenye kuheshimika, hili ni jambo muhimu sana, lazima upembuzi wa kumpata sheha.

Mhe. Mkuu wa Mkoa afanye *research*, ni mtu gani katika shehia hii anaheshimika, sio tunaweka mtu kwa maslahi yetu ni tatizo kubwa. Migogoro mingi imekuja kwa sababu ya masheha, awe mkaazi hili sina tatizo nalo, ndio muhimu hasa na hii sifa ya kuwa awe muadilifu hii ni sifa muhimu sana na huwezi kabisa kupata sheha muadilifu kama atakuwa anaegemea upande mmoja wa kisiasa.

Kwa hivyo, naomba kuwe na sifa nyengine hapa ya kusema sheha asiegemee wala asishabikie upande wowote wa kisiasa awe ni mtu *very neutral*, akishakuwa hivyo ataheshimika na sifa ya kielimu mimi nilikuwa nadhani kwa sababu ni mtumishi wa umma kama walivyosema wenzangu ni muhimu sheha awe na sifa ya kielimu na sio elimu ya dunia tu, mpaka elimu ya akhera awe nayo kidogo huyu, kwa sababu atasuluhisha migogoro na migogoro mingine inahusu ndoa za wanadini lazima awe na *ethics* ya dini ya kuweza kupembua pembua namna ya kusuluhisha.

Mhe. Naibu Spika, kuna kifungu cha 9, kinazungumzia kuondolewa sheha katika ofisi, bila shaka atakuwa na matatizo, matatizo yanayomfanya kuondolewa. Sasa mimi nina *objection* na siku zote nitaendelea nitakapoiona hii tu, kuipiga vita hii (d) kwamba amefanya kosa lolote la jinai na kuadhibiwa kifungo kisichopungua miezi sita.

Mhe. Naibu Spika, mimi nilikuwa nadhani sifa hii tuiondoeni katika kutunga sheria. Kwa sababu makosa ya jinai nayo pia yana mazingira yake, mara nyengine mtu anajishitukia tu yumo kwenye kosa la jinai, lakini hana tabia mbaya, ni bahati mbaya inatokea au kutokana na mazingira husika yanamfanya awe huko. Sasa nilikuwa naomba sana sifa hii iondolewe.

Mhe. Naibu Spika, kama ningekuwa na wakati ningekutolea mfano mimi mwenyewe, mimi si *corruptive* kabisa kabisa katika jamii, lakini yalinikuta haya na kasoro kidogo nifungwe kwa sababu maalum, sina wakati ningekuelezea.

Jambo jengine kifungu cha 11, kwanza kifungu cha 10 *sub-section two* pale kuna *repetition* ya maneno, naomba Mhe. waziri, ayaangalie katibu wa sheha imejirudia mara mbili. Halafu kifungu cha 11 kinasema; "Mtu atastahiki kuajiriwa kuwa katibu wa sheha, hili neno "atastahiki" nilikuwa naomba lisitumike, lina maana nyengine ambayo ni pana zaidi, bora tuseme atafaa kuajiriwa kuwa katibu wa sheha.

Mhe. Naibu Spika, nafikiri kwa sababu wakati haupo mimi naomba tena, nitaunga mkono itakapofanyiwa marekebisho ambayo nimejaribu kushauri Serikali ifanye. Ahsante.

Mhe. Naibu Spika: Ahsante sana Waheshimiwa Wajumbe, tunategemea kazi yetu hii tuimalize wakati wa jioni na wachangiaji wachache niliowataja kuna na wenzao wengine watatu wataendelea wakimaliza wale wataingia wengine. Sasa baada ya hayo niwashukuru na tujeni mapema jioni kwa sababu tunachelewa sana, ili tupate kumaliza kazi yetu. Naakhirisha kikao hadi saa 11:00 za jioni.

(Saa 7:00 mchana Kikao kiliakhirishwa hadi saa 11:00 jioni)

(Saa 11:00 jioni Baraza lilirudia)

(Majadiliano yanaendelea)

Mhe. Marina Joel Thomas: Ahsante Mhe. Mwenyekiti na mimi kunipa nafasi ya kuchangia Mswada wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tawala za Mikoa namba 1 ya mwaka 1998 na Kuanzisha Sheria Mpya ya Tawala za Mikoa ya Mwaka 2014.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza napenda kuipongeza Serikali kwa kuleta mswada huu mbele ya Baraza lako tukufu ili ujadiliwe na hatimae kupitishwa.

Pili, naomba nimpongeze waziri, wakuu wa mikoa, wakuu na wilaya na watendaji wote wa wizara hii kwa kazi kubwa wanayoifanya na kumpa mashirikiano Mhe. waziri ya kutelekeza majukumu yake ya kila siku. Mhe. Mwenyekiti, pia, nawapongeza masheha kwa kutekeleza majukumu yao ipasavyo.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda katika kifungu namba 7 kifungu kidogo (1) ambacho naomba nikinukuu niseme;

> "Kwa madhumuni ya ubora na ufanisi wa kutekeleza kazi za Serikali katika ngazi za shehia, waziri kwa kushauriana na mkuu wa mkoa anaweza kupendekeza kwa Rais kuanzishwa shehia na maeneo ya utawala chini ya ngazi ya shehia kama atakavyoona inafaa".

Mhe. Mwenyekiti, mimi nakubaliana na kifungu hiki na nasema hivi kwa sababu wakuu wa mikao ni Wawakilishi wakuu wa Serikali katika maeneo yao ya kazi. Kwa hiyo, Mhe. waziri, kushauriana na wakuu wa mikoa ni wajibu wake kwa sababu wote watendaji wakuu katika Serikali hii.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda tena katika kifungu hicho cha 7(3) ambacho kinasema; "Vigezo vya kuanzisha shehia". Mhe. Mwenyekiti, katika vigezo vya Kuanzisha shehia imesema itakuwa kama ifuatavyo;

> "Nitakwenda kwenye kipengele kidogo cha (d) ambacho kinasema mgao wa idadi ya watu. Suala la kukata mipaka kulingana na idadi ya watu".

Hapa nilikuwa naomba nitoe ushauri kwa Mhe. waziri, ushauri wa ugawaji wa mipaka kulingana na vigezo ambavyo vinahitajika kutokana na mahitaji na uwiano ambao Serikali itaona inafaa, hili ni wazo jema nakubaliana nalo kwa sababu kuna shehia nyengine ina watu wengi na shehia nyengine zina watu wachache.

Kwa hiyo, Serikali inagawa mipaka kutokana na uwiano, mahitaji na idadi ya watu ambao wanahitaji katika eneo lile na vigezo ambavyo viwekwa katika Serikali hii. Nitakwenda katika kifungu namba 8 kinahusu Uteuzi wa Sheha

kifungu namba 8 kinasema; "Mtu hatateuliwa kuwa sheha isipokuwa ni hiki kifungu kidogo cha 2, kuna makosa ya *spellings* hapa, ilikuwa inasema hatateuliwa. Kwa hiyo, hapa nilikuwa naomba irekebishwe isomeke;

> "Mtu atateuliwa kuwa sheha isipokuwa ni Mzanzibari mwenye kuheshimika, mkaazi wa shehia husika kwa muda usiopungua miaka 10 mpaka 15, mtu aliethibitika kwa uadilifu mwenye umri wa miaka 40 na zaidi na mwenye cheti cha kidato cha nne au zaidi".

Mhe. Mwenyekiti, hizi sifa za sheha ukiangalia zote hizi mwenye kuheshimika na mwenye uadilifu mzuri na hiki kidato cha nne. Lakini ukitoa hiki kidato cha nne, ukiangalia hii ya mwenye kuheshimika na uadilifu, hizi ni sifa za kiongozi. Ili kiongozi awe kiongozi mzuri, lazima awe muadilifu na lazima awe anaheshimika hata ukiwa na elimu ya kidato cha sita au Chuo Kikuu kama kiongozi, huna heshima kama kiongozi si muadilifu hata uongozi wako utakuwa si mzuri, utakuwa huongozi kwa vizuri.

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli elimu nayo ina-*matter* kwa sababu kutokana na sheria hii ina maana sheha atakuwa ni mtendaji tafauti na siku za nyuma.

Sasa nashauri aidha hiyo kidato cha nne ikiwezekana ibaki na kama mkiona bora itolewe kwa sababu haimfungi huyu sheha kuwa kutokuwa asiwe sheha ni wa kidato cha nne, lakini haya mambo mengine mazito ya kuwa na heshima na kuwa muadilifu, unaweza kuwa muadilifu, lakini ni *Form II* tu, lakini ukawa kiongozi mzuri kabisa na heshima mzuri tu, lakini si msomi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini hivi vyote vinaendana elimu nayo ina-*matter* kwa sababu sasa tunaingia kwenye mabadiliko ya huu mfumo wa Tawala za Mikoa kuwa ni *Form IV* pia inakuwa haimaanishi chochote kinacho-*matter*, ni uaminifu, uadilifu, Mzanzibari awe na miaka 40 au 45 na zaidi. Kwa hiyo, kiongozi bora awe ni kiongozi wenye heshima na mwenye uadilifu.

Mhe. Mwenyekiti, ukiangalia katika moja majukumu ya sheha kifungu cha 18(2) ambacho kinasema;

> "Kusuluhisha na kutatua migogoro yote ya jamii ya kifamilia na yanayojitokeza katika eneo husika kwa kuzingatia tamaduni, mila, desturi na busara za eneo husika".

Hii pia ukiangalia inaingia katika zile sifa za sheha, kazi yake hii ni kusuluhisha ina maana hapa ukiwa na elimu wa kidato cha nne anaweza kusuluhisha migogoro kwa sababu kusuluhisha migogoro ya kifamilia ambayo unajumuisha wananchi mbali mbali wenye silka, tabia na tamaduni mbali mbali, unatakiwa uwe na busara, unatakiwa uwe muangalifu, unatakiwa uwe na lugha na nzuri. Kwa hiyo, ikiwezekana hichi kidato cha nne kiendelee au kitolewe, haiwezi kupunguza kitu chochote.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda kifungu namba 18 kifungu kidogo cha 2 ambacho kinasema; Kila sheha atakuwa na dhamana katika eneo la mamlaka yake kufanya majukumu yafuatayo. Nitakwenda katika kipengele kidogo cha (e) kupokea taarifa za kufanyika mikutano ya hadhara kutoka mamlaka husika.

Mhe. Mwenyekiti, hili suala la kufanya mikutano katika shehia husika si jambo geni, liko zamani tu huwezi kufanya kitu chochote katika shehia bila ya sheha kuwa na taarifa yoyote, huwezi kuingia katika sehemu bila ya kutoa taarifa kwa sheha. Lakini kutokana na mtindo tu mtu anaingia sehemu hatoi taarifa kwa sheha akipata tatizo sasa ndio anarudi kwa sheha anamwambia mimi sheha niko hapa nimehamia muda mrefu naomba unielewe.

Kwa hiyo, jambo ambalo linafanyika katika shehia ni wajibu sheha apate taarifa, huwezi kufanya jambo ndani ya shehia bila ya sheha kuwa na taarifa yoyote kwa sababu yule ni kiongozi wa shehia, ni mlinzi wa amani katika shehia ile. Huwezi kuingia kwenye nyumba ya mtu usipige hodi, piga hodi ndio ukaribishwe.

Mhe. Mwenyekiti, katika suala hilo hilo nitaelezea kuhusu suala zima la Serikali imeamua kugatua madaraka kutoka Serikali Kuu hadi chini. Kwa hiyo, hapa nilikuwa namshauri Mhe. waziri, kuhusu hawa masheha ni viongozi wa Serikali katika ngazi ya shehia, hawa sasa ni watendaji na ukiangalia masheha hawana ofisi, yaani masheha ofisi zao ndani ya nyumba.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ninachoshauri namuomba Mhe. waziri, hawa masheha wapatiwe ofisi kwa sababu kazi wanazozifanya ni kuweka kumbukumbu mbali mbali za Serikali, kumbukumbu nyengine zinakuwa ni siri ya Serikali, lakini wakipata ofisi hizi kumbukumbu zitaweza kuhifadhika vizuri na hazitokuja kupata tatizo lolote.

Suala zima la vitendea kazi kwa masheha, madhali masheha sasa hivi watatakiwa wawe watendaji wanatakiwa wapatiwe vitendea kazi vilivyo bora, halafu pia mafunzo mbali mbali hata ndani na nje ya nchi ili wakapate kubadilishana mawazo na kuleta ufanisi katika kazi zao.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda kifungu cha 21(1) ambacho kinasema;

> "Kuanzishwa kwa Kamati za Maendeleo za Mikoa".

Mhe. Mwenyekiti, nakubaliana na kifungu hiki kuhusu Kamati za Maendeleo za Mikao, ziko siku nyingi. Lakini na miongoni mwa Wajumbe katika Kamati hii ni Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa Wawakilihi, meya, wakuu wa wilaya wenyewe, mkuu wa mkoa ambaye pia ni Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, moja ya majukumu ya Kamati hizi ni kusimamia utekelezaji wa Sera za Serikali na kuainisha matatizo na kuishauri Serikali njia nzuri ya kutatua matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, jengine kuzingatia mapendekezo kwa mamlaka ya Serikali katika mitaa, mipango na maendeleo ya kimikoa, nyengine kutoa ushauri kwa wadau ambao wanaguswa na mambo ya maendeleo kiuchumi katika mikoa na kuzingatia taarifa na kuishauri Serikali kuhusu miradi ya maendeleo ya Taifa, mipango, shughuli zinazotekelezwa na zinazohusiana na mikoa husika.

Mhe. Mwenyekiti, Kamati hizi ni nzuri na hapa nilikuwa niwaombe tu Wajumbe wa Baraza lako Tukufu hizi Kamati wazitumie ipasavyo, Kamati hizi zinakaa na kujadili mipango mbali mbali ya maendeleo kutoka ngazi ya chini hadi ngazi ya Taifa. Wanapanga ni miradi gani ambayo itatekelezwa kwa mwaka huu, halafu wanajadiliana kwa pamoja wanaweka mikakati.

Kwa hiyo, ninachopendekeza Wajumbe wa Baraza lako Tukufu, Wabunge watumie vizuri Kamati hizi za Maendeleo na wakitumia hivyo wataona manufaa yake hata zile changamoto zinakuja kujadiliwa hapa kwenye Baraza lako Tukufu na nyengine zinakuja kumalizia huko huko kwenye Kamati za Maendeleo wala hazina haja kuja hapa kwenye Baraza lako Tukufu yanajadiliwa huko huko yanamalizia huko huko, huku kunakuja yale mambo ambayo yameshinda kabisa, mambo mengi yanatatuka huko huko kwenye Kamati za Maendeleo za Mikoa.

Mhe. Mwenyekiti, nitakwenda kwenye kifungu cha 33, waziri anaweza kutunga Kanuni. Hapa nilikuwa namuomba Mhe. waziri, aharakishe kuhusu utungwaji wa Kanuni isikawie ili utekelezaji wa masharti ya sheria hii iweze kufanyakazi yake vizuri. Baada ya kusema hayo, naunga mkono mswada huu asilimia mia moja. Ahsante. (*Makofi*)

Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii na mimi kuchangia mswada huu kwa jioni hii.

Mhe. Mwenyekiti, naomba kuchangia Mswada huu wa Sheria ya Kufuta Sheria ya Tawala za Mikao namba 1 ya mwaka 1998 na kuanzishwa Sheria Mpya ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, kuanzishwa kwa sheria hii isiwe ndio sababu ya Serikali kukosa maadili yake kama inavyotarajiwa. Sheria hii inaletwa hapa ifuatwe maadili yake kwa mtu yoyote wa nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu namba 1, kinasema;

> "Kutakuwa na sheha ambaye atakuwa ni mtumishi wa umma atakaeteuliwa na mkuu wa mkoa kwa kushauriana na mkuu wa wilaya muhusika na kuthibitishwa na waziri kwa ajili ya kutekeleza majukumu na kazi zinazoainishwa sheria hii au sheria nyengine yoyote itakayotumika Zanzibar."

Mhe. Mwenyekiti, katika kifungu namba 2(d), naomba kifanyiwe marekebisho kinasema kwamba mtu aliethibitika kwa uadilifu. Hii tukisema mtu aliethibitika, ni kama wakati uliopita, lakini niseme kwamba na mtu anayethibitika kwa uadilifu. Naomba hapa tuangalie kwa sababu ukisema mtu aliethibitika itakuwa kama wakati wa nyuma uliokwisha pita, lakini mtu anaethibitika.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 13(1), naomba kunukuu;

> "Mkuu wa Mkoa anaweza kutoa amri ya kukamatwa mtu yoyote endapo ana sababu za kuamini kwamba;
>
> (a)Mtu huyo anaelekea kuvunja amani au kuchafua utulivu wa wananchi;
>
> (b)Mtu huyo amefanya kitendo chochote ambacho kinaweza kupelekea uvunjifu wa amani au kuchafua utulivu wa wananchi; na
>
> (c)Uvunjifu huo hauwezi kuzuiliwa kwa njia yoyote isipokuwa kumuweka mtu huyo kizuizini".

Mhe. Mwenyekiti, niseme kwamba hivi sasa tumekabiliwa na mshauri mkuu wa 2015 isijekuwa hii sheria ambayo inatafuta sababu za kuwakamata watu na kuwaweka ndani. Niombe sheria hii itumike kama ipasavyo kwa sababu kuna sheria nyingi tunazitunga hapa na baadae zinakiuka maadili yake. Niombe hii sheria wakati huu tunaelekea katika Uchaguzi Mkuu, isijekuwa mtu yoyote yule anafanya kazi zake akaja kuambiwa mtu huyu ana hatia, mtu yule akakamatwa akatiwa ndani akawekwa kizuizini na hatimae mtu yule akakosa haki zake.

Mhe. Mwenyekiti, naomba hili liweke, la ikiwa si hivyo, ikiwa sheria hii haikufuata hivyo inavyotakikana baadae nitakuja kuleta vurugu. Naomba iangaliwe sana hii, kwa sababu ni wakati wa uchaguzi na kampeni, mtu anafanya kampeni zake isijekuwa kafanya neno dogo tu ikawa ndio sababu ya kuwekwa ndani, naomba hichi kieleweke, la ikiwa si hivyo, sheria hii itakuja kuleta vurugu katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kufungu cha 14, ukurasa wa 207 kinachosema kwamba;

> "Mkuu wa Wilaya atakuwa Mwakilishi Mkuu wa Serikali ndani ya eneo na mamlaka yake na atakuwa na kazi zifuatazo".

Mhe. Mwenyekiti, mimi si mwanasheria, lakini nasema katika kifungu kiliposema kwamba; "Mkuu wa Wilaya atakuwa Mwakilishi". Naomba kifungu hiki kisomeke; "Mkuu wa wilaya atakuwa muhusika Mkuu wa Serikali ndani ya eneo la mamlaka yake na atakuwa na kazi zifuatazo".

Mhe. Mwenyekiti, nije katika kifungu cha 19 kuhusu Mamlaka ya Sheha. Kila sheha katika utekelezaji wa majukumu na kazi zake nchini na masharti ya sheria hii, anaweza kumtaka mtu yeyote kuhudhuria kwa hiari yake au atatoa hati ya wito kwa mtu yeyote ambaye hatohudhuria kwa hiari yake kwa sheha na kumtaka ahudhurie au kutoa taarifa.

Mhe. Mwenyekiti, naomba vile vile narudia bado ninasema kwamba sheria hii anaweza kumtaka mtu, naomba hapa kidogo ningeomba kwamba anaweza kuamua kwa mtu yeyote kuhudhuria kwa hiyari yake au atatoa hati ya wito kwa mtu yeyote ambaye hakuhudhuria kwa hiyari kwa Sheha kumtaka ahudhurie au kutoa. Mhe. Mwenyekiti, naomba kisomeke kwamba kuamua kwa mtu na sio kumtaka mtu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nije katika kifungu cha 3 hiyo hiyo 19 kinachosema kwamba mtu yeyote ambaye alitakiwa na hati ya wito, alitakiwa naomba hapa Mhe. Mwenyekiti, isomeke, "Mtu yeyote ambaye amepata hati ya wito ya kuhudhuria kwa Sheha kwa hiyari yake bila ya sababu ya kisheria hakudhuria atakuwa ametenda kosa na atakapotiwa", naomba na hapa ibadilishwe, "na atakapoingia hatiani atakuwa amewajibika kulipa faini isiyozidi shilingi elfu arobaini au kifungo cha siku kumi na tano au vyote kwa pamoja". Naomba Mhe. Mwenyekiti, hapa pafanyiwe marekebisho.

Mhe. Mwenyekiti, nikija katika kifungu cha 30 niseme kwamba tuje ukurasa wa 214. Mhe. Mwenyekiti, Kamati za Maendeleo za Mkoa zitakutana mara mbili kwa mwaka. Naomba Mhe.Mwenyekiti, tuachane na mara mbili, mara

mbili ishakuwa mno. Naomba Mhe. Mwenyekiti, hii itakutana mara tatu kwa mwaka. Hili naliomba Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Mwenyekiti, baaada ya hapo niseme kwamba la mwisho nawaomba Masheha wote kufuata maadili ambayo yataiweka Serikali yetu ya Umoja wa Kitaifa pahala ambapo panaondosha chuki, ubinafsi na udhalilishaji wa raia wake na pia ninaitakiwa mema sheria hii pale ambapo itakuwa inafuata maadili ya wananchi wake katika nchi hii.

Mhe. Mwenyekiti, ahsante ninakushukuru. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Mwanajuma Faki Mdachi. Mhe. Amina Mbarouk Iddi na baada ya hapo atakuwa ni Mhe. Salim Abdalla Hamad.

Mhe. Amina Mbarouk Iddi: Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana, awali ya yote nichukue nafasi hii kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye ametujaalia jioni hii ya leo kuwa wazima wa afya. Lakini pia nichukue nafasi hii adhimu kukupongeza wewe Mhe. Mwenyekiti wa Baraza jioni hii ya leo kuwa Mwenyekiti wa kikao hichi.

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nichukue nafasi hii adhimu kumpongeza sana Mhe. Waziri kwa uwasilishaji wake mzuri wa Mswada huu ambao unahusiana na kufuta Sheria ya Tawala za Mikoa Nam. 1 ya 1998 ya kuanzisha upya sheria ya Tawala za Mikoa ya 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Mhe. Mwenyekiti, lakini pia nichukue fursa hii kuwapongeza kwa dhati kabisa Kamati ya Katiba na Sheria kwa kazi nzuri ambayo wameifanya kwa marekebisho mengi waliyofanya na hatimaye kwa kweli wameturahisishia kazi sisi Waheshimiwa Wajumbe katika kuchangia Mswada huu. Ninawapongeza sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, lakini pia niwapongeze watendaji wa afisi hii kwa kumsaidia Waziri kwa sababu ninaamini kwamba kama sio kazi nzuri ya watendaji hawa kwa kweli tusingeweza kupata Mswada huu leo na hatimaye kuweza kuupitia. Mhe. Mwenyekiti, baada ya utangulizi basi naomba sasa niingie katika Mswada wenyewe, ninaamini Mswada mzuri wenzetu wamefanya kazi nzuri lakini basi ni vizuri na sisi tuweze kutoa yale ambayo tunayaona. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nikiingia katika ukurasa wa 203 wa Mswada huu unaosema kwamba mtu ambaye anastahiki kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, ametuonesha hapa Mhe. Waziri sifa ambazo zinatakiwa Mkuu wa Mkoa anastahili awe nazo au Mkuu wa Wilaya. Mhe. Mwenyekiti, hii sifa ya kwanza sina tatizo nalo kwamba mtu anastahiki kuteuliwa awe Mzanzibari, ni vizuri sana lakini (b) inasema, "Mtumishi Mwandamizi wa umma". Mhe.Mwenyekiti, Mtumishi Mwandamizi wa umma hili mimi sikubaliani nalo, kwa sababu maana ya Mtumishi Mwandamizi wa umma ni mtu ambaye yupo kazini, mtu ambaye ni mfanyakazi wa Serikali.

Sasa hapa inaonekana kwamba kwa mujibu wa Mswada kuwa mtu akiwa sio mtumishi mwandamizi wa umma hastahiki kuteuliwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa. Mhe. Mwenyekiti, tunaamini kwamba tuna watu wengi ambao wanastahiki kuwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya. Kwa mfano, tuna mabalozi mbali mbali ambao wametumikia katika nchi mbali mbali lakini wamestaafu, sasa kweli Mhe. Mwenyekiti, mtu kama huyu hastahiki kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya. Lakini sio hilo tu Mhe. Mwenyekiti, tuna majeshi wamefikia ngazi mbali mbali, makanali lakini pia kuna Wakuu wa Polisi wamefikia ngazi mbali mbali za Kipolisi za juu kabisa, lakini Mhe. Mwenyekiti, kama haitoshi tuna walimu pengine mtu amefikia mpaka Mwalimu Mkuu wa Skuli pengine Skuli ya Sekondari, Vyuo Vikuu. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa mujibu wa Mswada huu hawa watu wote niliowataja hawastahili kuteuliwa kuwa Mkuu wa Wilaya au Mkuu wa Mkoa. Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa mtizamo wangu hichi kipengele sikiwafiki. Mhe. Mwenyekiti, naomba kipengele hichi kiondoke na badala yake basi iwe mtu mwenye uzoefu wa uongozi. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na Mswada huu nije katika ukurasa wa 204, sifa ambazo anastahili kuteuliwa Sheha, zimeoneshwa hapa nyingi hapa sina tatizo nazo. Lakini kuna kipengele hichi cha (f) kinasema kwamba mwenye cheti cha kidato cha nne au zaidi ndiye anayestahili kuwa Sheha. Mhe. Mwenyekiti, pia mimi kipengele hichi sikiwafiki kwa sababu mimi ninaamini kwamba Sheha ni mtu ambaye anahudumia wananchi. Kwa hivyo tumamuhitaji Sheha ambaye awe na busara, awe na hekma, sio lazima kuwa Sheha awe kafika kidato cha nne. Kwa hivyo mimi naomba kuwepo kwamba Sheha awe anajua na kuandika, hususan Mhe. Mwenyekiti, kwamba Sheha sio mtendaji mkuu. Sheha yeye ana wasaidizi wake ambao wanamsaidia kazi. Kwa hivyo tunaamini kwamba tunahitaji

Sheha ambaye mvumilivu katika kazi zake kwa sababu tunatambua kwamba katika kazi za Sheha zina mambo mengi, unaweza mtu kamka vibaya tu akenda Sheha akamtukana bure bure! *(Makofi).*

Sasa Mhe. Mwenyekiti, kazi hii ya Sheha tunahitaji Sheha ambaye ni mvumilivu, Sheha mwenye busara lakini Sheha awe mtu mzima ambaye anaheshimika na watu. Lakini sio hilo tu Mhe. Mwenyekiti, awe Sheha ambaye anaweza akatatua migogoro ya watu lakini kwa ule umri wake wa Sheha akaheshimika na mtu pengine kenda na jazba pale, lakini kutokana na umri wake mtu akasema ninamsikiliza ninakupa wewe tu heshima Sheha kwa nasaha zake.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije katika sifa za Katibu wa Sheha. Mhe. Mwenyekiti, haya mengine mimi sina matatizo nayo lakini kuna kipengele hichi cha (d), kinasema kwamba mwenye cheti cha ngazi ya kidato cha sita au zaidi. Mhe. Mwenyekiti, sote tunafahamu kwamba vijana wetu au watu ambao wamemaliza kidato cha sita, wengi wao wamekimbilia katika kazi nyengine mjini na sehemu nyengine. Lakini Mhe. Mwenyekiti, sio hilo tu tunaamini kwamba mazingira yetu sote tunafahamu. Kwa mfano mazingira ya vijijini au mazingira ya maeneo mengine, unaweza ukakuta pengine huyo mtu wa kidato cha sita hayupo na hayupo pengine wapo masomoni, wapo pengine sehemu nyengine za kazi. Mhe. Mwenyekiti, sasa mimi ninamuomba Mhe. Waziri hichi kipengele cha kidato cha sita tukiondoshe na ninaamini kwamba Katibu wa Sheha anatosha kuwa na kuwa na kidato cha nne.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu nije katika kazi za Katibu Tawala wa Mkoa. Katika ukurasa wa 208 kuna kipengele cha 2 kinasema kwamba Katibu wa Wilaya atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Ulinzi ya Wilaya. Mimi ninapongeza kuwa Katibu wa Wilaya awe Katibu wa Kamati ya Ulinzi ya Wilaya, lakini Mhe. Mwenyekiti, nilivyokuwa ninapitia Mswada huu sijaona katika kazi, nimeona tu kama kutakuwa na kazi za maendeleo za Wilaya na Mkoa. Lakini hii kazi ya Kamati ya Ulinzi na Usalama wa Wilaya au Mkoa ninaona hajatuonesha hakioneshi katika Mswada huu na ninaamini kwamba sasa hivi tunatengeneza sheria ya Tawala hizi za Mikoa katika Wilaya na Mikoa. Lakini sio hilo tu Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyozungumza kwamba huyu Katibu wa Kamati imeonesha lakini Mwenyekiti wa Kamati katika Mswada huu hauoneshi kwamba Mwenyekiti wa Kamati atakuwa nani. Ninavyofahamu mimi kwamba uzoefu unaonesha kuwa kama sikosei kwamba hizi Kamati za Ulinzi na Usalama sasa hivi zipo katika ngazi ya Wilaya na ngazi ya Mkoa. Lakini na Mwenyekiti wake kwa ngazi ya Wilaya anakuwa ni Mkuu wa Wilaya, lakini na Mwenyekiti wake wa ngazi ya Mkoa anakuwa ni Mkuu wa Mkoa.

Sasa ndani ya Mswada huu hatuoni. Mhe. Mwenyekiti, ninamuomba Mhe. Waziri atufahamishe tuelewe kwamba sasa katika maelezo yake ametwambia hapa kwamba Katibu wa Wilaya atakuwa ni Katibu wa Kamati ya Ulinzi na Usalama ya Wilaya, lakini Mwenyekiti hajatwambia hapa atakuwa nani. Je, Mhe. Mwenyekiti, inabidi sasa hivi Mkuu wa Wilaya atakuwa anaingia tu kama mtu wa kawaida au haingii kabisa na hivyo hivyo katika ngazi ya Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, nije katika ukurasa huu huu wa 208 kwenye kipengele cha 15 kinachosema kuwa mtu anayestahili kuteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa awe ni Mzanzibari, awe mtumishi wa umma, lakini pia awe angalau ana shahada ya uzamili au inayofanana nayo. Mhe. Mwenyekiti, mimi nirudie kusema kwamba hizi ngazi zote ambazo zimeainishwa humu nyingi zina-*deal* na watu. Kwa hivyo ni vyema basi ni bora kuonesha kwamba mtu awe na uzoefu wa kazi hizi kuliko kusema kwamba awe angalau ana shahada ya uzamili. Mimi ninadhani Mhe. Mwenyekiti, hapa diploma inafaa, tusiende kwenye mashahada kwa sababu mtu anaweza kuwa na shahada ya uzamili lakini kuna mambo mengine ambayo yanastahiki katika ngazi hii ambayo anastahiki katika kazi hizi hana. Kwa mfano, pengine mtu ana sifa hizi lakini hana uzoefu, ataongoza vipi hapa na hapa anaongoza jamii, anaongoza watu na sote tunafahamu watu wapo wa aina tofauti, watu wapo wana akili tofauti. Kwa hivyo ni vizuri Mhe. Mwenyekiti, katika kipengele hichi kiwepo kwamba mtu awe na diploma inatosha. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema kwamba kamati yetu hii imefanya kazi nzuri ya kufanya marekebisho. Kwa hivyo mchango wangu hautokuwa mkubwa sana. Namuomba Mhe. Waziri mchango wangu wote nilioutoa na pale ambapo ninataka ufafanuzi anijibu nimfahamu, baada ya hapo basi nitauunga mkono Mswada huu asilimia mia juu ya mia.

Mhe. Mwenyekiti, ninashukuru sana. *(Makofi).*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Amina Iddi Mbarouk, anayefuata ni Mhe. Salim Abdalla Hamad na baada ya hapo atafuata Mhe. Salma Mohammed Ali.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, na mimi ninashukuru kwa kunipata nafasi hii ya kuchangia ya Mswada wa Sheria ya kufuta ya Sheria ya Tawala za Mikoa Nam. 1 ya 1998 na kuanzisha upya Sheria ya Utawala za Mikoa ya 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, katika kuanza michango yangu, mimi leo sana nitataka ufafanuzi tu pamoja na maelezo machache. Kwa hivyo moja kwa moja nianze na kifungu cha 4 (1) sehemu ya pili ukurasa wa 203. Katika kifungu hichi imeelezwa kuwa kunaanzishwa afisi za Tawala za Mikoa katika kila Mkoa, Wilaya, Wilaya ndogo na Shehia kwa lengo la kutekeleza majukumu na kazi za Serikali Kuu.

Sasa hapa kutaanzishwa Afisi za Tawala za Mikoa katika kila Mkoa, Wilaya, Wilaya ndogo na Shehia. Naomba maelezo kuwa ndio katika kila eneo kutakuwa na afisi ya Tawala ya Mkoa au pengine ni lugha tu imenicheza. Naomba nipate maelekezo.

Halafu jengine Mhe. Mwenyekiti, ni kifungu cha 5 (1) (c) kwa mujibu wa marekebisho kutoka kwenye Kamati, haya maelezo ana uzoefu katika utawala wa umma kwa muda usiopungua miaka kumi na tatu kwa Mkuu wa Mkoa na miaka kumi kwa Mkuu wa Wilaya, imeelezwa kuwa kifutwe. Na kimefutwa wala hapakuwekwa maelezo mengine. Kwa hivyo naomba kujua kwa nini kifungu hichi kimefutwa na wakati uzoefu ijapokuwa muda ni mrefu ni kitu muhimu sana. Kifungu cha 6 (1) ukurasa huu huu wa 203, kinaeleza kuwa endapo Mkuu wa Mkoa au Wilaya ameshindwa kutekeleza majukumu yake kwa muda kutokana na sababu na kuendelea, huu muda ni muda gani ambao kutasababisha kuwe na mabadiliko. Kwa sababu wamesema muda tu haikuelezwa ni muda gani.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea twende kifungu cha 8 (1) ambacho hichi kinahusiana na uteuzi wa Masheha. Kwanza kwa mujibu wa maelezo ni kuwa kutakuwa na Sheha ambaye atakuwa ni mtumishi wa umma atakayeteuliwa na Mkuu wa Mkoa kwa kushauriana na Mkuu wa Wilaya husika na kuthibitishwa na Waziri kwa ajili ya kuendeleza majukumu ya kazi zilizoanzishwa na sheria hii au sheria nyengine ambayo inatumika Zanzibar.

Mhe. Mwenyekiti, hapa kidogo naomba kutoa maelezo. Mhe. Mwenyekiti, kwanza niipongeze serikali kwa kuteuwa Masheha na niipongeze sana kwa kazi za Masheha wanazofanya, mambo ambayo ni ya kuvunja amani, mambo ambayo yanakwenda kinyume na haki za binadamu. Masheha ni watu wakubwa sana wana eneo dogo la utawala, mkubwa wake ni Mkuu wa Wilaya wajuu zaidi Mkuu wa Mkoa na wa mwanzo ni Rais mwenyewe, huu ni mrengo wa utawala.

Sheha ndiye mwenye jamii, yaani watu wote wanaoishi katika eneo lake na watu wanakuwa na shida mbali mbali na Sheha, ni uzoefu wa muda mrefu kwa nchi hii pamoja na kuwa inaitwa ni nchi ya mani, lakini mimi nasema ni wananchi tu waliokuwa na amani. Tumekuwa tukipata kila aina ya ukandamizaji kutoka kwa Masheha.

Hata juzi, Mhe. Mwenyekiti, nilifanya ziara katika jimbo langu na matatizo niliyoyakuta ni kuwa kuna Wazanzibari ambao wana vyeti vya kuzaliwa vilivyo sahihi kabisa na wakati sote tunaelewa kuwa kama sio Disemba pengine Januari daftari la kudumu la wapiga kura litapita kwa mara ya mwisho. Kwa hivyo, watu wanakwenda kwa Sheha kuomba fomu ili wakapigishwe picha wapate vitambulisho vya Mzanzibari, na daftari litakapokuja waweze kujiorodhesha na wao wawe na haki ya kupiga kura kama Katiba ya nchi inavyoeleza.

Kwa bahati mbaya Masheha wengine wanasema hatuna fomu, lakini nilipouliza kwa wakuu wao walinieleza kuwa Sheha anapewa fomu moja, kwa sababu anakusanya pesa anatakiwa atengeneze fomu hizo kwa kufanya *copy* mwenyewe na hakuna fomu wala hatoi. Kuna wengine wanasema mitambo imeharibika.

Mimi sikufichi Mhe. Mwenyekiti, nimekuja katika Baraza hili kwa unyonge, kwa sababu sikuwahi kupata muda wa kutumikia wananchi wangu kutokana na tatizo hili kubwa, na sio mara hii tu ndio siku zote Masheha wetu wanavyofanya. Kwa hivyo, tunasema labda wameongozwa kufanya hivyo na kufanya hivyo serikali imefanikiwa vizuri. Lakini kama serikali iliwachagua Masheha kwa nia safi, kwa kuendeleza kazi zao ipasavyo, basi Masheha ndio wanaochafua katika nchi hii.

Mhe. Waziri akitaka ushahidi twende Pemba, nikifika tu nitampa orodha ya vyeti vya kuzaliwa ambavyo wazee wamekwenda, watoto wamekwenda wenye umri wa zaidi ya miaka 18 kutaka fomu kwa Sheha na wamekataliwa na mpaka hivi sasa hawajapata bado, niliwauliza kabla ya kuja humu. Sasa Masheha hawa kuendelea kuchaguliwa katika mtindo huu na kwa madaraka ya juu zaidi, ni kuhakikisha kuwa huko tunakokwenda sio kuzuri na amani haitavunjwa na wananchi, amani itavunjwa na serikali yenyewe kwa sababu ndio wenye Masheha wao wanaofanya wanavyotaka.

Kwa sababu hii, nakuomba Mhe. Mwenyekiti, ile sheria ya vitambuliso ambayo ina sehemu inaeleza kuwa Mkurugenzi wa vitambulisho atafanyakazi kutokana na maelekezo ya Mhe. Waziri husika, ile sheria ifanyiwe marekebisho ili huku tunakokwenda tuende kwenye usalama zaidi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, tumeambiwa kuwa Sheha hatateuliwa kuwa Sheha isipokuwa awe Mzanzibari, sio sababu ya kutokujua lakini ni kwa sababu ya kutaka maelezo, kutokana na kuwa nchi hii sasa imeingiliwa kiasi ambacho hata mtu anayekuja muda mchache hapa kutoka nje ya Zanzibar, anapewa kitambulisho cha Uzanzibari. Kwa hivyo, hebu tuambieni Mzanzibari hasa ni nani, kwa sababu hatutambuani.

Mhe. Mwenyekiti, sisi tunajua tu huwezi kuwa Mzanzibari kama sio Mtanzania, na Mzanzibari ni Mtanzania yeyote anayeishi Zanzibar baada ya kukamilisha masharti, lakini sasa hivi hayo hayapo. Hili Mhe. Mwenyekiti, nimefanya utafiti na Mhe. Waziri akitaka nitampa majina ya watu waliokuja hapa kabla ya kutimia huo muda unaotakiwa na wamepwa vitambulisho.

Mhe. Mwenyekiti, sasa ikiwa kila mtu tu anapewa vitambulisho vya Uzanzibari maana yake ndio wenye Zanzibari. Huyu Mzanzibari anayekusudiwa ni yupi, kwa sababu sasa hatujuani tena kutokana na mkorogano huu.

Halafu Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 8(1)(c) kinaeleza kuwa mkaazi wa Shehia husika kwa muda usiopungua miaka 15, yaani mtu hawezi kuwa Sheha mpaka awe ni mkaazi wa Shehia hiyo kwa muda usiopungua miaka 15. Kama sheria haijabadilishwa tunajua mtu yeyote aliyetoka Tanzania Bara akifika hapa miaka 10 mfululizo bila ya kuondoka atakuwa ni Mzanzibari. Hii ni *long time process*, naamini kuwa ninavyoona mimi mwenyewe itafika wakati hata huo Usheha wale Wazanzibari asilia wasiuguse tena hapa. Hivi sasa tuko sijui nusu kwa nusu ni asilimia ngapi lakini itakwenda hivyo, ikienda hivyo mila, desturi, silka, utamaduni na mengine mengineyo yanayohusiana na hayo yataondoka. Kwa hivyo, Zanzibar itakuwa *bye-bye*.

Kwa hivyo, moja kwa moja ninaloomba kifungu hiki cha miaka 15 kiondoke apewe Sheha Mzanzibari aliyezaliwa hapa, akakulia hapa akawa na tabia njema na mambo mengine kama hayo, sio kila mtu akishakaa kwa miaka 15 apewe Usheha, tusichezeane kiutawala kiasi hicho. Sisi tuna nchi yetu ni lazima tuienzi na ni lazima tuidumishe katika uendelevu wa sheria na kadhalika, tusifanye mambo ya kiujanja ujanja. Hiki kifungu kiondoke vyenginevyo mimi mswada huu wote siuungi mkono, kwa sababu naujua ni mswada kandamizi.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako, ili kazi iende vizuri, kazi inakwenda na taaluma. Hakuna nchi inayokwenda kwa kuwapa vyeo wajinga. Natoa mfano sio mzuri lakini naomba radhi. Hata Firauna asingekuwa mtawala kwa miaka mingi, lakini wale watendaji wake walikuwa ni watu wenye nguvu, wajinga waliokuwa hawakusoma. Ukisema Firauna sio Mungu basi unakwenda na maji, kwa sababu ya ujinga wao.

Leo kwa makusudi ili Sheha afanye kazi yake na sisi tufaidike nchi hii iendelee, imeambiwa hapa kuwa Sheha awe mwenye cheti cha Kidato cha Nne au zaidi. Mtu kuwa na taaluma ni kitu muhimu sana, tunawasomesha watu wetu halafu leo tunarudi kule kule ajuwe kusoma na kuandika. Sijui kuwa ni Kiarabu, Kichina nakadhalika hiyo lugha haikutiwa. *(Kicheko)*

Mnaturudisha nyuma, kunawekwa kitu kizuri tunakiondoa tunakiweka kibaya. Mtu yeyote ambaye hakusoma nakuhakikishieni hawezi kufanya kazi zake ipasavyo, kwa sababu afanyekazi katika mambo ambayo anayafanyia kazi. Kwa hivyo, hii taaluma mimi naona ni muhimu, watu wameshasomeshwa miaka 50 na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, watu wengi wamesoma, wana uwezo irejeshwe. Sio wakati wa kumuweka mtu anayejua kusoma na kuandika kwa sekta kama hii ya kiutendaji. Jamani tuangalie umuhimu, Sheha ni mtu akae aweze kufanya jambo kwa kujua anafanya nini, sio kwa kufanyiwa, halafu tena tukaharibikiwa.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako kifungu cha 11, naomba kunukuu;

Kifungu cha 11

"Mtu atastahiki kuajiriwa kuwa Katibu wa Shehia ikiwa ni Mzanzibari, mtu anayeheshimika, mtu mwenye tabia njema na mwenye cheti cha ngazi ya Kidato cha Sita au zaidi"

Hii hapa nayo tunaambiwa ifutwe, hapana. Halafu tunaambiwa tuongeze "au mwenye elimu nyengine inayolingana na hiyo". Hapa imeshaelezwa mwenye elimu ya Kidato cha Sita au zaidi, imekusanya mchanganyiko wa elimu zote, au mwenye elimu nyengine inayolingana na hiyo, ni elimu gani hiyo inayolingana na Kidato cha Sita na zaidi, naomba nielezwe.

Mhe. Mwenyekiti, kifungu cha 13(1) kinaeleza kuwa bila ya kuathiri sheria nyengine za nchi, Mkuu wa Mkoa anaweza kutoa amri ya kukamatwa mtu yeyote, endapo ana sababu za kuamini kwamba mtu huyo anaelekea kuvunja amani, na kuchafua utulivu wa wananchi au mtu huyo amefanya kitendo chochote ambacho kinaweza kupelekea uvunjifu wa amani, au kuchafua utulivu wa wananchi na kwamba utulivu huo hauwezi kuzuiliwa kwa njia yoyote, isipokuwa kumweka mtu huyo kizuizini.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwanza nashangaa kuwa Mwenyekiti wa Kamati husika wa mswada huu ni Mwanasheria, ambaye kule Dodoma alifanya kazi kubwa sana. Leo hapa Zanzibar anaipitisha kuwa Mkuu wa Mkoa anaweza kutoa amri ya kukamatwa mtu yeyote. Tukisema mtu yeyote humu anaingia mpaka Rais, maana yake anaweza mpaka Rais akatolewa amri na Mkuu wa Mkoa akakamatwa. Mtu yeyote ni yeyote tu.

Kwa hivyo, ninaloomba jamani tunapotunga sheria, tusiwe tunaangalia upande mmoja tukasema yeyote kwa hivyo tunavyokusudia. Hiki kitu ni kikubwa sana yeyote inaingia kila upande. Kwa hivyo, naomba kifungu hiki kwa wanasheria kikae vizuri.

Vile vile hata sisi wawakilishi tuna sheria zetu, hawezi mtu akakamatwa akatiwa ndani bila ya Spika, kutoa amri. Leo inakuwa Mkuu wa Mkoa ana mamlaka hata Spika, mwenyewe mlolongo mzima hapa wa serikali, Bunge la Kutunga Sheria. Sasa kinachonipelekea mimi katika fikra zangu na ikiwa sivyo naomba radhi, naomba nifahamishwe vyengine.

Mhe. Mwenyekiti, tunajua tunaelekewa na uchaguzi mkuu, tunaelekewa na kura ya maoni kuhusu Katiba mpya iliyopendekezwa. Kwa hivyo, tutakuwa kwenye majukwaa na lugha zetu itakuwa hazilingani. Pengine huyu anasema *yes*, na huyu anasema *no*. Lakini Mkuu wa Mkoa tunajua ni mtu wa serikali, kichama na kadhalika na huko kuna mambo, utaona usoni kuwa atafanyakazi atakazopewa amri ambazo zitataka ufafanuzi.

Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, kifungu hiki ni cha kuhatarisha amani. Nchi hii ina watu wanaohusika na ukamataji, tunao maaskari na kadhalika. Kuna askari wa aina kwa aina na mtu hawezi kukamatwa tu kwa sababu Mkuu wa Mkoa anadhana, mtu anakamatwa kwa kuonekana kuwa kweli ana makosa baada ya kufanyiwa utafiti wa kina.

Halafu huku mwisho inaeleza kuwa mtu huyo atapelekwa Mahakamani au atatolewa haraka haraka, kwa nini iwe hivyo. Kwa hivyo, mimi ninaloomba Mhe. Mwenyekiti, tunakwenda vizuri, tumekuwa na muafaka kwa muda mrefu, sasa wenyewe tumekubaliana na nchi imetulia nasema mpango huu wa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya na Masheha, una hatarisha usalama wa nchi hii na tumechoka kukaa tukaendelea hivi Hewallah Bwana. Nahisi kama hatukuurekebisha huu mswada, tukaona kuwa haki inatendeka basi kuna hatari kubwa kuwa nchi hii tutaishia katika balaa.

Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mwenyezi Mungu atujaalie tuendelee katika demokrasia na sisi tuwe wakweli na tujuwe hii ni nchi yetu na tutaiwacha hapa hapa, kwa hivyo tufanye mambo yanayoelekea kwa maslahi ya watu wote.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, una dakika zako mbili kumalizia.

Mhe. Salim Abdalla Hamad: Mhe. Mwenyekiti, dakika mbili, haya. Kifungu cha 14(1), kinaeleza Mkuu wa Wilaya atakuwa mwakilishi mkuu wa serikali ndani ya eneo la mamlaka yake na atakuwa na kazi zifuatazo.

Moja ni kuhakikisha usimamizi wa sheria na amri katika Wilaya, hizi amri naomba nijuwe ni zipi. Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa nielezee mengi zaidi, lakini kwa sababu ya wakati naomba kumaliza kwa kusema; Mhe. Mwenyekiti, mswada huu kwa mimi ninavyouona ni mswada kandamizi, umetolewa wakati ndio kwa sababu mwaka 2015 ndio uchaguzi wanakuwa na pirika chungu nzima, kwa maslahi ya nchi hii Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba tukae tufikirie tunakokwenda, sivyo tutakavyokwenda tuiwache nchi katika hali ya utulivu. Kwa sababu hiyo, mimi sijaunga mkono mswada huu hata asilimia ziro, isipokuwa kwanza nipate maelekezo niridhike. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana kwa kunipa nafasi ya kuchangia mswada huu wa sheria ya kufuta sheria ya Tawala za Mikoa namba moja ya mwaka 1998.

Mhe. Mwenyekiti, naomba nianze mchango wangu katika kifungu cha 5(2), kumetajwa mtu anayepaswa kuteuliwa kuwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya. Mhe. Mwenyekiti, sifa zilizotajwa ni Uzanzibari na uzoefu, lakini katika zama hizi za sayansi na teknolojia huwezi hata kidogo Mhe. Mwenyekiti kuipuuza sifa ya elimu.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile kumetajwa Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya ni watumishi wa umma, sasa ikiwa ni mtumishi wa umma sifikirii kama anaweza kuteuliwa mtu huyu bila ya kuwekwa sifa yake ya elimu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, mimi nashauri sifa ya elimu ya Mkuu wa Mkoa iwe angalau Shahada ya Kwanza, na vile vile sifa ya elimu ya Mkuu wa Wilaya isipunguwe Stashahada.

Mhe. Mwenyekiti, nimeusoma huu mswada nimeona kuna kifungu kilichotaja sifa ya elimu ya Sheha ambayo iwe ni Kidato cha Nne, ingawa Mhe. Mwenyekiti Kamati imependekeza kama sifa hii iondoshwe. Lakini mimi ni miongoni mwa watu ambao nasisitiza sifa hii ibakie, wala sifikirii kwa sababu kuna baadhi ya wachangiaji wamesema sifa nzuri ni uadilifu na uaminifu. Lakini vile vile tujuwe kuwa mtu anaweza akawa na elimu hii ya Kidato cha Nne, lakini akawa ni mwaminifu na ni mwadilifu. Sasa sifikirii kama kumchukua mtu mwenye elimu ya Kidato cha Nne, sifa hii ya uaminifu na uadilifu itapotea, sio kweli kwamba watu waliokuwa na elimu ya Kidato cha Nne wote sio waaminifu au sio waadilifu. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti ni vizuri sifa zote hizi zizingatiwe.

Mhe. Mwenyekiti, kuna wengine wanasema hekima hawana. Ikiwa watu wote waliokuwa na elimu ya Kidato cha Nne hawana hekima basi kwa kweli nchi hii isingekalika. Wako watu wana hekima, ni waaminifu, ni waadilifu na ni elimu ya Kidato cha Nne wanayo. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti, namuomba Mhe. Waziri alizingatie hilo.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile hii sifa ya Sheha ya elimu ikiwekwa kwenye sheria na ni vizuri iwekwe, basi na hawa Wakuu wa Wilaya na Wakuu wa Mikoa hizi sifa zao za elimu ziwekwe kwenye sheria.

Jambo jengine ambalo Mhe. Mwenyekiti, naomba nilizungumzie ni mambo ambayo muda mkubwa yamekuwa yakijitokeza, na imekuwa ni uzoefu kwa Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuchanganya majukumu yao ya serikali na chama. Mhe. Mwenyekiti, hili limekuwa ni jambo la kawaida. Kuna baadhi ya Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya tunawashuhudia wakiwa na mambo matatu. La kwanza wakihudhuria na wakiishabikia mikutano ya vyama.

Mhe. Mwenyekiti, sifa nyengine ambayo wanayo baadhi ya watu hawa ni kuvaa sare za chama cha siasa mbele ya wananchi wanaowaongoza. Vile vile jambo la tatu mazungumzo yao ni kwenye maskani au mabaraza ya siasa. Mhe. Waziri kwa sababu katika hii sheria hakuweka zuio au kifungu kinachoonesha kama hii ni tabia inayokuwa haitakiwi kwa viongozi hawa. Kwa hiyo, naomba anipe ufafanuzi juu ya suala hili.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, kwenye ukurasa 204 kifungu cha 8 kinahusu uteuzi wa Sheha. Katika kifungu hiki Mhe. Mwenyekiti pameelezwa pia kama Sheha ni mtumishi wa umma na atakavyopatikana ni uteuzi kutoka kwa Mkuu wa Mkoa.

Mhe. Mwenyekiti, hapa ushauri wangu, ili kuondoa dhana ya kupendeleana na kwa sababu Masheha na watumishi wa umma, basi Sheria za Uajiri wa Utumishi wa Umma zitumike. Nadhani hapa wananchi wa shehia husika wangelitangaziwa kama kuna nafasi ya Sheha iliyowazi kwa sababu Sheha ni mtumishi wa umma na tunazo Sheria za Uajiri. Pia wananchi wanaotaka waombe na waeleze sifa zao.

Baada ya hapo, utaratibu wa usaili ufanywe na matokeo ya usaili apelekewe Mkuu wa Mkoa, kwa ajili ya kuteua. Mhe. Mwenyekiti, haya ndio tuliyoekewa katika Sheria ya Utumishi wa Umma.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza naomba unilinde kila mmoja anayo haki ya kuchangia na ikifika mtu kuchangia aseme analotaka. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe, tumuache Mheshimiwa Mjumbe achangie huu ni muda wake.

Mhe. Salma Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu, sasa niende kwenye kifungu cha 8 ambacho kimeeleza kwamba Sheha hatoteuliwa ikiwa hajafikia umri wa miaka 40. Mhe. Mwenyekiti, hili ni jambo zuri tena naliunga mkono sana, kwa sababu kuna hatari kumuweka Sheha aliyekuwa na umri wa miaka 18, watu wakikosana huko yeye akapata nafasi. Kwa hiyo, ninaipongeza sana serikali hapa.

Vile vile hawakuweka umri wa mwisho wa mtu kuwa Sheha. Mhe. Mwenyekiti, hii ni kwa sababu kuna shehia nyengine Masheha wake ni wazee wanaendea mkongojo na Sheria ya Utumishi wa Umma ina umri. Kwa hiyo, hapa pia ninamuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba atuekee umri wa mwisho wa mtu kuwa sheha.

Sasa naomba nizungumzie kuhusu sifa za Katibu wa Sheha, mimi binafsi sifa hizi ninazikubali. Lakini utaratibu wa uajiri, kwa mujibu wa Sheria ya Utumishi wa Umma ifuatwe na isiwe hawa wanapatikana kwa njia za ajabu ajabu. Mhe. Mwenyekiti, tumezoea Sheha Katibu wake huwa ni mwanawe na siku anayomaliza Sheha basi na Katibu pia kazi imemaliza na huu sio utaratibu mzuri.

Jambo jengine ambalo naomba nilizungumzie kidogo ni kifungu cha 14(1)(i) ambapo kimeeleza jukumu moja la msingi la Mkuu wa Wilaya ni kusimamia Mamlaka za Serikali za Mitaa. Mhe. Mwenyekiti, hapa panaonekana pana mkanganyiko, hivi vipi Mkuu wa Wilaya aingilie majukumu ya Serikali za Mitaa, nilidhani jukumu hilo ni la wananchi wenyewe kwa kupitia mamlaka zao.

Sasa iweje Mhe. Mwenyekiti, Serikali Kuu izisimamie Serikali za Mitaa. Pia ninamuomba Mhe. Waziri anifahamishe kwamba kulikuwa na umuhimu gani wa kuanzisha Serikali za Mitaa.

Katika kifungu cha 17(3) ambacho kwa marekebisho ya kamati kitakuwa ni kifungu kidogo cha (2) na kimeeleza hapa Katibu Tawala wa Wilaya na Wilaya Ndogo watakuwa na Mratibu wa Serikali za Mitaa katika mamlaya ya eneo lake. Mhe. Mwenyekiti, hapa namuomba Mhe. Waziri anipe ufafanuzi wa kifungu hiki, nini maana yake kazi hizi za uratibu ni zipi, je haitakuwa suala la kuziingilia Serikali hizi za Mitaa.

Kwa hivyo, hapa namuomba Mhe. Waziri kupitia kwako Mhe. Mwenyekiti, kwamba anifahamishe, kwa sababu nina wasi wasi hizi Serikali za Mitaa zitaingiliwa na kuyumbishwa.

Lakini Mhe. Mwenyekiti, kwa kumalizia kuna kifungu cha 21(2) kimetaja Wajumbe wa Kamati ya Maendeleo ya Mkoa. Mhe. Mwenyekiti, kifungu kidogo (g) kimeeleza kuwa Wakuu wa Idara za Serikali au Taasisi katika Mkoa watakuwa ni Wajumbe waalikwa.

Sasa hapa Mhe. Mwenyekiti, nina swali kidogo katika Mkoa huu wa Mkoa wa Mji Magharibu Wakuu wa Idara za Serikali nzima ndio walipo. Je, serikali hii ina idara ngapi au taasisi ngapi, nadhani kikao hicho Mhe. Mwenyekiti kitakuwa kama Kikao cha Bunge la Jamhuri. Hivi Mhe. Waziri, huoni kama kikao hicho itakuwa ni zogo. Kwa hivyo, hapa namuomba Mhe. Waziri kifungu hiki akitizame upya.

Pia ushauri wangu kila wizara ingeliwakilishwa na Mkurugenzi wa Mipango tu. Nadhani Mhe. Mwenyekiti ingelitosha na lile zogo lingepungua.

Mhe. Mwenyekiti, nakushukuru sana na siungi mkono hoja mpaka nipate ufafanuzi. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Salma Mohammed Ali. Sasa naomba nimkaribishe Mhe. Asha Bakari Makame na baadaye nitampa nafasi Mhe. Rufai Said Rufai.

Mhe. Asha Bakari Makame: Ahsante sana Mhe. Mwenyekiti, na mimi kwa kunipatia nafasi hii kuchangia mswada huu ambao ni mswada muhimu katika taifa hili la Zanzibar.

Vile vile Mhe. Mwenyekiti, nitaomba samahani kama nitasema maneno ambayo yatawakwaza watu katika Baraza hili. Mhe. Mwenyekiti, nilishangazwa sana kwamba sisi ndio watunga sheria na sisi ndio wasimamizi wa sheria pia ni watekelezaji wa sheria ambayo tunaitunga.

Sasa leo Mheshimiwa Mwakilishi mzima kusema mimi Sheha sitakafanya mikutano na nitakuja huko huko utakuja kuniona Mhe. Waziri, mimi limenisikitisha sana. Kwa kweli sisi tunatakiwa sheria hii tunayoitunga baadaye turudi kwenda kuisimamia na kutekeleza. Hivyo, kama wewe Mheshimiwa Mwakilishi mtunga sheria humu leo unazungumza maneno huko *serious* mimi hata sielewi.

Kwa hivyo, ninashangazwa kama kweli tunakusudia tuko *serious* katika mambo yetu hapa basi tuwe *serious* na wala tusiropokwe tu maneno ambayo hayaleti tija, hilo moja. *(Makofi)*

Jambo la pili, sisi hatukuja huku kujadiliana CCM na CUF, kujadiliana CCM na CUF tutakwenda kujadiliana kwenye viriri vyetu huko. Kwa kweli, sina uhakika na hakuna kitu kibaya kama dhana Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu huwezi ukasema kwamba Masheha wote ni wa CCM kwa dhana zako zinazokutuma wewe, dhana ni mbaya, yaani katika kitu kibaya basi dhana ni mbaya mno.

Mhe. Mwenyekiti, *Wallahi* ninajiuliza hivyo kweli Masheha wote ni wa CCM anayejuwa nani wakati kama una chama chako unakiweka hapa. Mhe. Mjumbe niachie niseme hapa na wewe omba nafasi uzungumze Mhe. Mwenyekiti nilinde hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Mjumbe, zungumza na kiti.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, nataka unilinde asinitupie maneno tu mimi sio mtoto mdogo hapa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan Hamad Omar, naomba tufuate utaratibu, muache Mhe. Mjumbe azungumze. Nakuomba uzungumze na kiti.

Mhe. Asha Bakari Makame: Mhe. Mwenyekiti, sifunui mdomo kwa sababu nastahi kikao hiki, kwa sababu sio kikao cha sokoni hili, isipokuwa hiki ni kikao cha kutunga sheria na wala tusijibizane maneno Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti: Sawa Mhe. Mjumbe, tuendelee.

Mhe. Asha Bakari Makame: Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti huwa ninashangaa kwamba sisi ndio walengwa na sisi ndio wasimamizi wale walengwa ambao wanalengwa katika sheria hii. Kwa maana hiyo, mtu kusema hapa kwamba Masheha wote ni wa CCM una dhana, ambayo ni mbaya Mhe. Mwenyekiti na wala usiwe na dhana. Sasa kama ingekuwa Masheha wote ni wa CCM basi tungestarehe sana sisi CCM, hilo moja.

Jengine Mhe. Mwenyekiti, nataka waelewe Waheshimiwa Wajumbe wenzangu, kwamba sisi tusingekuwepo hapa kama si Mapinduzi ya mwaka 1964. Kwa kweli, Mapinduzi ya mwaka 1964 ndio yaliyotukomboa sisi tukaweko humu kwenye Baraza lako hili tukufu na waliopindua wengine sio wasomi, isipokuwa wametuchukua na kutusomesha mpaka tumefika leo hivi, sasa huwezi ukamdharau mtu aliyekuwa hakusoma.

Kwanza hilo tulijue, kwamba wewe umesoma huwezi ukamdharau mtu ambaye hakusoma Mhe. Mwenyekiti, kwa sababu msohili ana lile, kama wewe una mabanda teletele yamekujaa, basi yule ambaye sio msomi anaweza akafanya vizuri zaidi kuliko wewe uliyesoma mabanda. Kwa hiyo, tusidharau wananchi wetu tukasema kwamba ni mambumbumbu nchi hii isingefika mpaka leo hivi, kwa sababu unapomdharau mwenzako, basi ujijue na wewe na utadharauliwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, naomba kutoa wito kwamba tusidharauliane kwa kupitia mpaka wa kwamba mtu lazima awe na mabanda yote ndio apate uongozi, kuna wangapi humu wametuchafulia, ambao wamesoma kindakindaki wametuchafulia, yaani wasomi wakubwa hao na hivi sasa hawajijui hahe hohe. *(Makofi)*

Kwa hivyo, usimdharau mtu ambaye humjui, nasema tena msihili ana lile, kama wewe umesoma zaidi basi yule ambaye hakusoma zaidi anaweza akakupita kwa mipango na kila kitu. Mhe. Mwenyekiti, nilisema hilo nilizungumze. *(Makofi)*

Jambo jengine Mhe. Mwenyekiti, niseme tu kwamba mswada huu una mambo mengi ambayo ni muhimu na umuhimu wa mswada huu wengine wanatetereka kwa dhana zao walizonazo. Kutokana na hali hiyo, ndio maana ikawa kila mmoja siungi mkono kwa dhana ambazo hazikuletei tija. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, sheria hii ndio inayopaswa kuondoa watendaji kwenye uwanasiasa, lakini wakati kile mtu ana dhana yake anayoifikiria yeye hatoamini. Hivyo, tunasema sheria hii ndio inayoondoa kwamba watendaji na tumepitisha kwamba mtu akeshafikia kima fulani asiwe mwanasiasa, ndio maana sheria hii tukasema inatakiwa ipitishwe, ili iweze kufanya kazi zake. *(Makofi)*

Hata hivyo, niseme kwamba mtu anasema kwamba Waziri na Mkuu wa Mkoa watampotosha Rais, hee! Jamani, basi kusingekuwa na uongozi tungemuachia Rais peke yake, yaani yasingekuwepo madaraka ya kugaiwa ngazi mbali mbali. Hivyo, kiongozi amemteua mwenyewe Rais, Mkuu wa Mkoa, Waziri wakae wapange na halafu wampotoshe Rais kweli inaelekea hiyo. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, narudia tena dhana mbaya sana, nitazungumza kisha narudia kwenye dhana kwa sababu ni mbaya sana. Kwa hiyo, naseme kwamba Sheha amepewa mamlaka yake na Mkuu wa Mkoa amepewa mamlaka yake, Mkuu wa Wilaya amepewa mamlaka yake.

Hivyo, sifikiri kwamba kama kutakuwa na sintofahamu ambazo ndizo zitakazoleta mtiririko wa kuwa nchi hii haina amani, si kweli, kwa sababu wao ndio wanaotakiwa kulinda amani ya nchi hii kwa mujibu wa dhamana zao wakishirikiana na vyombo mbali mbali ambavyo vinahusika, sasa leo tuseme kwamba wataleta nchi hii isiwe na, isipokuwa ni sisi wenyewe hatuna nia njema. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, kama sisi wenyewe hatuna nia njema tunaanza kupopotoana hapa, basi kazi kwetu, hivyo lazima tuwe na nia njema ya kupitisha sheria hii na kuifanyia kazi kwa mujibu wa taratibu na sheria zilizowekwa Mhe. Mwenyekiti. *(Makofi)*

Vile vile niseme tu kwamba Sheha hatotafuta watu akasema haya kanikamatieni fulani, kwa sababu Sheha ana uwezo wa kwenda Polisi tu na kusema mtu fulani ana matatizo haya na yale tena kwa ushahidi sio kwamba atambambikizia, hawezi kumbambikizia isipokuwa anao uwezo.

Kwa hiyo, naomba sana Mhe. Mwenyekiti, kwamba mswada huu tusiufanyie magube gube, kwa sababu ni mswada mzuri tena ni mswada ambao utatusaidia sisi wenyewe kutokana na zile taratibu ambazo wengine wanasema mimi naonewa hivi, mimi nafanywa hivi. Sasa watu wamepewa mamlaka kamili ya kufanya kazi zao, yaani wasimamizi sasa ndio sisi kuhakikisha kwamba haki inatendeka, lakini haki hiyo tusilalamike, isipokuwa tuache mswada huu upite vizuri na tukitoka hapa twende tukausimamie mswada huu au sheria hii, ili mambo yetu yaende sambamba. *(Makofi)*

Halafu ninasema Sheha ndio maana akatafutiwa Katibu, kwamba Katibu ndiye atakayeshughulikia yale mambo, lakini lazima Sheha awe darasa la kumi na mbili tusidanganyane; mtu amefanya kazi kama kiasi miaka hamsini uzoefu wa kila aina anao ukenda kwenye chama ana uzoefu, ukenda kwenye Serikali ana uzoefu, ukenda kwenye lolote lile ana uzoefu halafu mimi niseme huyu mtu afike chuo kikuu, uzoefu wote aliokuwa nao afike chuo kikuu kuna mambo mengine ya utendaji ndio tuwape madaraka ya kuwa awe na shahada, awe na PhD awe na nini yale mambo ambayo ya utendaji hasa katika Mawizara. Lakini mambo mengine tuwape nafasi wananchi wetu na wao wajisikie kwamba hii ni nchi yao Mheshimiwa Mwenyekiti tusiwabeze, kwa kweli leo mimi nimesikitika sana kusema humu watu ni mambumbumbu.

Wewe kama Mwakilishi umehakikisha vipi jimbo lako watu waliokuwa wasomi wamesoma mpaka angalau darasa la saba au la nane, wakati hiyo ni kazi yako umehakikisha vipi kwamba watu wako wote wanajua kusoma na kuandika, na sio kujua kusoma tu na kuandika mpaka uwafikishe yale malengo ambayo unayataka wewe yatekelezwe. Lakini wewe mwenyewe hushughuliki, wakati taratibu sheria zipo tumezitunga sisi wenyewe za kuwapeleka watoto wetu maskulini tusifanye mashara Mheshimiwa Mwenyekiti, tuamue mambo ambayo yatatusaidia na hayatotusaidia sisi, sisi tumekwisha yatawasaidia vizazi vyetu vijavyo sio sisi, sisi tunawatandikia *red carpet* vizuri ili wakija wao wajue nini la kufanya.

Mhe. Mwenyekiti niseme tu kwamba mimi nimeingia kidogo kama watu walivyosema mimi nina wasi wasi kwamba sisi ndio viongozi wa nchi hii lakini tunatia gati gati kwa dhana, narudia tena dhana ni mbaya ukimdhania mwenzio ukamnyooshea kidole hivi ujue hivi vingine vinakuelekea wewe ujiulize je wewe una nini ushanifahamu Mheshimiwa, kwa hivyo mimi nawaomba waheshimiwa tunapokuwemo humu tusifanye masihara, tuwe *serious* na mambo yetu tuikosoe Serikali pale ambapo tunahisi hapa kweli inataka kukosolewa tusiikosoe kwa jazba, jazba haijengi Mheshimiwa Mwenyekiti. Jazba haijengi hata kidogo.

Baada ya kusema hayo mimi nasema Mswada huu ni mzuri na niwaombe wajumbe wenzangu tuupitishe na utapita, ili baadae tuende tukaufanyie kazi vizuri, baada ya kusema hayo Mheshimiwa Mwenyekiti, naunga mkono mswada huu mia kwa mia ahsante sana.

Mhe. Rufai Said Rufai: Mhe. Mwenyekiti, kwanza sina budi kumshukuru allah kupata nafasi hii wakati huu na mimi kutoa mawazo yangu machache katika mswada huu wa Sheria ya kufuta sheria ya Tawala za Mikoa namba 1 ya mwaka 1998 na kuanzisha upya Sheria ya Tawala za Mikoa kwa mwaka 2014 na mambo mengine.

Mhe. Mwenyekiti, huu mswada mwenzangu asubuhi mmoja kasema hapa kwamba ni mswada mmoja ukiuona ni mdogo sana vifungu vyake havizidi 34 lakini yaliyomo ni makubwa na mazito sana, iwapo kwamba sheria hii itatekelezwa kama ilivyo basi ni sheria ambayo itakuwa ngumu kiasi fulani. Kwa hivyo tusikae tukaona kwamba kila kitu ni rahisi tu hapana hichi ni kitu kimoja kigumu na kinaweza kikaja kikachafua hali ya hewa tuliyonayo hapa Zanzibar Mungu atupishie mbali.

Mhe. Mwenyekiti, nianze mchango wangu katika kifungu cha nane uteuzi na sifa za sheha katika sifa saba kama sikosei zilizopo pale na mimi niunge mkono mjumbe mmoja kachangia katika (c) pale katika muda wa kuteuliwa mtu kuwa sheha, na mimi nahisi kwamba miaka kumi na tano haitoshi tuongeze tena mitano angalau mtu aishi katika Shehiya hiyo asipungue miaka 20 pale. Kuishi miaka ishirini pale Mheshimiwa Mwenyekiti, shehiya inawezekana isipungue vijiji viwili na vijiji kuna uwezekano watu hao watakaoteuliwa kwa miaka kumi basi anashindwa kuwafahamu watu waliomo katika vijiji vile vitakavyounda shehiya, lakini kama huyo mtu ameishi pale kwa muda wa miaka ishirini atakuwa na uwezo mkubwa na ufanisi wa kuweza kuijua mipaka katika shehiya yake na idadi ya watu waliopo pale na wale ambao si wakaazi wa shehiya ile, kwa hivyo ukiongeza miaka mitano itakuwa tumempa nafasi nzuri yule mwananchi wetu atakayeomba nafasi hii ya usheha.

Lakini pia Mheshimiwa Mwenyekiti tukitaka tusitake suala la elimu ni suala la umuhimu mno tukitaka tusitake, kitu chochote kinahitaji elimu kila kitu kinahitaji elimu na wakati sheha ni miongoni mwa watumishi wa umma kuwa na elimu ya kuanzia kidato cha nne hii ni haki yake kabisa, wako wengine si Masheha lakini ni wafanyakazi wa Idara mbali mbali hawana elimu ya kidato cha nne, pengine wengine wametokea darasa la nne la zamani au la hivi sasa lakini wanafanya kazi katika Serikali. Lakini kazi ya kuongoza watu inahitaji mambo mengi lakini katika hayo mengi moja wapo ni hiyo elimu, na katika ufanisi wowote Mheshimiwa Mwenyekiti, wewe ni kiongozi lakini walio chini yako wamekuzidi taaluma hili litakuwa ni tatizo sugu hata zile amri zako zinakuwa wale wafanyakazi wako wanakuwa hawazijali vizuri kwa kitu kimoja tu kwa sababu wamekuzidi taaluma.

Kwa hivyo tusimfanye sheha akawa hana elimu mimi bado nasema mabadiliko yaliyokuwepo mwanzo basi tuweze kuyaachia yaendelee na masheha wawe na taaluma hiyo, lakini kifungu hichi hichi cha 4(3) naomba nipate ufafanuzi. Hiki kifungu kinasema kwamba kutakuwa na Naibu Sheha katika kila shehiya ambaye atateuliwa na Mkuu wa Wilaya kutoka miongoni mwa Wajumbe wa Baraza la Ushauri na Shehiya, baada ya kupokea pendekezo kutoka kwa Mjumbe wa Baraza la Shehiya husika. Naomba nipate ufafanuzi hapa Mheshimiwa mwenyekiti kupitia kwa Waziri.

Hili jina la kuwa naibu wa sheha katika Baraza lile litakapoteua huyo mtu mmoja lipendekezwe lipelekwe la nani, lipelekwa huyu mtu au huyu katibu wa sheha ndiye aliye na jukumu hili la kupeleka jina lile kwa Mkuu wa Wilaya, naomba nipate ufafanuzi hapo. Lakini pia katika kifungu hichi tunayo (5) kwa mujibu wa masharti ya sheria ya utumishi wa umma na kanuni zake, Mkuu wa Mkoa atamthibitisha na kumteua kaimu sheha kuwa sheha. Mheshimiwa nina tatizo hapa naomba nipate maelezo vile vile inawezekana katika kupata ukaimu wa sheha kwa sababu sheria hii inasema kwamba sheha kama atakuja kupata maradhi au kuumwa na mambo mengine huyu kaimu ndiye anayeweza kuja kuwa sheha, lakini katika hizi sifa alizopewa sheha, lakini katika kumpata kaimu hazikuzingatiwa hizi sifa za sheha lakini sheria hii sisemi kwamba naibu sheha kama sheha atapata matatizo naibu ndio atakuja kuwa sheha kuteuliwa na Mkuu wa Mkoa.

Kwa hivyo hapa pia nilikuwa naomba nipate maelezo vizuri inawezekana naibu sheha wakati kapata nafasi ya unaibu sifa hizi zote hizi hazikuangaliwa, lakini akaonekana ni mtu mzuri pengine hata miaka 40 hajafika lakini kapata unaibu wa sheha, pengine uadilifu ni mdogo kwake lakini kapata unaibu sheha, lakini pia sheha wake kapata matatizo huyu akafariki au kapata maradhi mengine au jambo jengine lolote. Kwa sheria hii inavyotuelekeza ni kwamba Mkuu wa Mkoa baada ya kukaimu ndio atakayeteuliwa kuwa sheha. Mimi hapo naomba kwamba tufanye mabadiliko asiwe aliyekaimu kuwa apate uteuzi huu wa kuwa Sheha, ila tu tuseme kwamba kwa mujibu wa masharti ya Sheria ya utumishi wa umma na kanuni zake Mkuu wa Mkoa atamthibitisha au kumteua Kaimu Sheha au mtu mwengine kuwa Sheha kwa sababu inawezekana huyu kaimu baadhi ya sifa za Sheha akawa hakuzitimiza, sasa ikawa sheria ishatubana. Kwa hivyo katika watu hawa wa Baraza la Sheha iwe mtu mwengine kutokana pengine na hawa hawa aliyetimiza hizi sifa aweze kuwa Sheha wa Shehiya hiyo.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu napenda niendelee katika kifungu cha 13 kinachozungumza mamlaka ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya, lakini pia Mhe.Mwenyekiti katika sifa hizi za Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya wakati hawa ni miongoni mwa watumishi wa umma sifa ya elimu kwao ni lazima kuwepo. Sheha tumemuwekea lakini Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya hastahiki aa hii itakuwa hatujawatendea haki. Ni lazima tuweke sifa ya elimu kwa viongozi wetu hawa wakuu wa Wilaya na Mkoa, kama tumesema kwamba huyu asipungue kidato cha nne hii jamani sheria na sheria ni msumeno, isiwe wengine inawakwereza wengine haiwakwerezi hapana bwana, Wakuu wa Mikoa na Wakuu wa Wilaya kuwe na kiwango chao cha elimu kama viongozi wengine wa umma walivyowekewa viwango hivi.

Mheshimiwa Mwenyekiti, nikiendelea Mamlaka haya ya Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kifungu (a) kinasema hivi yaani namba 13(1) kinasema:

> "Mkuu wa Mkoa anaweza kutoa amri ya kukamatwa mtu yeyote endapo ana sababu za kuamini kwamba;
> (a) mtu huyo anaelekea kuvunja amani au kuchafua utulivu wa wananchi.

Mheshimiwa Bi Asha hapa amesema dhana kitu kibaya lakini na hii sheria hapa imejenga dhana, hii sheria hapa imejenga dhana mtu huyo anaelekea kuelekea si kitu ambacho huna uhakika nacho sasa hapa tunaanza kujengeana dhana mbaya na tukianza kujengeana dhana ni kweli kwamba Magereza yatakuwa madogo, Polisi zitajaa kwa sababu tayari tunaanza kujengeana dhana mbaya. Kuelekea hasa kufanya hata Mungu amemsamehe mtu aliyekuwa ana malengo kufanya baya lakini ameelekezwa kulifanya hamsubiri vile anaelekea mpaka alifanye ndio anaanza kumtia adhabu.

Lakini sisi binaadamu leo kuelekea tu mtu umemuona ameelekea kwenye mlango ule sio useme kwamba kaingia mule anaweza akaelekea halafu akapinda njia nyengine bila ya kufika pale, sasa tukaanza kuelekezana huko hii ni dhana. Mheshimiwa mimi hichi kifungu hapa nataka kifanyiwe marekebisho, tusianze kutuhumiana vibaya kwa hivyo ni lazima hapa tufanye marekebisho dhana haitotupeleka pazuri itakuwa hapa Serikali ndiyo iliyoanza kuondosha utulivu wa nchi na kwa wananchi.

Waheshimiwa kama tunavyofahamu mtu anapata wadhifa fulani wa umma kuna watu kazi yao kupeleka majungu tu, kumpikia majungu mtu mwengine na yule kumpikia mwengine kwa hivyo tayari watu kupeleka majungu akipewa Mkuu wa Wilaya atoe amri mkamate fulani bila ya kufanya uchunguzi kutokana na suala lile, hili linaweza kuiweka nchi pabaya kutokana na kudhani tu kwamba tokeo hili lipo. Kwa hivyo ningeomba hichi kifungu Mheshimiwa Mwenyekiti kifanyiwe marekebisho.

Mheshimiwa Mwenyekiti, katika kifungu hicho hicho 13(4) kuna maelezo hapa yanasema kwamba: "Mtu aliyekamatwa chini ya kifungu hiki kwa haraka iwezekanavyo ataachiwa au kupelekwa Mahakamani au kwa

vyovyote vile hatawekwa kizuizini zaidi ya masaa 24 chini ya amri ya Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya. Mheshimiwa naomba nipate ufafanuzi. Mara nyingi Serikali sehemu za Mahkama zinafanya kazi kuanzia Jumatatu hadi Ijumaa. Lakini watu katika maisha yao wanafanya shughuli zao nyakati zote. Inawezekana mtu kafanya jambo akaonekana kwamba kweli amefanya tatizo lakini tatizo lake kalifanya Ijumaa saa 10.00 za jioni kafanya tukio na sheria ishasema asiwekwe kizuizini zaidi ya masaa 24 afikishwe Mahkamani, lakini Jumamosi hakuna Mahkama Jumapili hakuna Mahkama. Je, mwananchi huyu tutakuwa tumemtendea haki kiasi gani kuweza kuwekwa kizuizini muda wote huo. Hapa naomba nipate ufafanuzi mzuri sana.

Mhe. Mwenyekiti, kuna kifungu cha 18 kazi na majukumu ya Sheha, kila Sheha atawajibika kwa Mkuu wa Wilaya sawa lakini kifungu cha 2 kila Sheha atakuwa na dhamana katika eneo la mamlaka yake kufanya majukumu yafuatayo. Tusome (c) katika majukumu ya Sheha:

> "Kuweka kumbukumbu za nyaraka zote zinazohusiana na usajili, usajili wa ndoa, talaka, vizazi na vifo, vibali vya ngoma, usafirishaji wa mazao, mifugo, vibali vya mkaa na mambo mengine."

Waheshimiwa wenzangu wamesema kwamba Masheha nyumba zao ndio Ofisi zao hawana Ofisi za kuweza kuhifadhi vitu hivi na Masheha wetu wanazidiana kiuwezo. Kuna Masheha wengine nyumba zao dhaifu sana na hivi sasa kuna mambo mengi yanataka kutiwa na majukumu yote haya yanamuangalia Sheha.

Sasa Mheshimiwa katika mambo yote aliyopewa Sheha lakini bado nasema mambo ya ndoa na talaka zisiwe kazi za Sheha. Kazi hizi ni mambo ya kidini kwa hivyo wahusika wa dini mambo haya wayasimamie, ikiwa mtu muislamu, ikiwa ni mkristo akiwa ni nani lakini masuala ya ndoa ni masuala yamo katika dini. Kwa hivyo tusianze kuikimbia dini na wakati Serikali haina dini lakini wenye nchi wana dini zao na hawa Masheha hili linaweza kujakuwa ni tatizo kubwa, wanaweza kugombana mtu na mke wake lakini mke akamwambia bwana mimi sirudi nyumbani kwa sababu kanambia nikirudi nyumbani atanichinja huyu. Sheha akasema wewe bwana nenda zako kwako huyu mke atalala hapa, hilo ni tatizo. Ni lazima mambo haya ya ndoa na talaka wapatikane watu wenye hekima za kidini ili waweze kusimamia mambo haya. Sikatai Sheha kuweka kumbukumbu si mbaya kabisa kuweka kumbukumbu lakini na watu wanaohusiana na mambo ya dini nafasi hii tuwape wenyewe ili kuondosha migogoro katika jamii zetu.

Lakini pia katika kifungu cha (e) Mhe. Mwenyekiti, kuna kupokea taarifa za kufanyika kwa mikutano ya hadhara kutoka mamlaka husika. Mheshimiwa hii ni kazi moja kubwa mno, mimi ninahisi kwamba utaratibu tulionao bado tuuache uendelee tumeshasoma tokea kuanza vyama vingi vya siasa hadi leo tulipo hapa tuna karibuni miaka 20 na zaidi, tumeshaona utaratibu wa nchi wapi sasa imefika. Kwa hivyo tusitafute njia nyengine za kuja kuchafua amani tuliyonayo ni vyema utaratibu tulionao kifungu hiki tukifute tuendelee na utaratibu tulionao ili kuijenga vizuri nchi yetu kuzidi kuwa katika amani.

Kwa hivyo Mhe. Mwenyekiti, kwa upande wangu nilikuwa niyaseme hayo na mimi nitaunga mkono pale nitakapopata maelezo ya kina kabisa yatakayonituliza moyo wangu ili kuona kwamba sheria hii haikuletwa haraka haraka kama ilivyokuja, bali ni kuijenga nchi yetu vizuri. Ahsante Mhe. Mwenyekiti.

Mhe. Abdalla Mohammed Ali: Mhe. Mwenyekiti, mimi nilikuwa nisizungumze sana leo au sitaki nizungumze sana lakini kuna sababu mbili tatu zimenifanya na mimi nisimame hapa niseme machache. Mhe. Mwenyekiti, sisi wengi katika Baraza hili ni waislamu na kitabu chetu kinachotuongoza ni kur-an. Na kur-an imetusifia sisi binaadamu kwa sifa tofauti, kuna wanaotaka na kuna wasiotaka lakini ukweli ni huo. Na moja kati ya sifa tulizopewa sisi na Mwenyezi Mungu ni udhaifu, akatwambia kwamba sisi ametuumba tukiwa ni dhaifu. *Wakhulikan insana au inasanu dhaifa* hilo tusikatae.

Lakini pia akatwambia kwamba katika kutuumba sisi ametuweka magurupu tofauti, kuna wanaofahamu na waliokuwa hawafahamu, kuna aliowapa elimu na aliowazidishia elimu. Kwa hivyo hilo kama mtu anataka hiari yake, hataki hiari yake hailazimishwi. Lakini hicho ni kitabu kama ni muislamu tunatakiwa tukifuate. Kwa hivyo uwepo wa elimu haukuanza leo umeanza tokea karne hizo na naomba nikumbushe tu kwamba mtu wa mwanzo ni Mtume Muhammad *Sallallah Alayhi Wasalaam,* yeye katika kushushiwa kazi kwanza alisomeshwa ili apate kufanya ile kazi yake kwa uadilifu, hakupewa tu akaambiwa wewe nenda kawalinganie watu aliambiwa *iqra* baada ya kusoma *Bismillahi Rahmani Rahiim,* sasa kama anatokea mtu anabisha hilo huo ni utashi wake. Lakini hivyo ndivyo tunavyoongozwa na kitabu chetu kitukufu.

Mhe. Mwenyekiti, wengi wamezungumza kuhusu Sheha na mimi nitasema hapo hapo kuhusu Sheha kwamba kulikuwa kuna kifungu na naona Serikali ilijua ikakiweka kifungu hiki kwamba Sheha awe na taaluma fulani na hili ilifanywa kwa makusudi kwa sababu kama hujasoma kama huna maarifa si kweli kwamba utafanya kazi zako kwa uadilifu. Lakini kwa mshangao kwamba kifungu hiki kimefutwa. Sasa nashangaa mimi leo tunatakiwa tuongozwe na mtu ambaye maarifa yake ni madogo tukitaka hilo usitake hilo ni lazima hivi sasa kwa karne tunayokwenda basi tutafute watu ambao wana taaluma.

Mimi binafsi nilipokuwa najifunza komputa nilipata tabu sana lakini baada ya muda mtoto wangu akanambia tulia baba mimi nitakufundisha na hivi sasa mambo mengi ninayoyapata yanapitia katika mitandao. Na nina imani kwa karne tunayokwenda Mhe. Mwenyekiti, itabidi mambo mengi ambayo yanapitia kwa Sheha yapitie katika taalum hizo katika mitandao hiyo ya kisayansi. Sasa ikiwa tutatafuta mtu tu huko aje akae pale aambiwe wewe Sheha uongoze watu ambao wengine watakuwa ni wataalam, Mheshimiwa hapo tunavunja taratibu na huyu atalalamikiwa kila siku na wananchi lakini sasa hebu tumpe mtu ambaye atakuwa anaongoza tukifate hiki kitabu chetu kituongoze kidogo, kwa nini hatutaki kukifuata. Tumeambiwa hivyo aliyesoma na asiyesoma watakuwa sawa, hawawi sawa. Sasa kama si hivyo basi tufuate haya mambo ambayo tumeletewa, leo unakwenda kusema Sheha asiwe hivi, umesahau kwamba wewe umetakiwa uwe hivyo na wewe umetakiwa usome ujifunze.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba Mhe. Waziri hili alione kwamba kwa hivi sasa tunatakiwa tuwe na watu ambao tutawaita katika semina watafundishika, tutawaita katika mafunzo tofauti watafahamu. Sasa leo unakwenda kuchukua mtu ambaye utamwambia andika, hajui kuandika kweli hapo semina itakuwa. Kweli lile lengo la Serikali Kuu litapatikana, Mhe. Mwenyekiti, sasa hapa ndio tunapojenga mawazo kwamba hivyo mswada huu umekuja kwa lengo hilo. Kwa sababu kila kitu wazungu wanasema kuna *something behind*, nyuma kunakuwa na kitu. Sheria ukiisoma kwa juu juu unahisi ni nzuri lakini kwa nini tuweke vigezo kama hivi ambavyo wengine vinatupa mashaka. Mhe. Mwenyekiti, naomba Waziri hilo alione na aone kwamba sisi tumeshaondoka ile karne ya ujinga.

Mhe. Mwenyekiti, nilisema sitaki kusema sana lakini nakuja tena kidogo katika kipengele kinachompa madaraka Mkuu wa Mkoa na hiki kinasema kwamba:

> "Mkuu wa Mkoa anaweza kutoa amri ya kukamatwa mtu yeyote endapo ana sababu za kuamini kwamba," zimeletwa hapo chini.

Mhe. Mwenyekiti, tupo karne nyengine naomba nitoe mfano kwa sababu Mwenyezi Mungu ametuusia kwamba tutoleane mifano ili tupate kufahamu zaidi. Katika nchi ya Misri alikuwepo Mfalme anaitwa Firaun. Mfalme huyu aliambiwa na washauri wake kwamba atazaliwa mtoto katika nchi hii na mtoto huyu atakuwa mwanamme na mtoto huyu ndie atakayekuja kukuondoa wewe katika madaraka. Matokeo yake mfalme huyu akaichukua fikra hii na alipoifanyia kazi ikawa kila mtoto anayezaliwa mwanamme anachinjwa kwa maana ya kwamba asije akafikia hatua ile ya kumuondoa katika madaraka yake. Sasa huku aliyetuumba katwambia kwamba sisi alotuumba tukiwa dhaifu mtu anaweza akafanya jambo lolote, sasa mtu huyu ambaye Mkuu wa Mkoa hayumo katika vipengele hivyo yeye si binaadamu ambaye ameumbwa dhaifu naye hawezi akafikiria jengine akasema mimi aa kwa sababu nimepita pale nimefanywa hivi nifanye jambo fulani.

Mhe. Mwenyekiti, karne sio hii, hii ni karne nyengine ya watu wanaokwenda mwezini sayansi na teknolojia. Sisi leo tumetunga sheria hii tunasema kwamba tunaleta mswada wa kufuta sheria ya 1998 bado tunayaleta mambo yale yale ambayo yako *century* ya 17, tubadilike! Hatuwezi kwenda tena na mambo kama haya. Mkuu wa Mkoa amtie mtu ndani *why* Mhe. Mwenyekiti, hili nalo lionekane kwamba katika sheria ya kufutwa nalo lifutwe, sheria hii kama ni Rais apewe huko lakini Mkuu wa Mkoa *no* yeye ni mtu ambaye ni dhaifu kwa vile ana udhaifu atautumia udhaifu wake kwa kufanya anayoyataka na mfano mzuri ni kiumbe huyo ambaye alikuwa na ufalme wa nchi nzima lakini roho yake ikawa ni dhaifu waliokuwa wakizaliwa wote wanaume wakaamulia wachinjwe kwa kuogopa yeye kumuondoa madarakani. Je, leo Mkuu wa Mkoa?

Mhe. Mwenyekiti, karne hii haituruhusu tena na hapa ndio utatukuta kila leo tunatunga sheria lakini ukiangalia sheria hizi tunarejea yale yale ya nyuma tunasahau kwamba sisi tunatakiwa tubadilike, *mindset* yetu tui-*set* vyengine karne imeshabadilika.

Mhe. Mwenyekiti, labda la mwisho mimi nimuulize Waziri katika vigezo vyake vya kuanzisha Shehia amesema kwamba kutakuwa na idadi ya watu. Sheria ukiiweka hivi inakuwa inaipa fursa ya mtu kufanya anavyotaka,

ukisema idadi ya watu ni kigezo kimoja cha kuweka shehia lakini watu hao wangapi kwa nini usijifunge. Hebu twambie shehia itakuwa na idadi ya watu wasiopungua 400 sawa ili na mwenzako akija akitaka ku-*practice* jambo *100 years* au 50 years inayokuja na yeye itamfunga lakini leo unaweka wazi pengine kesho unaweza kuona aa mimi pale hebu nianzishe kijishehia fulani kwa ajili ya maslahi yangu. Sheria haziwekwi *loop hole* kama hizi zinatakiwa ziwe na mantiki fulani.

Kwa maana hiyo Mhe. Mwenyekiti, mimi ninahisi kwamba mswada huu una malengo fulani kwa hivyo siungi mkono hoja hii. Nakushukuru. *(Makofi).*

Mhe. Mohammedraza Hassanali Mohamedali: Mhe. Mwenyekiti, awali ya yote naomba kuchukua nafasi hii hatuna sote kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa kutuwezesha kutupa pumzi ambazo ndizo tulokuwa tunaringa nazo sisi waumini wote bila kujali rangi, kabila na dini.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza nichukuwe nafasi hii kumshukuru Waziri kwa kutuletea mswada huu, kuipongeza Kamati ambayo iliipitia mswada huu. Lakini vile vile Mhe. Mwenyekiti, labda niseme tu kwamba tuko hapa kwa maslahi ya wananchi lakini vile vile tuko *on trust*. Kwa hivyo mimi ningelipenda kuwaambia wenzangu kuweko na hekima na busara katika masuala yote ya kuendesha Serikali yetu ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa.

Mhe. Mwenyekiti, nilikuwa napitia mswada huu wa Sheha pamoja na Wakuu wa Mikoa na mambo mengine. Mhe. Mwenyekiti, sisi wawakilishi tuliokuwemo humu ndani ambao tunawakilisha wananchi wa Visiwa vya Unguja na Pemba kubwa zaidi kilichotuleta hapa na Katiba yetu inasema ni suala la kusoma na kuandika na kujua lugha ya Kiswahili. Lakini haikusema kwamba humu tuliokuwemo ndani tumefika form IV. Sasa Mhe. Mwenyekiti, kwa kuchukulia kifungu hiki cha ukurasa wa 204 kifungu cha 8 kusema kwamba Sheha awe amefika form IV ni lazima twende nalo kama tulivyokuwepo humu ndani sisi kama wawakilishi.

Lakini vile vile Mapinduzi yetu tumefanya mageuzi mengi, kuna watu walikuwa hawajui kusoma, hawajui kuandika lakini leo *alhamdulillahi* kidogo kidogo watu wameanza kuelimika, kujua kusoma, wamejua kuandika. Kwa hivyo mimi ninafikiri ningeliomba kwamba hili suala la kusema Sheha awe amefika form IV zito naona kwamba kwa kuwa tunakwenda huko basi isiwe kikwazo kwamba ikiwa sisi wawakilishi humu hatukuwa na vikwazo kuweka *form IV* tumekuja humu tunajua kuandika na kusoma basi isomeke kama Sheha awe hivyo hivyo kwa kusoma na kuandika. Sasa kama tunataka kupeleka *form IV* basi sisi tuje tuamue hapa tufike *form IV* halafu tuwapelekee na wenzetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini suala jengine vile vile kwa sababu sitaki kuwa msemaji sana, hili suala la sheha na la pili hili suala la Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kwenye kifungu cha 13.

Mhe. Mwenyekiti, nimesema lazima tuwe na *trust* na wenzetu Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya huteuliwa na Rais wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar chini ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa. Mimi nafikiri nasema kuweko na *trust*, sidhani wala siamini kama tulipo hapa duniani *we are in transit* awe Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya mwendawazimu wa kwenda kuchukua watu akawatia ndani, *I don't believe in*, hilo siliamini. Kwa hivyo, mimi ninachoomba kwamba tutoe nafasi hii kwa Mkuu wa Mkoa, Mkuu wa Wilaya nchi yetu imekuwa na demokrasia ya kutosha, kuna haki za kibinadamu, kuna sheria.

Kwa hivyo, mimi naona kwamba Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya naamini na wao vile vile watakuwa wana jambo vile vile kwa Mwenyezi Mungu kwa sababu wamekula kiapo, na vile vile ni *trust* lazima tuwe tunawaamini, lakini bila ya kuwaamini vitu vyingine vinakuwa havijengeki. Kwa hivyo, Mhe. Mwenyekiti naona mswada huu mimi kwa niaba ya wananchi wangu wa Jimbo la Uzini naunga mkono asilimia zaidi ya mia, na namshukuru Waziri kwa kazi yake nzuri na Kamati hii iliyosimamia. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Mussa Ali Hassan: Mhe. Mwenyekiti, ahsante kuweza kunipa nafasi ya kuweza kuchangia mswada huu kuhusu Tawala za Mikoa.

Kwanza nikiendelea nichangie Ibara namba 8 kama walivyochangia wenzangu wengi hasa sehemu hii ambayo ina mvutano mkubwa kwa jinsi ya uongozi. Ibara namba 8 inazungumzia sana kuhusu utawala wa Sheha wa Shehia, tunaelewa kwamba kila shehia sio sawa na jimbo au sawa sawa na Wilaya. Kwa kweli shehia inajuulikana kwamba

haitozidi watu wake kuwa zaidi ya 3000 au 5000, lakini katika Wilaya tunaelewa inaweza ikachukua watu 100,000 na kuendelea. Kwa hivyo, sheha anao uwezo wa kuongoza akijua kusoma na kuandika ili shehia ile si kweli kwamba watu wake wote inawezekana ikawa *form IV* na *form VI*. Ila shehia zetu watu ambao wana *form IV* hawazidi katika shehia moja watu zaidi ya 20 au 15.

Ukweli ni kwamba tukifuatilia masuala ya sheha, sheha hatotakiwa kuwa na kidato cha nne ama kidato cha sita kutokana na uongozi wake watu wake sio wengi kiasi hicho kwamba atatumia ajenda ya usomi hata ikafika kwamba watu wake hawatomfahamu. Tunakumbuka sisi umri huu tulionao hapo nyuma palikuwa na masheha ambao walionza mwaka 1960 mpaka mwaka 1962 au 1963 masheha walikuwepo na walikuwa hawana hata darasa moja na waliweza kuongoza shehia zao na wakati huo sheha ilikuwa anatakiwa sheha ambaye yule anaaminika katika kijiji ama ana heshima kubwa katika kijiji kile ndio sheha aliyekuwa anatakiwa, na ambaye alikuwa hapungui kuanzia miaka 50 na kuendelea. Hivi sasa sheha ameshushwa nafasi ya kuweza kuongoza hata akiwa na miaka 40.

Kwa hivyo, sheha wa uhakika ukweli anatakiwa awe anaweza kusoma na kuandika, na hii kusoma na kuandika ndivyo ilivyo Serikali yetu inavyoendelea. Hivi sasa tukikumbuka hayati Mzee Karume alisema kwamba nchi hii itaongozwa na wananchi kuanzia Serikali yake itaongozwa kuanzia darasa la sita, na itaongoza nchi na hivi sasa inaongozwa nchi hii tangu alipotoa historia hiyo kwamba darasa la sita wengi wao ndio wanaongoza Serikali hii na mpaka leo inaendelea kuongoza na tunaendelea vizuri. Na alijua kwamba Serikali itawekwa wasomi watupu kwa kweli haitoendelea na itakuwa na ubishani na wakati mwingi ikiwekwa wasomi watupu haitokuwa na uongozi, isipokuwa itaongoza siasa tupu hata mtu kama hahusiki na siasa atakuwa yeye anazungumzia siasa katika uongozi wake. Uongozi utashuka hadhi na itakuwa mara nyingi inazungumzwa siasa, ndio utaona sasa wasomi wengi wanazungumzia sana siasa kuliko uongozi. Kwa hivyo, mimi na-*support* kwamba alivyopendekeza Mhe. Waziri au ilivyozungumza Kamati kuwa sheha anatakiwa kujua kusoma na kuandika.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono kuhusu suala la Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya kuwa kidato cha nne na kuendelea, hawa inapaswa kwamba wawe wasomi kwa sababu sehemu yao wanaoongoza ni watu wengi na kila Mkoa ina wasomi wengi, ama katika Wilaya ina wasomi wengi. Hivyo anayeongoza Mkoa tunahakikisha kwamba ana kidato cha nne ama kidato cha sita ama anaongoza katika chuo. Na Mkuu wa Wilaya hivyo hivyo inategemea kwamba ni hakika awe na kidato cha nne ama chuo hiyo ndio sababu ya kwamba Mkuu wa Wilaya ana wasomi wengi na ndio anaweza kuongoza.

Mhe. Mwenyekiti, naunga mkono katika ukurasa namba 13 kuhusu suala la Mkuu wa Mkoa kuweza kuhakikisha kwamba anao uwezo wa kumuweka ndani mtu anapoamua yeye mwenyewe pamoja na Mkuu wa Wilaya kuwa ana uwezo wa kuweza kuhakikisha kumuweka mtu kwa maamuzi yake ya Mkuu wa Mkoa ama kwa vile ni Mkuu wa Wilaya. Kwa sababu sheria hiyo inamruhusu na uwezo anao na hilo ndilo litalosababisha nchi yetu mpaka sasa ndio ikawa ina utulivu na amani na inaendelea kuwa hivyo. Kama tutamshusha Mkuu wa Mkoa asiwe na uwezo kama huo kwa kweli nchi yetu itashuka amani na itakuwa hakuna uwezo wa kuweza kuwa nchi yetu salama kama ilivyokuwa hivi sasa.

Mhe. Mwenyekiti, suala la sheha nikiendelea ukurasa ule ule wa 18 yeye ni kuwa ana uwezo wa kuongoza kwa sababu hivi sasa utakuta masheha tulionao wengi wao tunapendelea sana kuwatafuta wale masheha ambao wana ukakamavu hasa waliotoka katika jamii ya askari, na askari mara nyingi ndio anayeweza kuongoza nchi hii. Nchi hii ni ya Kimapinduzi ni lazima iongozwe na maaskari ambao ni wastaafu ndio utakuta kwamba masheha wengi hivi sasa tumechukua wastaafu ndio wanaoweza kuongoza ndio utaona amani na utulivu unazidi kuendelea katika nchi yetu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea kuhusu suala la Mkuu wa Mkoa na Mkuu wa Wilaya anahakikisha anamchagua sheha wa shehia na yeye kupasishwa na Waziri mwenyewe. Hilo mimi naliunga mkono kwani hilo ni suala zuri na ni suala ambalo litatupa maendeleo ya kuhakikisha kwamba sheha wetu wanaochaguliwa ni wazuri ni sawa sawa kwamba wananchi hivi sasa wengi wanaokuja katika Baraza hili la Wawakilishi. Tunajua kuwa tumeweka sheria ambayo ndio endelevu hivi sasa mwakilishi anajua kusoma na kuandika ukichukua mfano mwakilishi wetu wa Micheweni hivi sasa tuna historia yake tunaielewa kwamba hana darasa hilo, lakini anaongoza na mpaka sasa hiki ni kipindi cha pili anaendelea kuongoza.

Sasa sisi wengine tunachoendelea ni kuhakikisha anajua kusoma na kuandika na wala hatujamfuta. Na ukitizama katika wawakilishi wengi ambao tulionao katika jengo hili hao ambao tunawategemea wanajua kusoma na kuandika

na hamna mwakilishi ambaye tumemuondoa katika Baraza hili kwamba hakufika kidato cha nne, tunao wengi na tunaendelea nao katika Baraza hili. Hivyo na sheha kusema ni lazima awe darasa la *form IV* hicho ni kitandawili ambacho kwa kweli kina historia ngumu na itakuwa ni siasa sio kweli kwamba tunataka uongozi. (*Makofi*)

Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mimi na-*support* sana sheha ajue kusoma na kuandika walioendelea hao wengine hao tunaweza kutafuta darasa na tukaendelea zaidi. Ni kama tulivyosema kuwa Rais ndiye aliyetakiwa ahakikishe ana chuo, ama ana *form IV* na kuendelea, lakini sio sheha. Mhe. Mwenyekiti, kwa kweli mchango wangu huu ni mdogo sana lakini ni endelevu sana nahakikisha kuwa suala la sheha liendelee kama lilivyo na naunga mkono Kamati kama ilivyoamua kwamba sheha ajue kusoma na kuandika kama walivyo wawakilishi hawa wa majimbo wanavyoendelea hivi sasa. Ahsante sana. (*Makofi*)

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, na mimi nakushukuru sana kwa kunipa nafasi hii kutoa mchango wangu na kwa siku ya leo sitokuwa na mchango mkubwa. Lakini baada ya kukushukuru wewe kwanza kabisa nimshukuru Mwenyezi Mungu Subhanah Wataalah aliyenijaalia pamoja na nyinyi kuwa katika hali ya uzima na afya inaturuhusu.

Mhe. Mwenyekiti, kwanza kabisa nakuomba umwambie Mhe. Mama yangu Asha Bakari Makame aniombe radhi kwa aliyonitamkia.

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nenda kwenye hoja.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Alinitamkia kwamba mimi ni mtoto, mimi sio mtoto.

Mhe. Mwenyekiti: Endelea na hoja baadae atajibu, endelea kwanza na hoja turudi kwenye mswada nakuomba. Mheshimiwa kaa tuendelee baadae tutayamaliza, sasa hivi naomba tuendelee na mswada kwanza.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, naendelea lakini bado mpaka uniweke sawa, aniombe radhi mama yangu ili tuendelee kukaa vizuri humu ndani ya Baraza, kwa matamshi aliyonitamkia narudia kusema tena sikuridhika na alivyoniambia.

Mhe. Mwenyekiti: Mhe. Hassan nakuomba uendelee na hoja, tuendelee na hoja iliyopo mezani tafadhali au utakaa chini.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Ukiniweka chini ni haki yako kwa sababu wewe ndiye Mwenyekiti na nitakutii kuniweka chini, lakini naomba aniombe radhi.

Mhe. Mwenyekiti: Sawa, sawa basi nakuomba uendelee na hoja.

Mhe. Hassan Hamad Omar: Mhe. Mwenyekiti, naendelea na mchango wangu.

Mhe. Mwenyekiti, amezungumzia kitu dhana na hii sio dhana wala ni utashi wa Waheshimiwa wanaozungumzia sio utashi, kwamba hawa masheha mimi nathubutu kusema kwamba wamewekwa kwa malengo maalum. Katika jimbo langu Jimbo la Kojani kuna shehia tisa, na masheha tisa nathubutu kusema mbele ya Baraza lako tukufu hakuna sheha hata mmoja aliyekuwa si CCM pamoja na Wajumbe wake wote. Na leo ndio maana haki haitendeki kwa sababu maamuzi yanatoka kwa upande mmoja tu kama amri.

Mhe. Mwenyekiti, zimezungumziwa sifa za sheha, sheha sifa zake zimezungumzwa hapa kwanza awe ni Mzanzibari. Lakini mimi katika hapa naomba yaongezwe maneno haya yafuatayo. Sheha atakayeteuliwa awe ni Mzanzibari wa kuzaliwa na sio *within ID.* Wenzangu wengi wamezungumza hapa kuna Wazanzibari halisia waliozaliwa hawana ID lakini kuna watu sio wazaliwa hapa wanazo ID, na hao wote wanaweza kuwa masheha. Lakini Mzanzibari halisi anaweza akaikosa hiyo nafasi kwa hivyo hapa tuweke kifungu hiki tuongezee hayo maneno hapa.

Mhe. Mwenyekiti, vile vile imezungumziwa kama sheha ni mtu wa kuheshimika, hili ni jambo jema kama kweli atahitaji kuwa na heshima lakini hata ukiwa mtu mzima kama hujiheshimu na wewe huwezi kuheshimiwa. Kwa hivyo, imezungumzwa neno uadilifu katika kifungu hiki cha 8 (d), ikiwa limezungumziwa neno “uadilifu” ni haki

na unapotoa haki utakuwa muadilifu, na ukatoa haki kwa upendeleo uadilifu haupo. Sote ni mashahidi hapa Mhe. Mwinyihaji Makame alipokuwa Waziri ya nafasi iliyochukuliwa na Mhe. Haji Omar Kheri tulikwenda tukamtaka hapo na akatukubalia ombi letu tukenda kukuta huko, tukasema sheha sasa hana nafasi ya kumdai mwananchi cheti, kama alivyodaiwa cheti atadaiwa mbele ya safari. Lakini hali kama hiyo mpaka leo inaendelea, si jambo zuri hivyo haki itolelewe kwa wote, haki asipate huyu na mwingine akanyimwa, hapo uadilifu haupo.

Hata Mhe. Haji Omar Kheri katika bajeti iliyopita tulimwambia bado wananchi wetu wananyanyaswa baadhi yao, na kwa sababu amekwenda Bunge la Katiba na amesharudi tunamwambia ile safari yetu iwepo twende akashuhudie kwa macho yake, kwamba bado wananchi wananyanyaswa na wanyanyasaji wakubwa ni hawa masheha. Leo unampa sheha rungu hii kama mtu ameitwa kwa sheha hajafika basi itafutwe sehemu ya kumuweka kizuizini kwa masaa sita, sote tutakwenda kizuizini kwa sababu hakuna sheha aliye na upendeleo na mwananchi wake, si wote.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu huo basi ingekuwa vyema hawa masheha kwa sababu mimi mwaka 1995 nilipokuwa diwani nilikuta hii sheria ya masheha hii. Sifa moja kubwa iliyokuwa ya masheha, sheha awe mpendwa na wananchi wake lakini nathubutu kusema sasa hivi hakuna sheha hata mmoja anayependwa na wananchi wake, labda baadhi yao kwa mambo wanayoyafanya. Niliikuta sheria ile inayozungumza sheha sifa kubwa awe anapendwa na wananchi wake, leo tunabadilisha sheria hii au tunaifuta sheria hii kwa kumpa rungu zaidi, ni tatizo.

Mhe. Mwenyekiti, sheria nzuri ni ile inayotekelezeka, sheria kama haitekelezeki ni matatizo sisi tunatengeneza sheria leo tuko madarakani hapa, na tunavyosema hadi tuone mbali, leo uko madarakani kesho hupo itakukumba hii. Kwa hivyo, tunapopendekeza mambo lazima yafanyiwe kazi sheria ikishapitishwa ni sheria kwa hivyo tufanye kazi kwa uadilifu kabisa ndani ya Baraza hili tukufu.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu katika kifungu cha 13 mamlaka ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya. Mamlaka ya Mkuu wa Mkoa na Wilaya katika kifungu hiki (b) mtu huyu amefanya kitendo chochote ambacho kinaweza kupelekea uvunjufu wa amani na kuchafua utulivu wa wananchi, na kwamba uvunjifu huo hauwezi kuzuiliwa kwa njia yoyote isipokuwa kumuweka mtu huyo kizuizini. Kile kitu nilichokataa kama ni dhana hii ndio dhana moja wapo, lakini hata hawa askari wetu Askari Polisi si lazima mamlaka haya apewe huyu Mkuu wa Mkoa au Mkuu wa Wilaya, Askari Polisi wakimuona mtu anavunja amani hawamuachii na hata huyo Sheha akisharipoti kwa polisi basi mtu anachukuliwa ndio tunavyokwenda kwa nini tuwanyime haki zao hawa polisi, hatujawatendea haki. Mimi naomba kifungu hiki cha (b) na (c) kiondolewe kifutwe kabisa, naomba sana kifutwe.

Mhe. Mwenyekiti, nikiendelea na mchango wangu katika kifungu cha 15(2), Mtu atastahiki kuteuliwa kuwa Katibu Tawala wa Mkoa. Zimeelezwa sifa hapa, kwa nini lile suala la kuwa Afisa Tawala limeondolewa, mimi naona ile Afisa Tawala imekaa vizuri kuliko Katibu Tawala tunaiga mambo lakini mambo mengine si mazuri. Mimi napendekeza hili la Afisa Tawala lirudi hapa hapa limekaa vizuri zaidi au ni sababu gani zilizopelekea kuliondoa Mhe. Waziri atupe ufafanuzi wa kutosha hapa.

Mhe. Mwenyekiti, kama nilivyosema mchango wangu mimi hautakuwa mkubwa lakini siungi mkono mpaka nipate ufafanuzi kwa haya niliyoyatoa, sitounga mkono mpaka nipate ufafanuzi kwa haya niliyozungumza. Mhe. Mwenyekiti, ahsante sana.

Mhe. Mwenyekiti: Nakushukuru sana Mhe. Hassan Hamad sasa tunampisha Mhe. Mahmoud Mussa na baada ya hapo mchangiaji wetu wa mwisho leo atakuwa Mhe. Abdi Mosi Kombo.

Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa: Ahsante Mhe. Mweyekiti, na mimi kunipa fursa ya kuweza kuchangia mawili matatu juu ya mswada wetu huu ambao unahusu Sheria ya kufuta Sheria ya Tawala za Mikoa Nam. 1 ya mwaka 1998 na kuanzisha upya Sheria ya Tawala za Mikoa ya mwaka 2014 na mambo mengine yanayohusiana na hayo.

Mhe. Mwenyekiti, nimekuwepo hapa toka asubuhi na nimefanya kazi kubwa sana ya kufuatilia mijadala ambayo ilikuwa inachangiwa hapa na Wajumbe mbali mbali. Mimi nikiangalia maana halisi ya madhumuni ya kuletwa kwa mswada huu nashindwa kuelewa wenzangu wameuelewa vipi mswada huu. Sasa labda Mhe. Mwenyekiti, mimi ninukuu madhumuni ya mswada huu kama ambavyo imeelezwa katika mswada huu ambao tumekabidhiwa.

Mhe. Mwenyekiti, mswada huu madhumuni yake ilikuwa ni kutunga sheria itakayoonesha kwa uwazi majukumu na muundo wa utawala wa mikoa, kazi na uwajibikaji ya kila ngazi ya Serikali Kuu katika ngazi ya Mikoa, Wilaya na ngazi ya Shehia. Lakini vile vile mswada huu ulikuwa na lengo la kuimarisha uhusiano kati ya Serikali za Mitaa na Serikali Kuu ya Zanzibar.

Pia sheria ya sasa ya Tawala za Mikoa haioneshi uajibikaji wa kila ngazi ya Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Hivyo basi, kupitia sera ya Serikali za Mitaa ngazi zote za Serikali Kuu zitabadilika kulingana na maelezo ya sera na kutekeleza sheria ipasavyo. Pia ngazi zote za Serikali Kuu zitashirikiana na kila moja wapo.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nikiangalia madhumuni hasa ya mswada huu sioni sababu tukaweza kufika pahala ambapo mpaka baadhi ya wenzetu wakatushangaa, kuona kwamba tumekuwa kama tunalumbana humu ndani tukafika pahala wengine hadi kutumia aya za Qur-ani katika kutoa mlinganio au ufahamisho bora juu ya suala hili.

Mhe. Mwenyekiti, hapa tuliwasikia baadhi yetu wakinukuu baadhi ya aya za Qur-ani zinazoelezea maumbile ya binadamu kwamba Mwenyezi Mungu amemuumba binadamu kuwa ni dhaifu. Haya yote yalikuwa ni katika kuhalalisha udhaifu wa kuweza kukaa katika nafasi fulani ya uongozi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nilihisi si jambo sahihi kuitumia Qur-ani katika mambo kama haya, kwa sababu kama tulifika pahala tukaona kwamba Mwenyezi Mungu amesema kuwa *Khulika-l-insana dhwaifa*, basi tusisahau kwamba Mwenyezi Mungu huyo huyo kwenye Qur-ani yake amesema: *Khulika- l-insana haluaa* vile vile. Kwamba Mwenyezi Mungu anasema kwenye Qur-ani nimemuumba Mwanadamu kuwa ni kiumbe kisichofahamika**,** *Idhaamasahu sharru jazuaa,* ukimletea shari utamuona anavyohangaika. Lakini hapo hapo *Waidhaa masahu khairu Manuwa***,** na ukimletea kheri anaing'ang'ania abakie nayo. Sasa hizi aya tuzitumieni vizuri jamani katika masuala yetu.

Mhe. Mwenyekiti, lakini zaidi ukiangalia kuna ambao walikuwa wametamka kwamba suala la Sheha kuja kupatanisha watu si katika majukumu yake wala halimhusu, si jambo ambalo linahusu masuala ya usheha, Sheha yeye ana mambo yake ya kidunia mambo ya kuweza kutoa talaka na mambo mengine mengine haya yako katika dini. Mwenyezi Mungu ametufahamisha kupitia kwa Mtume wake Muhammad (*S.A.W*) katika watu ambao wana daraja kubwa na watu wana fadhila kubwa ni watu ambao wamo katika mafungu matatu. Moja kati ya fungu hilo ni yule mwenye kuleta *islaha baina nnas*, yaani kupatanisha watu ambao watakuwa wana matatizo.

Sasa haya ni mambo ambayo tukimchukua kijana mfano tuseme wa *Form IV* hata mwanangu yuko *Form IV* Muhammed. Sasa hivi tukimchukua tukasema labda tumpe usheha kwa sababu amefikia *Form IV* je ataweza kuyakamilisha haya, hiyo ndoa haijui imekaa vipi, haya si mambo mazito? Lazima tufike pahala tutafute watu wenye busara, wenye hekima, wenye mawazo mazuri ambao wanaweza kutusaidia ili kuweza kusimamia mambo haya na yakaweza kwenda vizuri kama ambavyo ilikuwa imelengwa. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, mimi sikuwa na mengi sana katika kuzungumzia juu ya mswada huu, lakini zaidi naomba kwenda katika hiki kifungu cha 18 ambacho kwa leo niliona kwamba ndicho kimekuwa ni mada kubwa humu ndani.

Mhe. Mwenyekiti, mimi hapa katika kifungu cha 18 ninachokiona kikubwa ni kazi na majukumu ya Sheha. Jamani tusisahau kwamba Sheha huyu ana serikali yake na Sheha madaraka yake anafanya kazi za Rais katika shehia yake. Kule katika ngazi ya juu jamani tusisahau kwamba tuna Rais, lakini tukija katika mikoa tuna Wakuu wa Mikoa, tukienda katika wilaya tuna Wakuu wa Wilaya na tukishuka katika shehia tuna Masheha; hawa wote ni wawakilishi wa Rais katika maeneo yao kwa kila mmoja kwa ngazi yake ambayo amepewa. Sasa leo nambieni Sheha hana mamlaka ya kumfunga mtu sasa hivi? Wewe mwenyewe ukifika sasa hivi ukileta tabu kidogo Sheha ana uwezo wa kukushughulikia.

Sasa lakini pengine haya yalikuwa yanafanywa ilikuwa haijawekwa sheria ambayo iko wazi inatoa maelekezo na taratibu zake ziko vipi. Hapa kilichosababishwa na kuweza kuletwa leo na Mhe. Waziri wetu ni utaratibu wa kisheria tu ndio ambao umehalalishwa hapa ili suala hili liweze kwenda kwa mujibu wa taratibu. Leo tukifika pahala tukasema kwamba Masheha wote siwo, Masheha wote wamerubuniwa na serikali, jamani hawakuchaguliwa Masheha kutokana na itikadi za vyama wamechaguliwa kutokana na uwezo wao. Kuna wazee wetu wengine walikuwa Masheha hata mtiririko wa vyama vingi hakuna, wamekuwa Masheha babu yangu mimi marehemu alikuwa Sheha akastaafu, matokeo yake akaja akarejeshwa tena usheha mpaka mwisho ameukataa mwenyewe. Haya

mambo mimi nawaomba wenzangu tuyaangalie kwa vizuri tusifike pahala tukaweza kufanya vitu ambavyo havieleweki wala havifahamiki.

Vile vile tukizungumzia suala la elimu, watu wengi wanasema kwamba Masheha hawana elimu, masheha wana elimu bwana tena wana elimu ya dunia na wana elimu ya akhera, tena basi na kwa sababu ya kwamba elimu zao ni nyingi zimekwenda katika fani tofauti ndio maana Mwenyezi Mungu amewapa uwezo huo. Tukiwa tunazungumzia suala la elimu kuhusiana na Masheha tumtizame Mtume wetu *(S.A.W)* daraja yake aliyokuwa nayo na elimu aliyokuwanayo ni vitu viwili tofauti. Lakini ameweza kutuongoza na sote tukaweza kumfuata na mambo yote yakaenda vizuri na mpaka sasa hivi imekuwa yeye ni kigezo bora, tena basi sifa ya kuwa yeye ni kigezo bora sio kwamba ninatoa mimi, hata Qur-ani ambayo sisi tunaiamini na kuifuata inazungumzia juu ya ubora wa Mtume wetu Muhammad *(S.A.W)*.

Mwenyezi Mungu ameyathibitisha hayo katika Qur-ani yake aliposema kwamba: "Hakika yako wewe Muhammad ni katika mfano bora". Sasa jamani tunakwenda wapi, tunafanya nini. Nakuombeni sana hata maalim wangu huyo ninayemtaja ni maalim wangu mimi, kwa hiyo na yeye vile vile ana fani ambayo inaendelea mpaka leo. Nawaombeni sana wenzangu tufike pahala tuone kwamba kwa malengo ambayo nimekwishakuyasoma na madhumuni ya mswada huu sidhani kama mswada huu una matatizo kwa wale wote ambao walikuwa wanaitarajia nchi hii iweze kwenda vizuri kwa mujibu wa mambo ambayo tumejipangia. Naomba sana Wajumbe wenzangu wa Baraza la Wawakilishi tuliomo humu nakuombeni, pamoja na kwamba kuna wengine wamesema kwamba hawataunga mkono, hawatapitisha, hawatakubali nakuombeni sana tupitishe sheria hii na hatimaye tumpe uwezo Mhe. Rais ausaini mswada huu uwe sheria na baadae uweze kutumiwa na Inshaallah Mwenyezi Mungu atajaalia haki itakuwa inatendeka na batili itakaa pembeni. *(Makofi)*

Mhe. Mwenyekiti, baada ya maelekezo hayo kwa heshima na taadhima kwa niaba yangu na kwa niaba ya wananchi wa Jimbo la Kikwajuni naunga mkono hoja ya mswada huu kwa asilimia mia moja. Naomba kuwasilisha.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsane sana Mhe. Mahmoud Muhammed Mussa au nikuite Ustadh Mahmoud Muhammed Mussa. Sasa nimpishe Mhe. Abdi Mosi Kombo ambaye nafikiri atakuwa mchangiaji wetu, kuna mkono pale Mhe. Hussein Ibrahim nitagawa dakika saba saba kila mtu angalau achangie kidogo ili tufunge mjadala wetu mpaka kesho tukijaaliwa.

Mhe. Abdi Mosi Kombo: Ahsante Mhe. Mwenyekiti, kwa ruhusa yako na mimi namshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunijaalia leo hapa kwamba tuko wazima sote na tukafika kuchangia mswada huu ambao unatubainisha au unatufahamisha kwa uongozi wetu wa Serikali za Mitaa.

Mhe. Mwenyekiti, mimi nitaanza katika ukurasa wa 204 kifungu cha 8 kinachohusu uteuzi na sifa za Sheha.

Mhe. Mwenyekiti: Waheshimiwa Wajumbe tumsikilize Mhe. Abdi Mosi Kombo kumekuwa na zogo kidogo.

Mhe. Abdi Mossi Kombo: Mhe. Mwenyekiti, mimi mtu wa mwisho basi lazima iwe ni tatizo. Mhe. Mwenyekiti, wachangiaji wengi sana hapa wameshazungumza na wengi wamesema kwamba hawaungi mkono mpaka wapate maelezo sahihi. Lakini mimi kabla ya kumaliza naunga mkono mswada huu lakini naomba kidogo nikariri:

"Kutakuwa na Sheha ambaye atakuwa ni mtumishi wa umma atakayeteuliwa na Mkuu wa Mkoa kushirikiana na Mkuu wa Wilaya kuhusika na kushirikishwa na waziri kwa ajili ya kutekeleza majukumu na kazi zilizoainishwa na sheria hii au sheria nyengine yoyoe itayotumika Zanzibar".

Mhe. Mwenyekiti, hapa pana maelezo katika kifungu kidogo cha (2) kinachosema kwamba, mtu hatateuliwa kuwa Sheha isipokuwa kuwa ni Mzanzibari, mwenye kuheshimika, mkaazi wa shehia husika kwa muda usiopungua miaka kumi na tano, mtu aliyethibitika uadilifu. Halafu mwisho katika kifungu cha (2)(f) kinasema, Mwenye cheti cha Kidato cha Nne au zaidi.

Mhe. Mwenyekiti, mimi ninavyoelewa kwanza tukitafsiri neno Sheha, Sheha ni neno la Kiarabu linatokana na neno "Shekhe". Shekhe ni mtu mzima na Sheha wakati walipokuwa wakichaguliwa Masheha walikuwa wakichaguliwa kwa sababu ya utu uzima, mtu mwenye busara ameshafika kiwango cha kuwa ni mtu ambaye atakuwa ana akili tena mwenye kupanga na kuweza kueneza mambo kwa mpango na kuweza kumfahamisha kitu mtu akaelewa.

Sasa kitu kikubwa cha usheha sio kuwa na cheti, usheha akijua kusoma na kuandika tayari ameshakuwa Sheha, isipokuwa umri ndio unaomruhusu kuwa Sheha ni neno la Kiarabu. Sasa labda wengine hatujui hapa kwamba labda Sheha awe Rais, awe nani, hapana, neno Sheha ni neno la Kiarabu ambalo maana yake ni shekhe, ni mtu mzima. Kwa hivyo, Sheha anapendezwa achaguliwe mtu mzima mwenye busara na akili na hata Mtume wetu (*S.A.W*) ameanza kuteuliwa na Mwenyezi Mungu miaka 40 kwamba ametimia ***tahtimu l- baleghe*** lakini sasa hapa watu wanasema wewe huna cheti awe na cheti, ziko kazi za cheti kama daktari anaruhusika awe na cheti lakini sio usheha. Sheha atahitajiwa kusoma na kuandika tayari ameshakuwa Sheha na akishakuwa mtu mzima mwenye akili timamu utamchagua mtu miaka 18 hana cheti atamhukumu mtu gani. Sheha ni kazi ya busara, Sheha ni kazi ya ujitu uzima ndio maana yake.

Kwa hivyo, nawaomba Wajumbe tufahamu kwamba Sheha si lazima awe na cheti akishajua kusoma na kuandika basi anaweza kuwa Sheha.

Mhe. Mwenyekiti, mimi kwa vile Wajumbe wameshachangia mswada huu na washaufahamu mimi naimba tu, kwamba wale Wajumbe waliosema hawaungi mkono ni kwamba sisi hapa ni wawakilishi ni watunga sheria, sheria bora zikataliwe na wananchi kuliko sisi. Kwa sababu sisi ndio watunga sheria, sisi ndio wapelekaji wa sheria. Sasa kama sheria tunazipinga sisi hapa nani atazikubali? Kwa hivyo, nakuombeni Wajumbe nyote mswada huu ni mzuri umeeleza na hauna matatizo.

Mhe. Mwenyekiti, kwa vile mimi ni mtu wa mwisho kwa leo dakika zangu saba sitaki kuzimaliza nimpe mwenzangu Mhe. Hussein Ibrahim Makungu azimalize. Mimi naunga mkono mswada huu hauna matatizo. Mhe. Mwenyekiti, ahsante.

Mhe. Mwenyekiti: Ahsante sana Mhe. Abdi Mosi Kombo sasa Mhe. Hussein Ibrahim Makungu una dakika tano.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, nitazitumia hizo vizuri kidogo ili niweze kumaliza.

Kwanza nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kuwa sote tuko katika hali ya uzima na afya njema leo jioni hii.

Pia nikushukuru wewe Mhe. Mwenyekiti, kunipa nafasi hii ya upendeleo ya mwisho kabisa, nakushukuru sana.

Pia nimpongeze sana Mhe. Waziri na nimpongeze sana Mhe. Rais kwa kumchagua kuwa waziri wa wizara hii, kwani wizara hii anaiweza Mhe. Haji Omar Kheir imepata mtu ndiye na mahiri kabisa na umakini wake unaonekana kwa kazi yake nzuri kabisa. Mimi nampongeza sana Mhe. Waziri. (*Makofi*).

Lakini pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kumrejesha Mhe. Waziri wetu wa Fedha, tulikuwanaye China kwa kazi yake nzuri kwa anavyojitahidi kabisa kwa nia njema na nchi hii na mambo aliyoendea kule *inshaallah* Mwenyezi Mungu amjalie ile ndoto yake aliyokusudia basi iwe na tufanikiwe kwa maendeleo ya nchi yetu. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti, niingie kwenye Mswada huu kwa haraka haraka kwa sababu muda umekuwa mdogo, lakini nianze kwenye ukurasa wa 204 kifungu namba 8 (2)(c), Sifa za Sheha. Kwanza mimi nije hapa kwenye hiki kifungu namba 8(a) mimi napata wasiwasi mkubwa Mhe. Mwenyekiti. Huu Mswada wa pili unaandikwa Mzanzibari kwa nini hapa isiandikwe Mtanzania tuweke Mzanzibari. Mimi naona kama tunajiweka sisi mbele sana wale wenzetu wakija kuandika hivi Mtanzania au Mtanganyika wao wenzetu wanaandika Mtanzania lakini sisi tunaandika Mzanzibari na wao wakiandika Mtanganyika itakuwa sawa.

Mhe. Mwenyekiti, kidogo hapa akija Mhe. Waziri anambie kwa nini tunaweka Mzanzibari. Hatuoni kama sisi ni upendeleo au na ubaguzi fulani unatokezea baina ya Uzanzibari na Utanzania na Utanganyika na wao wakijiita Watanganyika itakuwaje hapa. Naomba Mhe. Mwenyekiti, sisi ni ndugu tujue tunavyoandika hapa na Mhe. Waziri anieleze akija, anifafanulie hii Mtanzania na Mzanzibari maana yake hali halisi inakuwa hivi?

Mhe. Mwenyekiti, nije kwenye kifungu cha 8(b) huyu Sheha awe ni mtu mwenye kuheshimika. Hili ni sawa na mtu mwenye kujiheshimu na mwenyewe anajua nini anachokifanya, mtu mwenye hekima na busara. Hili halina shida ni zuri kabisa kwenye Mswada huu na Sheha awe na sifa hiyo mwenye umri wa miaka 40.

Mhe. Mwenyekiti, mimi naomba huu umri wa miaka 40 tuuangalie kwa nini tusiweke miaka 35 hapa, Sheha kuwa tupate mtu kijana awe anaweza kwenda mbio kufanya kazi vizuri. Tukiangalia Masheha wetu wengi sasa hivi wazee wazee na pia tuweke muda wa kustaafu, pia tuangalie miaka fulani amefika astaafu yule Sheha.

Kwa hivyo, Masheha wengi ukiwatizama ni wazee, tubadilike sasa tuweke Masheha vijana waweze kufanya kazi kufatilia majukumu yao. Kama unavyojua Mhe. Mwenyekiti, Sheha ana kazi kubwa ukitizama sasa hivi kwenye Shehia zetu, Majimbo yetu Sheha anajua kila kitu ukimtaja mtu fulani Sheha anakwambia huyu anakaa sehemu fulani. Kwa hivyo, wanafanya kazi vizuri wanatambua, wanaelewa mambo mengi sana Masheha wetu. Kwa hiyo, naomba miaka hii Mhe. Waziri aiangalie ishuke kidogo iwe angalau 35.

Mhe. Mwenyekiti, niendelee haraka haraka kwenye kifungu 8(f) Sheha anatakiwa awe na cheti cha Kidato cha Nne. Mimi nasema hii si lazima kwa Sheha, kazi anayoifanya kwani hawa Masheha wetu ukitizama mpaka sasa hivi wametufikisha hapa miaka 50 leo hawana hata mmoja mwenye cheti cha Kidato cha Nne, lakini wanafanya kazi kwa nia njema, kwa nia safi kwa nchi yao na uadilifu wa mambo mengi mpaka tumeweza kufikia hapa leo miaka 50 Mhe. Mwenyekiti.

Mimi naona sifa hii isiwekwe haina umuhimu wowote, tukiangalia nchi hii kwa sifa zake wazee wetu waliopindua Mapinduzi ya nchi hii nani waliofika *Form IV* katika wazee wa Mapinduzi yale na wamefanya kazi nzuri. Vijana wa *Form IV* sasa hivi kazi ile kuifanya hawawezi, lakini hawa wazee wana nia njema bila ya kufika *Form IV* na hawana cheti Mapinduzi wameyafanya na mpaka leo matunda yake tumeyaona kwa Zanzibar. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa malizia una dakika mbili tu.

Mhe. Hussein Ibrahim Makungu: Mhe. Mwenyekiti, niseme kitu chengine kimoja, tunaweka huu uzito wa kuweka cheti cha *Form IV* lazima mtu apate. Sisi bado serikali yetu na wanafunzi wenyewe ukitizama wanafunzi hao hata kufika skuli wanashindwa kwa usafiri au kwa hali ngumu ya maisha. Ikiwekwa hii *Form IV* kwanza hawa wanafunzi hawafiki skuli kwa wakati tuangalie maisha yao tuwafikishe skuli kwa wakati, wasome baada ya miaka 50 ndio tuweke mtu afike *Form IV*. (*Makofi*).

Mhe. mwenyekiti, wako wanafunzi wengi wanataka kufika skuli kwa wakati, lakini hawawezi wana shida, wanataka kusoma lakini hawana fedha. Kwa hiyo, naomba sana huu ukomo usiwekwe. Nikitoa mfano mzuri hata Bungeni juzi ukomo wa Bunge uliwekwa afike *Form IV* lazima cheti, lakini ikaonekana sio muhimu kutokana na kuwa bado hatuwezi kuwapa wananchi wetu elimu ya kutosha kwa nchi yetu nzima. Kwa hivyo, tusiweke ukomo huu tuache hivi hivi ilivyokuwa sasa hivi mpaka ifikie miaka 50 mbele. (*Makofi*).

Mhe. Mwenyekiti: Mheshimiwa nakushukuru sana umeeleweka vizuri katika mchango wako na naomba radhi kwamba imebidi tukukatize, lakini na muda vile vile umefika wa kuakhirisha kikao chetu.

Waheshimiwa Wajumbe niwashukuru kwa utulivu wenu pamoja na michango yenu mbali mbali, natarajia leo tumemaliza michango kutoka kwa Wajumbe. Kwa hiyo, Mwenyezi Mungu akitujaalia kesho tunamsikiliza Mhe. Waziri katika Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais na baada ya hapo Mhe. Waziri mhusika mkuu atakuja kutujibu yale ambayo tumemuuliza.

Baada ya kusema hayo naakhirisha kikao hadi kesho siku ya Ijumaa tarehe 31/10/2014 saa tatu asubuhi.

(Saa 1.45 Usiku Kikao kiliakhirishwa mpaka tarehe 31/10/2014 saa 3:00 asubuhi)